

## **Msimulizi, 1892<sup>1</sup>**

Edited and corrected by  
Arvi Hurskainen  
Department of World Cultures, Box 59  
FIN-00014 University of Helsinki, Finland  
*arvi.hurskainen@helsinki.fi*

### **Abstract**

This is a corrected version of Msimulizi, the first periodical written and printed in Swahili language. The periodical was established to be an information channel between scattered mission station of the Universities' Mission to Central Africa, and also between the supporters of the mission work in Great Britain. The periodical was originally scanned and made available by SOAS (School of Oriental and African Studies, London). Obvious scanning errors were corrected. Also, clear errors in original print text were corrected. However, nonstandard spelling was not corrected, if it was possible to assume that the writer intended to write in the way it was done.

The file follows the original pagination. A page in the original publication is a page in this file. Page numbering is continuous from year to year, and it is printed at the top of the page.

This file contains the text of year 1892.

MSIMULIZI. 1892  
Imepigwa chapa Kiungani, Zanzibar,  
katika "Universities' Mission to Central Africa,"

---

<sup>1</sup> The text is issued under licence CC BY-NC

MSIMULIZI. 510

## **HABARI ZA MBWENI.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu. Baada ya salaamu nakuarifu kama siku ya December 20 tulikwenda Mkunazini kuwatazama Bev. W. M. Mercer na Rev R. A. Hood, wakipokea daraja la Ukasisi; sala zote zilipokwisha fanyika tukarudi zetu Mbweni.

December 21 ikiwa siku kuu ya Tomaso Mt. twalishinda hapa hapa nyumbani; ilipokuwa alasiri tulikwenda miembeni kucheza huko.

December 24 tulitengeneza nyumba tayari kwa siku kuu. December 25 ndiyo siku kuu ya Kuzaliwa, watu 169 walishariki hapa siku hiyo. December 27 tulifurahishwa na ngoma zilizochezwa shambani petu, Revnd W. H. Woodward akichukua watoto zamu kwa zamu, siku tatu palikuwa hapana kazi watu walicheza siku hizi zote.

December 31 ilikuwa harusi ya Herbert M. Feruzi na Rose Dunia, na Yakobo Chorola na Katharina Shanura, na Frank Dema na Kandake Kabutu, na Charles Masegwe na Florence Kachapao.

January 1, siku ya Tohara, watoto 15 walitiwa mikono katika kanisa la shamba; majina yao ni haya, Eleza M. Siwatu, Rhoda Mwajuma, Caroline M. Yasmini, Mattie Nzila, Paulina Yasmini, Etheldrida Kambachocho, Audri Kinzunza, Justina Tatu, Jenie B. Ngonzi, Anne Clayton Mahamla, Diana J. Kalele, Maiilda Nyamisi, Korale Urelia, Eunike Mwasuano, Lilian Zoe Kidala. Kenda walikuwa wa nyumbani, na sita wa shamba. January 1, alasiri ilifanyika kusanyiko la Chama ya Mchungaji aliye mwema, kwa kusudi ya kumwaga Mwalimu Faith Kayamba na mumewe, waendao Bonde kufanya kazi ya kufundisha. Walipiga magoti mathbahuni

## MSIMULIZI 511

wakapokea mbaraka na Kasisi Mr Woodward.

January 2, wakaja kanisani kwa Usharika Mt. baadaye walisafiri. Na January 7 tulikaribishwa Mkunazini na Miss Dean-Pitt, Bwana Askofu akatufanyia killa mtoto zawadi ya pesa, hivi tukanunua killa mtu kimpendezacho.

Siku hiyo twalitembea tu mchana kutwa madukani.

January 16 palikuwa na harusi ya mwalimu Manfred Manyula na Dorothea Nangambi, na Harold Ghechande na Mary A. Kalisha, na George Songolo na Veronica Chausiku. Sasa wamesafiri Magila, illa Mary Ashdon na mumewe wamekaa hapa.

January 2, Rev. H. W. Woodward akarudi zake Magila, alikaa naswi kwa miezi minne hapa Mbweni. Naye alikuwa mwema kwetu siku zote, akawasayidia wengi. B. M.

## HABARI ZA MASASI.

Kwa Mtengenezaji salaam. Wa baada ya salam nakuarifu habari chache ulizosikia zamani. Bassi baada ya kuarifu kama sisi hapa tunakaa upande wa mlima huu unaitwa Mtandi tuko upande wa magharibi. Tukataka kuhamia mashariki, ukipima kwa dira ni sawa-sawa na hapa tulipo. Lakini haikuwezeka kuhama kwa maana mbili, ndio (a) watu wenyi tamaa hawapatani katika biashara pa kununua miti ao mianzi, ndio (b) huona watu kama kanisa liendapo likawa karibu tutaathika, waona ndio kama utumwa tu. Wanataka kuwa huru katika kanisa lao kuliko kuwa nalo karibu.

Bassi bwana Smith hana buddi na kushindwa, akaacha kujenga kule akaanza kujenga hapa hapa tena. Naye L. Mkwasomba akaja illi School tuwe waalimu wawili. Lakini bwana akamwelea kama watu wawili chuoni haipo kazi. Akanitwaa mimi kuwa msimamizi, baadaye L. Mkwasomba

**MSIMULIZI. 512**

akarudishwa Newala tena, nami nilirudia kazi School. Na sasa nyumba ile tulioanza hapa imekwisha, juu pia imezekwa yote pia, ina sakafu yake ya mianzi ao ghorofa. Ni furaha kuu kuisha nyumba hii, kwani vitu vyote ni nje tu, mvua yake jua lake, mchana wake na usiku wake pia, kwani hapana nyumba ya kutia. P.K.

**HABARI ZA MLOLELA.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu, nakuarifu habari zetu za hapa tukaapo.

Dec. 15 na 16 tuliwatazamia watoto wetu wa kiume akili zao (Examination); na Dec. 17 tuliwatazamia watoto wanawake.

Dec. 21 Siku kuu ya Tomaso Mtume ndipo tulipoanza kufunga vyuo vyetu (Schools), na siku zilizofuata ndizo zilikuwa za kuwafundisha kuimba waimbaji (Choirs).

Dec. 24 tulipamba Kanisa letu kwa majani ya miti na maua ya mwitu, na jioni ilikuwa sala kubwa sana.

Dec. 25 Ndio furaha ya Siku kuu ya Kuzaliwa Bwana wetu. Assubui alfajiri na mapema mimi na mwalimu Cyprian Chitenje pamoja na watoto wetu na nusu ya waimbaji wetu tukaimba Christmas Carols, ndizo nyimbo za siku ya Kuzaliwa Masiya, tukazunguka ua wetu wa Kanisa na wa kuchezea mpila, na kulipopambazuka tukaenda killa mtu kunawa. Saa kwanza ikapigwa kengele ndio sala kuu ya Siri. Mbarikiwa, tukaingia Kanisani na kwa shangwi ya sifa ya kumwambia Muungu sifa zake; na watu wengi walioshariki. Kiisha tukatoka Kanisani tukaingia mezani, Bwana Padre wetu akamtoa mbuzi akachinjwa; tulipotoka mezani marra kengele zikalia kwa sala ya assubui. Kwanza wakaja wenyi uvumba na msalaba, wakasimama ndani ya ua wa nyumba yetu, na nyuma yao wakafuata Wamasihiya.

MSIMULIZI. 513

waume, na nyuma yao hawa wakafuata Wamasihiya waanawake wote wawili wawili; tena nyuma yao hao tukafuata sisi waimbaji (choir); tena mwisho ndio Baba Padre wetu. Ukatolewa uimbo wa Carol ya 6 "Bikira ni safi wanenavyo nabii," ndio tukaenda pole pole mpaka mlangoni pa Kanisa tukasimama; tena tukaimba "Benedictus" (Abarikiwe Bwana &c), tukaingia Kanisani, ndipo sala ya assubui ikaanza; na watu wengi walikuwapo. Tulipokwisha tukatoka Kanisani tukiimba kurudi nyumbani kwa taratibu ileile kama tulivyoingia.

Dec. 26 Siku kuu ya Stefano Sha. wa kwanza, assubui saa kwanza Usharika Mt. Alasiri saa nane unussu tukapiga kengele kuwakusanya watoto wote wasomao hapa tuwaambie nani walioshinda katika "Examination" yao.

Watoto wanaume wa kwanza katika darasa ya kwanza ndio - 1. Useni; na wa 2. Kalemwanga, na wa 3. Gideon Kawanga Katika darasa ya pili 1. Pesa, na wa 2. Msoma, na wa 3. Kapamba. Katika darasa ya tatu 1. Banali; na wa 2. Njechele, na 3. Mtutile. Katika darasa ya nne 1. Mkwemba, na wa 2. Manji, na wa 3. Kapili. Darasa ya tano 1. Tibu, na wa 2. Malenga, na wa 3. Malamya. Watoto wanawake wa kwanza katika darasa ya kwanza ndio - 1. Durham Chiwiwi; na wa 2. Che Syao, na wa 3. Chehjololaga. Katika darasa ya pili 1. Che Ngondelaga, na wa 2. Akwalachia, na wa 3. Pasonje. Darasa ya tatu 1. Ajanjeuli, na wa 2. Akusigala na wa 3. Dora Sihaba. Darasa ya nne 1. Akumbolela, na wa 2. Akungwewa, na wa 3; Akulaiti. Katika killa darasa walioshinda wale watatu walipewa zawadi hivi, wa kwanza alipewa nguo ya bendera ya mikono minne, na wa pili alipewa ya mikono mitatu, na wa tatu alipewa ya mikono miwili.

Dec. 28 Tulitoka assubui na mapema kwenda Newala,

MSIMULIZI 514

mimi na mwalimu Cyprian Chitenje na watoto wetu 6, na watoto wawili wa Baba Cecil, Florence na Mona, tukafika saa kenda unusu.

Tukafurahi sana kuwaona akina bwana hawajambo, juu yote waalimu wenzetu Daud M. Leonard Mkwasona na Leonard Pesa na mkewe; na watoto wa Masasi walikuja pia. Ikawa mashindano ya watoto na vingine.

Dec. 31 kwa alasiri marra tukasikia bunduki zinalia. Tulipokimbilia tukasikia kama ni watu waliosafiri Nyassa pamoja na Bwana. Maples wanarudi; marra tukawaona waliotangulia, wakasema, Sisi tumetangulia na wenzetu watafika kesho.

Jan. 1 Siku kuu ya Tohara ya Masiya, assubui tukasikia bunduki nyingi na vigelegele vya waanawake wengi waliosafirisha waume zao, wangine ndugu zao na wangine watoto wao; ikawa furaha kuu na kuimba na kucheza. Kwani waliokota pembe mbili kubwa za tembo nyikani, moja ametwaa Bwana Smith na moja imekuja hapa, bassi furaha ikazidi; aliyeokota ndio Adimu Twanje. Mbele ya kufika mjini alikaa ziwani akapelekewa nguo apambwe; alipokuja alivaa kitambi bura na kanzu ya kazi; na kilemba kitambi bura na bendera. Bassi pembe ilipofika mlangoni pa Mwenye Barnaba Nakaam, bunduki nyingi zikalia furaha sana sana. Hatta jioni ngoma nyingi zikaletwa tayari.

Watu wengi wakaja kwa machezo ya usiku; watu wakazidi furaha kwa kuwaona rafiki zao.

Hatta jioni ngoma bado kuanza kupigwa, marra hiyo akaingia mtu atokaye njia ya Lindi tukapata barua zetu za Unguja. Marra Padre akasoma barua yake isemayo - Utahuzunika ukisikia kama mtoto wako mmoja Stefano Mteta amefariki. Marra ikawa kimya kabisa mjini pote hapana

**MSIMULIZI. 515**

sauti wala ngoma; kimya kabisa kimya. Marra akaenda kuarifiwa babaye na mamaye kama mwanao amefariki. Ah! ah! Ee maskini baba na mama na nduguze wawili, msiba mkubwa juu yao na kufathaika kwa malio makubwa. Kama tusemavyo siku zote furaha yafukuzana na huzuni; mahali pa furaha pakaingia vilio vitupu, ndio kutupa sisi fundisho kama sharti siku zote tuwe tayari kupokea litokalo kwa Muungu; tukiwa na furaha tuwe tayari kupokea huzuni, na tukiwa na huzuni tuwe tayari kupokea mbaraka na faraja tupewayo; kwani Bwana wetu asema, - "Heri wenyi huzuni, kwani watafarajika." Kwani ni kweli, Muungu hawezi kusema uwongo wala kudanganya, kwani Muungu amependa kumtwa ndugu yetu mpendwa astarehe katika taabu za dunia. H.S.M.

**HABARI ZA MKUZI.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Wa baada ya salaam nakuarifu habari za hapa petu. Dec 11. Wametuwasilia hapa mwalimu Alfred Juma na Sisters kutoka Unguja, wanakwenda Magila. Dec 23 walifika hapa watoto watokao Unguja wa Kibondei pamoja na waalimu wawili G. J. Swedi na W. J. Swedi. Hatta Dec. 25 ndio siku kuu ya Kuzaliwa; assubui tukaimba na kuzunguka mji wote wetu: tena saa kwanza ikawa Usharika Mt: na mahubiri. Siku iliyo baada yake walibatizwa watoto wawili wa hapa petu, ndio Basili Kitanjo na wa pili Tomaso Lukindo, na saa nne sala ya assubui na mahubiri, watu walijaa kwa kadri yao. Na juma a mosi watoto walianza kutawanyika kwao kwa jumaa tatu, na Mr Dale akaenda Umba kuwafanyia nao siku kuu yao. Dec 28 assubui akaturudia kasisi wetu Mr Dale tayari kwa harusi, Siku ile ya juma a tatu watu wakaja wee, tangu saa edashara hatta saa tatu watu wakaja tayari kwa harusi, wakawa

**MSIMULIZI. 515**

wengi hatta wangine wakalala nje. Siku hii akabatizwa mzee mmoja anayekaa Umba. Hatta assubui mapema bunduki zikaanza kulia moja moja, kengele ya Kanisani ikalia watu wakavalia mavazi yao tayari, tukaingia kanisani, ikafanyika kwanza taratibu ya Ndoa, tena Usharika Mt. Kanisa likajaa mno ajabu. Tulipoisha kutoka tu marra watu wakazipiga bunduki hatta kuumia mikono, ikawa furaha kuu, bunduki zote zilizopigwa hazihesabiki kama mchanga, naona kwa kweli sijaona wala sitaona harusi iliyostawi kama hii kwa killa kitu kwa harusi. Zalichinjwa mbuzi mbili na kondoo watu wakaja hatta kuutazama. Na Sister mmoja alikuja pamoja na watoto wake wa kike hatta kama saa nane akarudi nao Magila. Alhasiri ukawa mchezo. Mtu jina lake Kidungwe akaja naye kushangalia akapata pesa nyingi kwa mchezo wake, hodari kwa kutunga nyimbo, na ikawa dandaro, na kinyasa wakacheza. Hatta saa thenashara ya usiku wakaenda zao nayo ikasitawi sana. Ndio habari za harusi. Watu wangine wakaenda siku ile ile, wangine juma tano.

Siku hii hii ya harusi jioni wakafika hapa Mr. Edwards na Mr. Roberts, kwani Mr. Edwards alikuwa hawezi Magila, amekwenda Unguja kupata afya, siku ya juma a tano Dec 30 alfajiri na mapema wakatelemkia Pangani.

Pamoja na Kasisi wetu Mr Dale na mwalimu Manfred ma George Songolo, kuja kuoa; twatumaini wataturudia upesi. Dec 31 Doctor Henriques amekwenda Magila kupata afya kwani alikuwa hawezi hapa, naye twatumaini kuturudia upesi, kwani hatuna mganga sasa. Ndio mwisho. A.A.S.

**HABARI ZA KIUNGANI.**

Juma a tano, Jan. 15, Bwana Askofu alituwasilia salamu salimini baada ya safari yake ya kwenda Nyasa; waalimu



MSIMULIZI. 517

wote wa hapa tukaenda kumlaki, pamoja na Schoolmasters wa hapa na Bev. A. Hood. Tukafurahiwa sana kumwona aliyekuja pamoja naye mwalimu Yohana B. Abdallah na mpishi Barnabas Farajala, na watoto watano wa Nyasa, ndio hawa, Gabriel M.Katoma, Daniel Chisombe, William E. Kaikeni, Bernado Mkaki, na Stefano L. Ponanga.

Dec. 18, watoto wote wa Magila walienda zao kwao, pamoja waalimu George J. Swedi na Willie J. Swedi.

Dec. 20, Tulienda Mkunazini watoto wote wa hapa, na watoto wa Mbweni kuwashuhudia Rev. A. Hood na Rev. W. M. Mercer wakiamriwa Ukasisi; tulipoisha toka kanisani tukapata chakula, kisha tukarudia.

Dec, 24, Vijili ya Kuzaliwa Bwana Wetu. Bwana Askofu aliwabatiza watoto kumi na moja wa hapa, ndio hawa Patriki Kiaka, John Kasimbwa, Andrea Lukata, Jude Liwago, Richard Alfred Ndauka, Samuel Faraji, Aidan Mekenda, Bruno Sauli, Tomaso Yanikore, Cyril Mabruki, Guy Dawnay Ngumbi. Ndio marra ya kwanza kutumia Font yetu mpya. Kwani tumeletewa Font nzuri mno ya marmara nyeupe na nyekundu, na nakshi nzuri.

Dec. 25, Kuzaliwa Bwana. Twaliamka saa edashara usiku tukaimba nyimbo za siku kuu, na siku ile twaliharimiwa sana na General Mathews. Na tena tulifurahiwa sana kwa kula siku kuu akiwapo na Bwana Askofu hapa petu.

Dec. 26, tulienda asubuhi tunakocheza mpila kujaribiwa mbio, kutupa mpila, &c. Saa sita tukarudi.

Dec. 28 Siku yao Wasiokosa, watu wa Mbweni walikuja hapa petu, tena Wahindi wakaja wawili wakafanya miujiza yao mbele yetu, kama siku ya Bartolomayo Mt. Hatta saa sita tukapewa chakula, saa nane tukaenda

MSIMULIZI. 518

Mnazi Mmoja kutazama mashindano ya killa namna, saa thenashara tukarudi.

Dec. 29, wenzetu watu 38 walienda Dunga pamoja na Mr. Matthews na Mr. King. Wakarudi Dec. 30, Alhamisi Dec. 31 watoto wote wa hapa tulienda Mbweni kwa arusi ya mwalimu Herbert M. Feruzi, na Yakobo Chorola, na wa Mkunazini Frank Deina na Charles Masegwa. Siku hii tulifurahiwa, hatta jioni tukajirudia zetu.

Katika wakati huu wa Kuja twalipata huzuni kwa kutwaliwa ndugu yetu STEFANO MTETA, ugonjwa wake aliugua kwa siku tano. Alipopelekwa Mkunazini auguzwe, siku ya pili yake akafa panapo saa a pili, Dec. 13th. Akazikwa Juma a tatu, Dec. 14th. R.I.P.

Jan. 28th. Alifariki tena mtoto mmoja wa hapa, naye ni mtoto wa Nyasa DANIELE CHISOMBE, alikuwa mgonjwa kwa siku tano, akafa Alhamisi, panapo saa a tissa. Akazikwa Ijumaa. saa mbili unussu. R.I.P.

Jan. 1, 1892, salamu za mwaka mpya kwa wote! Siku hii aliwasili Rev. G. Dale Ijumaa pamoja na waalimu Manfred Manyula, na George Songolo. Jan. 3, Padre Woodward alisafiri Magila pamoja naye mwalimu Herbert Feruzi, na Yakobo Chorola. Waliwasili hapa waalimu George Swedi na Willie Swedi. Jan. 11-15, Palikuwa kufunga kwa rohoni (Retreat), na mkubwa wa Retreat Bwana Askofu. Jan. 17, Bwana Askofu aliwatia mikono watoto kumi na tatu wa hapa ndio hawa. James H. Mpila, na Michael

MSIMULIZI. 519

Chikokota, Leonard M. Kamungo, David Kalanda, Patriki Kiaka, John Kasimbwa, Andrea Lukata, Judo Liwago, Richard A. Ndauka, Aian Mekeada, Bruno Sauli, Cyril Mabruki, na Guy Dawnay Ngumbi.

Jan. 19, Bwana Askofu alitoka Unguja kwenda Newala. Pamoja naye walienda waalimu Harry Mnubi, Arthur Kasembe na Yustino Mkandu.

Jan. 29, tumefurahiwa sana kwa kumwona tena Rev. S. Weigall.

### **HABARI ZA LIKOMA.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu habari za huku. Lakini, bwana, sikia kwanza, kwanza naona nitaandika habari za hapa, tena za Makanjila tena za Chizumulo tena labda nitarudi hapa. Na tena, Ah! sijui.

Habari za hapa habari ni njema, tena mbaya. Njema kwa kuwa bwana Wilde anawajengea nyumba wajomba wa hapa. School imeanzwa nayo ya mawe. Mbaya, kwa maana Archdn. Maples tangu alipokuja hajapata afya, hatta sasa yu kitandani.

Habari za Makanjila. Hivyo watu nasikia, Mzungu akienda kwa Makanjila atakufa. Naona uwongo. Mbona Makanjila akakimbia mlimani, na mizinga yake 2 imetwaliwa? Amepigwa bwana Makanjila, hana idadi. Na wafalme wapata watano wamepigwa. Lakini naona sitaweza kuelezea zote illa za Makanjila. Ss. "Domira" ilipokaribia kwa Makanjila, haikutaka kufanya vita, illa kupatana.

Lakini jemadari wa asikari alipoona watu wengi wapo pwani na wanapiga bunduki, akaona hana buddi kufanya vita. Na stima hii Domira haikuogopa kitu ikaenda mpaka bandari soooo. Huku watu wa Makanjila wanapiga bunduki, lakini marisasi yao yapita juu juu tu. Tena

**MSIMULIZI. 520**

wameingia majini hivyo wanapopiga bunduki. Bassi Captain akashusha mashua ndani, yake wakaingia askari 7 tu wala si wengi. Wakashuka wakapigana. Askari wakaona vimoto, bwana, wakarudi nyuma kidogo. Akaja Captain akawasaidia akawafukuza, akazichoma nyumba. Na anapoamrisha kupiga bunduki, ah! kama mzaha tu. Akisikia katika msitu huu panalia bunduki moja tu. Yeye huamrisha askari zake wapige pamoja pamo hapo. Bassi bwana, Makanjila yuko mlimani tu.

Habari za Mchizumulo, ndio, mimi naenda kaa huko kwa miezi mitatu. Kwani hamna mwalimu. Tangu leo Msimulizi wenu simshiki tena, huu ndio wa mwisho. C.K.

**HABARI ZA NEWALA.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Tena nakuletea habari hizi za huku.

Dec. 12 Ulikuwa mkuki wa Makwangwara kwa mzee Mutola kusema, Upinde; ndio alama ya urafiki. Lakini yeye alikataa kufanya nao urafiki kwa haraka. Na sasa ameandika barua kwa Wadachi kuuliza wanaonaje wao.

Dec. 21 Siku kuu ya Tomaso, tukaanza Examination, kwani ndio desturi zetu hapa killa mwaka. Ikaisha siku ya 24. Nao walioshinda katika darasa ya kwanza ni: 1. Francis Sapuli, wa 2 Siluano Ngaweje, wa 3 Ambrosio Mitande. Katika darasa ya pili, 1. Lesile Namate, 2; Eriko Akuchigombo, 3. Adam Saburi. Darasa ya tatu 1. Mleika Malesho; 2. F. Ruben Namalowe, 3. Mika Twanje. Darasa ya nne, 1. Msieri 2 Mbilichila, 3. Matipa. Darasa ya 5. 1. Mwenyi, 2. Mmenyariga, 3. Mtambarika. Darasa ya sita, 1. Ausale, 2. Alban Chiwisa, na Mtipa sawa. Darasa ya saba, Kachinga wa kwanza, wapili Chibwana.

MSIMULIZI. 521

Dec. 24, Tukapamba Kanisa letu baada ya kwisha examination.

Dec. 25, Siku ya Christmas Usharika Mtakatifu. Tena bwana alihubiri. Saa ya nne ikawa "Matins" na Ubatizo, nao waliobatizwa ni watoto wa nyumbani watano. Na majina yao ni haya, Cecil Kamsila, Mika Twanje, Mikael Malesho, Andrea Msuweta, Yusuf Chiuibihdu. Juma a tatu yakawa mashindano ya bunduki. Siku ile ile akaja Bwana G. Atlay pamoja na watoto sita wa Masasi. Jioni siku ile ile wakaja waalimu wawili wa Mlolela Cyprian H. Chitenje na H. S. Mtoka. Pamoja na watoto wanane wawili wao ni watoto wa Bwana Cecil Florence M. na Harriet Mona. Juma 'nne yakawa mashindano kwa watoto wa school wote. Tena jioni Bwana Hainsworth alifanyiza sanamu za taa, na ile juma a tatu pia alifanyiza kwa watu wa hapa tu. B. M.

(Ziko tena habari zilizotoka Newala, nazo nzuri sana. Lakini hatuna nafasi safari hii. Twatumaini zitapigwa chapa baadaye, habari za hatari za ndugu zetu wanne kwa Maviti). Mtg.

### **HABARI ZA MAGILA.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Siku nyingi bado hatujaonana: bassi uwe rathi bwana. Dec. 14 nikaanza kuwatazamia watoto wote wa chuoni elimu zao. Naliifanyiza kwa siku 'nne kwa sababu ni peke yangu. Na walioshinda katika darasa ya kwanza 1. Gabriel Kikavu sawa na Ngoma, na wa 2. Mzimba sawa na Antonio Mchancha; darasa ya pili wa 1. Bebe, na wa 2. Ndiga; darasa ya tatu wa 1. Mbaruku, na wa 2. Kingodi; darasa ya nne wa 1. Geldart Senkoba, na wa 2. Kamtande; darasa ya tano wa 1. Kukuti, na wa 2. Salu;

**MSIMULIZI. 522**

darasa ya sita wa 1. Semsule, na wa 2. Sengonda.

Katika Dec. 24 wakatuwasilia hapa watoto wetu waliokwenda kusoma Unguja, furaha nyingi sana. Siku kuu yetu ya Uzaliwa ilitufurahisha sana. Ilipokwisha tu watoto wakapata (holidays) juma tatu, tuziponde tu. Siku ileile tupatapo ruhusa mwalimu Manfred M. akaenda Unguja, na tena watoto tulioweza tukampeleka mwalimu C. Lizani kwa harusi yake.

Katika Jan. 5 akawasili Padre Woodward na Bwana Roberts, wakitoka Unguja, pamoja na Josephin Yasmini, na Ellen Fayida.

Katika Jan. 9 wakawasili wenzao mwalimu Hugh P. Kayamba, na mkewe, Herbert Feruzi, na mkewe, Yakobo Ohorola na mkewe. Oh! si furaha hiyo kuwaona wageni wa Unguja.

Katika Jan. 13 Padre Woodward akawafanyia waalimu wote wa Bonde karamu, kwa kuwafurahia wageni akina Hugh Kayamba, karamu ambao karamu.

Katika Jan. 25 Siku kuu ya Paolo Mtakatifu tukafanya mkutano wa siku kuu ya Uzaliwa. Watoto wa vyuoni mwote karibu wote walikuja wakashindania zawadi kidogo, tena wakala mpunga kwa ng'ombe; baadaye wakaenda zao.

Katika Jan. 26 athuuri wakawasili ndugu zetu mwalimu Manfred Manyula na mkewe, na George Songolo na mkewe Sifuraha hiyo, tukiwaona wenzetu tena? Siku hii alasiri akatoka hapa Charles Mkumbukwa, na James Chuma; kwenda Kiungani kusoma. Kwa heri bwana. J.B.M.

**KOROGWE.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam; wa baada ya salaam, nakuarifu hali yetu ya huku. Nov. 29 Juma a pili assubui tulikwenda kwa Mugumi

MSIMULIZI. 523

kusema na watu habari ya kuleta watoto wao kusomeshwa na kuwaeleza mambo ya Muungu tena; bwana Lister asema Kingereza, Henry mfasiriji. Jibu tulilopata na Wilfred Madudu kwao ni hili, Huu uzima wa ulimwengu ujao u vipi? tuelezeni vema. Ndio tukawaeleza. Yaonyesha kama wanafikiri mioyoni mwao.

Dec. 1 School tumeianza sasa, i katika kujengwa; na watoto wanazidi kuingia Mission kukaa hapa, zayidi wa kwa mji wa Kwa Sigi ulio mbali na hapa, kama mwendo wa saa mbili. Tunao 8 wa huko, majina yao ni haya - Mchogwe, Chaba, Vulu, Kiwayo, Mwamoto, Mwejaha, Kungulu, Mdimu Jonga. Jumla yao sasa watoto 12.

Dec. 21, Mimi Henry Daud Mhina Boko tulikwenda Bonde kwa siku kuu ya Uzaliwa wa Bwana wetu. Dec. 31, tukarejea Kologwe kushika mji mahali, kwa Mr. Lister na watoto wote wa hapa wamekwenda Bonde kuamkia tamaa, tukakutana nao njiani wakirudi Bonde nao, nasi ukija Korogwe, Mr. Lister amethoofika sana kwa homa. Watoto wa hapa (Mission) ya Korogwe ndio safari yao ya kwanza kwenda Magila, kutazama watoto wa kule, nao waenda kwa furaha sana. Si jambo tulilotazamia kama wataachiwa na wazee wao kwenda mbali kwa amri yetu sisi. Wenyewe waana hawakai illa baba zao ndio wenyi uthia sana, ndipo tuonapo kama watoto waanza kutuzoea na kufahamu, na baba zao kwa kadri wazana kutumaini kama tu watu wa kweli kwao, si adui kama walivyokuwa wakithani; kwanza hawakututumana sana. Jan. 6, Tuna shidda sana ya kupata watoto mimi na Wilfred japo tukaenda mjini kuwatafuta. Zuo limekuwa tangu watoto wao wa hapa (Mission) walipokwenda Magila kutembea pamoja na Mr. Lister. Wasema ah! waana wetu

MSIMULIZI. 524

mmewachukua mbali huko wakiwa ni watu wasiojua neno. Wasema 'Mmewapeleka Ulaya; labda hatutawaona tena. Marra kwa marra mama zao wanijia hapa kuniuliza habari za waana wao, hawaamini kabisa kama wamekwenda hapa Bonde karibu wapajuao wao wenyewe.

Jan. 14th. Mr. Lister na watoto wote wa hapa wamerudi kutoka Magila kama saa tatu ya usiku.

Jan. 17th. Jioni twalikusanyika wote hapa kwa uchache wetu tukaenda mji wa Kologwe tukaimba nyimbo za dini. Na mwalimu John Mdoe akasimama kati ya watu akawahubiria juu ya kazi yetu hapa &c.

Watu wingi walikusanyika wake na waume, wapata waume mia na zayidi na wake kama mia na zayidi, walisikiliza vizuri sana; kwa mwisho wakathani ni mambo za kujibiana, wakawa tayari watu wangine kutoa majibu yao, tukawaeleza haya ni maneno ya Muungu mfundishwayo, si ya kujadiliana kama masa. Hii ndio marra ya pili tu kuhubiri mjini mwao. Na sasa watoto wanakuja vema sana kufundishwa killa siku, pamoja na waana wetu wa Mission. Hatta waanza kufahamu kazi yetu nini?

Sasa School yetu yaezekwa, karibu itakwisha mahali pa juma mbili labda.

School ya watoto yaendelea sana, na Yakobo Chamdangwe; afanya bidii sana katika kazi yake ya kwanza kusomesha kwani sisi tungelikuangalia mambo za majengo ya nyumba na kutengeneza Station.

Siku moja tuliambiwa, Nendeni Mazinde kwa Dachi kuleta punda. Tukachukua na barua ilioandikwa na Padre Edwardes kwa habari hiyo. H. N.

(Habari za safari hii nzuri, tena zapendeza sana. Tumeziweka makusudi zipigwe chapa baadaye, kwani nafasi hapa hapana. Mtg).



MSIMULIZI. 525

### **ANJILI KATIKA UGANDA.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Naona ndugu zetu watapenda sana kusikia habari niliyopata kwa Bwana Askofu wa Mombasa juzi juzi, nilipoingia kule nikiwa katika njia ya kurudi hapa. Wajua kama ndiye asimamiaye Wamasihiya tangu Mombasa hatta Uganda.

Bassi akatueleza ginsi inavyoendelea kwa ajabu kazi ya kufundisha.

Alichukua huko vitabu vya Anjili mia nyingi sana, hatta afikapo, kwa saa mbili tatu tu vyote vimeuzwa kwao Waganda. Hapana aombaye kupewa burre; huleta thamani yake wakitamani mno kupata. Hatta wengi wengi wameisha weka mali yao amana kwa Wazungu tayari, wakinena, Vikija vingine tena bassi utugawie.

Tena majumbe wengi wa Uganda wamewaambia Wazungu wa Upelekwa wao, Tupe waalimu tu waje mijini mwetu, tutawajengea nyumba na vyuo, na chakula chao chote na vifao tutawapa pia burre. Waje tu kutufundisha Anjili.

**MSIMULIZI. 526**

Tena wale walioisha tiwa nuru na elimu ya Kimasihiya wengine wanaiga sana kujitia pia pasipo mshahara wo wote katika kazi ya kufundisha ndugu zao. Pana waalimu yapata 18 wameisha kujiweka kwa kazi hii wakisema, Tupeleke mji wo wote hatta ukiwa mbali kwetu mwendo wa siku kumi, hatta kwa watu wa kabila ngingine, utupeleke tu, tuende tukawafundishe wenzetu; mshahara hatutaki hatta pesa, tutakula yale tu tupewayo na wenyeji, kwa mangingine tukakuwa rathi. Mmoja wao afanyaye hivi ni ndugu yetu Henry W. Duta aliyesoma zamani Kiungani, naye ikampasa kutiwa ujumbe katika inchi yake, asikubali, alichagua Upelekwa akamwachia mwingine ujumbe.

Tena katika mji wao mkuu Waganda wenyewe wanajenga sasa Kanisa la kutosha kwa Waganda 2000 kwa gharama yao wenyewe, nao watu maskini tu.

Bassi, ndugu, haya yote yatupasa tuyaige tusiitumanie mno fayida ya ulimwengu huu illa ya ule ujao, ndipo Dini yetu takatifu itazidi kuenea kwetu kama kwao ndugu zetu Waganda. P. L. J-B.

**MKUZI.**

Feb. 15, wakati wa magharibi, tukasikia mdundo wa ngoma, tukaangalia tukaona ni Wadachi wawili na askari zao na wapagazi, wakaenda kulala mji wa Mkuzi wanatoka pande za Kilimanjaro. Na katika Wadachi hawa mmoja ni yule Dr. Peters, aliyetaka hutwaa Uganda zamani. Naye anatoka kutiisha pande za Masai, Ah! mtu huyu ni hodari sana kwa mambo ya vita. Na tumesikia

MSIMULIZI. 527

kama atarudi pamoja na yule barozi Consul Smith.

Feb. 18, panapo saa 5 alifika Mdachi kutoka Tanga hatta saa kenda akaenda zake Minyuani. Feb. 19, mimi na Mr. Dale tulienda Magila, tukapitia Kilulu kujaribu kufanya mashauri na wazee wa huko, lakini wakatuambia tuje tena tutokapo Magila. Hatta juma a mosi alasili tukarudi pamoja na mwalimu Henry kutoka Kologwe kuja kuangalia mkewe na mtoto wake. Hatta Feb. 23, tulienda Magila na watoto wote pamoja na Padre wetu, tukapitia kule kule Kilulu, na wazee wakatuambia tuje tena, tukarudi Magila. Bassi Padre akatangulia Magila illa sisi tukabaki pale Kilulu tupate kula chakula chetu, kwani tulichukua pamoja nasi chakula chetu. Bassi tulipokwisha kula tukamfuata Magila, hatta panapo saa kumi unussu tukafika Magila. Hatta assubui ni siku kuu ya Mattiya; kama saa tatu tukaanza kushindana kupigana mpila. Tukashindana wee hatta saa sita, tulipigana kama tuwezavyo, illa tukafungwa moja sisi watu wa Mkuzi.

Feb. 25, assubui tukaja na Mr. Woodward akafuatana mpaka Kilulu; wazee wenyewe hawajapatana vema, kwani hawana nia vema ya kumkubali Mwalimu kukaa nao; na mwalimu anayefikiriwa kwenda Kululu ndio George Songolo. Tena pale Mr. Woodward akarudi Magila na Mr. Dale akaja huku.

Tena Tomaso Likindo tumemwacha huko anafanya kazi ya kupiga chapa. Panapo Feb. 26, akafika Carlo Mwaimu na Samuel Mhesa kutuaga, kwani wanaenda Unguja.

Feb. 29, ikatokea mvua ya mawe: watoto waliokota wakala, nayo ni baridi kama barafu.

**MSIMULIZI. 528**

March 2, tulianza mfungo wetu kama kwa desturi.

March 3, akafika Mdachi mmoja kutoka Lewa, anaenda Tanga, kwani ni mgonjwa huyu. March 5 akafika hapa Mr. H. Lister kutuangalia, tena siku hiyo hiyo alasili akaenda zake Magila. March 6 ndio Juma a pili ya kwanza ya Kwaresima wametiwa watoto sita wa nyumbani na mtoto mmoja wa nje kuwa waanafunzi. Ndio hawa Sayidi, Sezua, Semboni, Sangai, Changale, Mavovo, na huyo wa saba, ndio Semnkai.

Mwalimu Andrew H. Abdallah anaanza kufundisha Mangidi anakokaa John Mbwana, nao watu wa huko wanajenga "school" yao wenyewe: na nyumba yake mwalimu itajengwa huko. A. A. S.

**KOROGWE.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Naanza kukueleza habari zipatikanazo huku kwetu.

Feb. 2, Siku kuu ya Kutakasika B. Maryamu.

Twalikuwenda Ulwengela watoto wote wa hapa Mission na wa nje pia, na bwana Lister na killa mtu wa mji, tukaleta mtu mmoja aitwaye Sengaya tumwaminiye naye ana mwanawe akaa hapa Mission, angoje mji. Saa moja assubui tukatoka na vyakula vyetu, na vibarua wetu kwenda shinda kule na vibarua, na fundi Daud Mhina wakitengeneza ulalo wa Ulwengela penyi mto huo, usifiwao kuwa na mamba wengi na hatari kupita, ginsi gogo hilo lilivyokaa vibaya juu ya mto na njia ya watu wote ni hiyo.

MSIMULIZI. 529

Tukafika tukaanza kupiga, na kwenda huku na huku, na kutazama mahali palipo pema kwa kujenga daraja njema halafu ya kuweza kupita vema pasipo hofu, na punda na nyama zote zipitazo kama ng'ombe &c, kwani sasa zaogelea siku zote. Naona hutastaajabu kusikia kama, wapitishapo nyama zao kupeleka Bonde, ao pwani kuuza wafikapo hapo wanafanya dawa zao walizochukua, ao hutwaa mtu ajuaye uganga wa kufunika mamba wasiwathuru kwa waaminivyo uganga wao. Bassi huku vibarua wafanya kazi ya kukata miti, na fundi Daud aweka vema, na kukomelea misumari. Athuuri wote tukala chakula na wapagazi wetu pia, ua mikate ya zabibu itokayo Ulaya aliyotoa bwana Lister, halafu watoto wakavua samaki, na tena tukafanya michezo na kutembea huku na huku. Alasiri bwana Lister na wapishi 2 na watoto wa nje wa Kurogwe wakatangulia kuja mijini; sisi tukakaa kule na watoto, tukawafanyia michezo mimi na Yakobo kuruka na kukimbia, kwa mapesa. tukajifurahisha sasa na karamu yetu ya Ulwengela. Na ulalo ukatengenezwa kama walivyoweza jioni, tukarudi kwa furaha na nyimbo za zumo. Hii siku kuu ya kwanza ya Mission Korogwe waliyoona. Wameona, na watu wa Korogwe, tujifurahishavyo kwa kukumbuka siku takatifu za Kanisa. Wengi walistaajabu, Ah! Mzungu aenda fanya nini Ulwengela na waana wote pia hawa? Siku ile killa wapitao wakienda safari zao, twawaambia watoe kitu, kwa wafanyao kazi kama tumbaku kuku ao cho chote kwa kuwaonyesha kama twawafanyizia wao, na watu wa inchi nzima, wapite vema.

Jan. 29 Mdachi mmoja alikuja akajenga hema lake kwa Mgumi na wapagazi wake, naye atoka Kilimanjaro, kazi yake kupiga sanamu kwa mikono na kuzitia rangi.

### MSIMULIZI 530

Akaja hapa Mission akatuonyesha sanamu zote alizoandika huko bara za Wamasai atokako, kwa kweli nzuri, ma hodari sana Mdachi huyu, siku hii akaandika mji wetu huu vizuri sana, nyumba vile vile na sisi tuliokaa barazani pia akatuandika, kwa saa 2 alikwisha mji wetu kuupiga sanamu. Siku ya pili akatuletea kutuonyesha tena kwa wema wake akatupa wenyewe sanamu ile iwe Ukumbusho kwa Mission.

Feb. 6th. Akaja Mhindi jina lake Dosa anayetoka Tangani aja fanya biashara zake za kuuza nguo &c, naye amefikia hapa petu, na atajenga nyumba yake hapa baada ya siku chache.

Feb. 8, Bwana Lister, na mwalimu Wilfred Madudu, na Boko, na Herbert Mkande, na watoto wawili, Kidungwe, na Kiwayo, na wapagazi wao watatu, na mwana wa Mdaini na Chikulu, waliokuja mtwaa Mzungu aende huko kwa mfalme Mdami aliyehitaji sana kuonana na Mzungu akaaye hapa. Na huko ndiko akaako yule mtoto wa Mdami aitwaye Tongomeso aliyekuja Bonde Magila Mission zamani akakaa asome illa kwa ugonjwa akarudia kwao. Na kwa tumaini kama safari hii labda atakuja na hawa ndugu zetu waliokwenda huko, na kama ikiwezekana wapate watoto wangine kuja kufundishwa kusoma hapa Korogwe mimi ningekwenda illa sababu ni mgonjwa.

Watu wa Korogwe, na asikari wa Kinubi wa Dachi wamepigana, na wakaja hapa mji kuhukumiana.

Feb. 8th Ulalo wa Korogwe umeanguka.

### **SAFARI YETU YA ZIGUA.**

Siku hiyo hiyo tukatoka kwenda kwa Mdami, tukasafiri hatta ilipopata saa sita tukafika inchi ya Kinamo tukakaa katika mji wenyewe Kinamo. Lakini taabu ya inchi hiyo

### MSIMULIZI 531

ni maji, na katika mji wa Kinamo twalitaka maji, tukapewa maji ya visimiko vya vinu. Bassi tulipoisha kupumzika tukaondoka tukashika njia tukasafiri hatta ilipopata jioni tukafika Zaila, wenyewe wakatukaribisha vizuri lakini tulipoonja maji yao wanayokunywa ni chumvi. Bassi hatukuweza kunywa sisi, bassi ikatupasa kuendelea mbele, tukaenda tukafikia kijiji kidogo kiitwacho Hediboma (ao Hangoto); bassi pale tukalala. Assubui yake tukashika safari yetu vile vile tukakanyaga nyika haina maji wala mji tukaenda hatta athuuri tukaona mji uitwao Kwamasimba tukatua nje ya mji, sisi watoto tukaingia mjini. Watu walipotuona wakakimbia wangine wakabaki, na waliobaki tukiwaambia, tupeni maji, wanakataa; lakini tukiwatanyia ukali wanatupa tena si maji tu hatta togwa pia wanatupa. Mr. Lister akatangulia na wapagazi, sisi watoto tukabaki, nyuma kununua chakula, tukakipata tukala tukaisha, tukashika njia, tukaenda hatta ilipopata saa nane tukafika kwa Mkono tukamkuta Mr. Lister anakula chakula tukakaa pale saa moja. Bassi kutoka pale tukaenda mwendo wa saa mbili tukafika mji mdogo wa Mgaya uitwao Luringo. Marra mwenyewe akapelekewa habari kama Mzungu amekuja, Marra mwenyewe akaja na askari zake waamkiane; wakaisha akamletea kondoo na kuku watatu; alipokwisha kutupa kitoweo, akatuambia, "Nawataka mje kesho kwa Mkolo mji wangu mkubwa." Tukamwambia, "Vema, bwana."

Tukalala pale Lusingo, lakini usiku ilikunya mvua Mr. Lister akavujiwa pale alipolala, lakini afanyeje, hakuwa na hema, bassi ikampasa kulala na mbuzi, akaenda panapolala mbuzi akalala. Na juu ya nyumba kumetundikwa mihindi, panya wamo, madudu yanaanguka, moto umo,

**MSIMULIZI. 532**

na mambo ya mbuzi yamo, bassi siku hiyo Mr. Lister twathani hakulala, alikumbuka Ulaya siku hiyo, twathani kama mito yake imeliwa na mbuzi. Hatta asubuhi tukaondoka tukaenda kwa mji wake mkubwa akatupa kondoo mbili wakubwa sana tukalala pale siku mbili, kuku nyingi sana. Akatufanyia heshima sana. Tukaondoka pale tukazidi kwenda mbele kwa Jumbe Mdami mwendo wa siku mmoja tukafika mji wake mkubwa sana. Tulipokaribia kuingia tukapiga bunduki mbili, marra watu wakatoka nje ya mji, labuda wamethani kama ni vita, maana huko watu wanaogopa Wadachi sana. Bassi tukafika kwa mzee Mdami akatupa kondoo na kuku tatu tukakaa pale siku moja, Juma a mosi.

Feb. 23rd tukaondoka kurudi kwetu, tukaenda hatta kati ya njia tukapotea njia tukarudi nyuma tukaiona njia yetu, tukaenda hatta kwa Mgaya tena.

Tulipofika Mgaya akatufanyia heshima lakini hatukulala pale tukaendelea mbele hatta Korogwe. Tukawasili Feb. 14 kwa uchovu mwingi sana. W. M.

**VITA YA CHIZUMULU.**

Zamani mfalme wa Chizumulu, jina lake Mataka, alikuwa hawezi, lakini siku nyingi zilikuwa zikipita naye alikuwa hawezi sana. Bassi mwezi wa Dec. tumesikia kama amekufa, na kufa kwake kulikuwa hivi: alikufa mchana, lakini watu wa kwake hapana mmoja wa kutangaza kwa watu wengine, kusema, Mfalme Mataka amekufa; walimficha hatta jioni. Bassi tutafanyaje?



MSIMULIZI. 533

Wakaanza kusema, ni vema tuende kwa mwenzetu Mbuluma tukamwambie kama Mataka amekufa. Walipofika kwa Mbuluma, naye Mbuluma akatoka na mikuki yake na watu wengine wa kumsayidia kufanya vita pale pale, na yeye ni ndugu yao; lakini hawakuweza kusimama wakakimbia. Wana wake wakaogelea majini. Mtu mengine jina lake Kambwili akawaambia watu wake kusema, watu hawa walioingia majini msiwafanye kitu, lakini wachukueni, halafu yake waende zao, sababu ni ndugu zetu, na sisi hatukujia vita lakini kuwaambia.

Alikuwapo mtu mmoja mwenyi mji, jina lake Chapema; alifanya kwa hila yake, lakini vita si yake. Akakimbia mbio kwake, alikwenda Kusami kwa ndugu zake kupiga mbiu ya vita. Wale watu waliofiwa walikwenda kwao, wakalala, asubui yake wakaona vita inakuja, na mwenyewe Chapema.

Bassi wakasema. Ah! tutafanyaje? tena watu wa hapa wamo Likoma. Ah! tutafanyaje tena? tutajaribu.

Wakajaribu lakini hawakuweza kusimama, kwani wao walikuwa wengi, wakazama tu majini na kukimbilia visiwani. Wale watu wakautwaa mji wao, wakateka vitu vingi vya mjini.

Wengine wakaingia nyumbani, ulimolazwa ule mzoga wakaufanyia vibaya sana.

Watu wengine walikuwa wakisema, msiufanyie hivi mzoga, wale watu wakachukua mbuzi zote za ule mji Masasa. Wenzao wakajaribu kuwaambia, turudishieni mbuzi zetu; hawakukubali. Ambuluma alikuwa akisema, mlininyweshwa sumu, hapana hatta sababu, wala kukupeni sikupeni. Na wao wakamwambia. Na sisi vile

#### MSIMULIZI 534

vile umetunyweshwa sumu tulipe na sisi. Lakini vita yenyewe bado haijaisha. Na upande mmoja walijeruhi wawili na upande wa pili vile vile. A. T. M.

#### **LIKOMA.**

#### **HILA YAKE MAKANJILA**

Leo Jan. 17, S. S. Domira imetufikia hapa Likoma. Tumepata habari kidogo ginsi Domira ilivyokwenda kutafuta vyombo vya Makanjila, kama wakiviona waviharibu. Wenyewe wametuarifu hivi:

S. S. Domira ilitoka kwa Mponda kwenda Livingstonia hatta Andindi mji mmoja wa Myao. Bassi wakaenda kwa Kasembe wakamwambia, tupe mtu awe kiongozi. Wakuuongoza mpaka vikaapo vyombo vya Makanjila. Kiongozi wakapewa. Walakini safari hii Domira haikwenda kwa vita lakini kuharibu vyombo vyake. Marra wakakikuta chombo kiko pwani wala watu hapana, wakakipigia bunduki, wakashuka wakakichoma moto. Wenyewe walipoona ule moshi pwani, watu wengi wa Makanjila walishuka na bunduki zao, chuma kwa chuma kikanenekana pale. Kaptain Makwaya alipoona vifao vimekwisha akapeleka mashua kwenda kwenyi Domira akatwae vipololo, lakini mashua ikapinduka kwa mawimbi, wala haikufika.

Akaondoka mwenyewe akaingia majini apate kwenda kutwaa, lakini hakudiriki kufika, alipigwa risasi la mgongoni akafa. Wazungu wawili wa Mlemle wakajeruhiwa tu, na Wahindi wawili wakafa, wa tatu alikufa kwa maji. Waswahili 2, waliotoka kwa Jumbe, walifia pwani.

**MSIMULIZI. 535**

Makanjila alipoona vya moto baba, aliitweka bandera nyeupe ndio ya amani. Bassi Wazungu wale waliojeruhiwa, kwani hawakufa, walipoona kweli ni amani, wakavalia nguo zao vizuri kumpa zawadi Makanjila.

Halafu yake Makanjila akasema, sasa vema, nimefanya amani, je chombo changu mlichokichoma hamnilipi? nilipeni mitumba 20. Lakini wakasema, mitumba 20 hatuna, hiyo 11, tutakupeni, wakampa. Bassi hawa Wazungu wakachukuliwa na watu wake, wakafika kwenyi nyumba yake wakapewa vitanda vya kukalia, wakakaa. Wakasema tena, Twendeni mpaka huko anakokaa Makanjila, ndio mji wake wa pili, wale Wazungu wasijue kama ni hila yao, wajua kwenda tu. Kabla hawajafika tu kwa Makanjila, wale Wazungu wakauawa, wakawakata vitwa vyao wakavitundika. Makanjila akasema, ninyi watu weusi tokeni ndani ya stima yao tupate kuwachinja nao waliosalia, lakini wakakataa kutoka.

Baada ya siku mbili stima ikatolewa ikaenda zake.

Tunasikia wengi sana waliouawa wa watu wa Makanjila kupita waliouawa kwanza.

**MASASI.**

**NYOKA LITEO.**

Liteo ndilo jina lake nyoka huyu mwenyi sumu nyingi; bahati na nasibu kupona, usipoingizwa kilema ao kufa pia. Akishikwa na ghathabu kooni huvimbiana sana sana. Naye mrefu pia, na mnene pia, kitwa kinene, rangi yake kijivujivu. Bassi sikia habari, ao barua yaamusha akili,

**MSIMULIZI. 536**

killia neno lililomo humo. Siku hiyo bassi nalipokea barua itokayo Unguja kwa bwana mmoja. Bassi kama jioni nikapokea barua ile nikasoma nikatafakari maneno yake.

Waima isha nikaingia chumbani kulala, siku hiyo kweli barua ile iliniamsha akili kama ninenavyo. Na siku hiyo nimechoka kufuru sana. Nami desturi kulala saa tano ao nne nikiwa kitandani bado. Bassi nikasali nikaisha pia tena zeze liliharibika zamani, nikatwaa nikapiga hatta saa sita, marra nasikia kwanza kelele ya panya, baadaye kidogo nasikia gho! ooo! gho! ooo. Nikaondoka nikarukia kitanda kingine nikatwaa taa mezani haikolei vema, nikainulika mvunguni sioni kitu. Tena kulia vilevile marra mbili. Bassi nikamwamsha mke wangu na mtoto pia akaondoka nikainulika juu, karibu kabisa na kitwa amejikunja, kinwa wazi, machavu ameyatunisha tayari kutema mate.

Bassi nikatwaa bunduki nikamkolezea ya kwanza, ikakataa moto, akaruka juu ya kitanda tulicholala, nikakimbilia nje, naye anatambaa kiwambazani ili kunijia niliko. Tena nami nikarukia ndani kitanda kingine nikaona ananyemelea nilikokimbilia mimi kwanza. Nikampiga tako la bunduki nikamwua. Waima furaha kuu kuona amekufa huyu. P. K.

**CHITANGALI.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu. Baada ya salaamu nakuarifu, kama Jan. 23 Askofu akafika hapa, tulimtazamia sana, hatta usiku akafika, alikaa naswi siku tatu.

MSIMULIZI. 537

Jan. 27, akaenda Newala tayari ya kujitengeneza kwa "retreat," hatta Feb 8 Padre wetu akatoka kwenda Newala kwa "retreat," hiyo.

Feb. 14 Bwana Carnon akaupokea Ukasisi, hatta Feb. 15 Padre akarudi kusudi kuwaweka tayari watu wa ubatizo.

Feb. 16 Askofu akaja hapa, hatta Feb. 17, saa nne ubatizo, ilipopiga kengele utazame watu waliokuja wengi; iliponyamaza tuliingia kanisani, kanisa halina nafasi.

Bassi waliobatizwa ni waume watano na waanake kenda, na majina yao Elisha Sulemani, Luka Mselem, Yohana Martin Nakaam, Yuda Barnaba Omari, Francis Wemba: Naotni Achiwa, Hanna Akwitigani, Lea Akubena, Kate Angachiwila, Sarah Achisagamila, Tabitba Orpa Akuminganduka, Monika Akulembe, Louisa Akwajewanya, Rose Rabeka Chenyao; ndio waliopokewa katika kanisa letu, akawahubiria mambo yampasayo Mmasihiya, tena tukaimba wimbo 189 "Shangalieni leo."

Siku ile ile Askofu akawa hawezi sana homa, assubui akachukuliwa kwa machela hatta Masasi.

Feb. 20 akaingia mtu kusema salaam Bwana Weigall akikute chakula; tuliona ajabu sababu hatukusikia habari ya kuja kwake, marra tukitupa macho njiani, uwanjani twamwona, furaha ikazidi kumwona, naye akafurahi kutuona sisi. Ghafula alifika hapa.

Jan. 28 tulipoingia School assubui hatujaanza kubadili kazi yetu marra tukasikia mashindo makuu sana baraza ya kuchezea mpila, hamtuma mtoto kutazama nini? akirudi hawezi kusema anatemeka; hatoka mwenyewe

**MSIMULIZI. 538**

kutazama, ee bwana wee! kumbe Madachi askari wengi wamefunikiza baraza lile kubwa na mkuu wao Wolfrum ana askari 100, marra tena nikawatoa watoto School; na marra kuku zinaletwa kwa kuuzwa, wangine unga.

Siku hiyo Bwana mkubwa aliwanunulia askari mbuzi 7, alisema ndiyo siku aliyozaliwa Sultani wao Madachi, wakaralala hapa hapa barazani. Hatta siku ya pili wakatoka kwenda Newala; askari wawili walikuwa hawawezi miguu wakaachwa hapa siku ya tatu wakafuata.

March 1, saa kwanza assubui kengele ikalia, tulipoingia Bwana Askofu akawatia mikono watu kumi na nane wale waliobatizwa Feb. 17, lakini kwa kutiwa mikono wamezidi watoto wanne ndio hawa, - Gideon Kawanga, Mona Harriet M., Durham Chiwiwi na Neema mtoto wa Yona,

Feb. 28, tulimtazamia Bwana Weigall kuja hapa kumwona Bwana Askofu akitoka Newala, lakini tukapata barua kusema hawezi sana homa, na jana Feb. 29, amepata hajambo kidogo.

March. 3, Askofu atoka hapa kuja Unguja. H.S.M.

**MISOZWE.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu. Wabaduhu salaamu nakuarifia habari zetu za Misozwe chache na thaifu pia.

Nov. 15, alifika mtoto wa jumbe Ntununtu kule unakokwenda siku hizi upelekwa wetu huu, ndio Gonja, jumbe

MSIMULIZI. 539

Mkilindi na jina la mtoto Falu; akanipa salaamu akawa nami siku tatu; ya nne tukaagana akaenda zake.

Nov. 17, ilikuwa harusi ya kijana Mmasihiya aitwa Cecil Senyovi na mkewe aitwa Mambwana.

Dec. 1, usiku nasikia ngoma za vita upande wa kaskazini matlai; kumbe ni Wadachi na Wadigo wanatiana moto na sababu ni hii, kama niliyowaambia kwanza; walishika shauri hilo hatta ijapokuwa Wabondei wamekataa.

Dec. 12, alikuja marehem Bwana Herr Krenzler na mtu Mdigo aliyochaguliwa kuwa liwali wa Digo, naye ni Mdigo, aitwa Mwamvula. Kuingia tu mjini wakamkaribisha vema hatta kitambo kidogo wakafanya shauri wamwangamize na wale aliokuwa nao, kwani ni askari haba tu. Wakaondoka wote mjini, marra Bwana yule akitazama hapana awaye yote, ghafula aona vita mkononi naye akawa tayari wao nje, yeye ndani ya mji wao. Wakapambana utasema simba na mbogo, wasimweze, hatta wakampa njia kwa mvumo wa bunduki za Kidachi na kwa akili ya vita akakamata watatu wao wake wawili na mume, akaenda nao kwa Tanga, akawaua Wadigo 9. Na waliojeruhi hawana hesabu, yeye akaangusha askari zake wawili na jemadari Mnubi, ndipo akarejea na ghathabu tena.

Dec. 20, Wakachoma miji karibu yetu, umbali wa mayili 8.

Dec. 25, Furaha kuu kwa wote. Tulikuwa wote na furaha, ila hatukuwa na Kasisi; Christmas ya rohoni ikawa.

Dec 27, Ndipo alipokuja Kasisi kwetu.

Dec. 30, Wazee wa Kibondei wanakwenda Segga wanaitwa na Liwali mwezi wa mwisho wa siku za mwisho wa December. Imeanza homa katika inchi imeendelea hatta siku za February hatta wengi waliondoka wathani wataweza kuzuia ugonjwa ule kwa nguvu kumbe wanauzidisha.

MSIMULIZI. 540

Jan. 4, Usiku tukasikia simba anafukuza kulunga wanapita shambani mwetu.

Jan. 9, ilikuwa saa edaashara. Mvua ikanya marra ghafula hiyo umeme ukaanza ghafula tufano, ikavuma tufano. Nyumba ya Padre Woodward mabati ya barazani yote yakaondolewa mbali na miti yao pia, nyumba yote ikajaa maji juu na chini, kuvuja pote pote hatta nyumba ya matofali; lakini lilikuwa haifai jumba hilo; lakini kwa rehema na kwa uponde tumeokoka nyumbani humo. Mvua hiyo tu pasipo tufano ikatushika kwa siku tatu. Miti mingi mikubwa karibu yetu imeanguka na baathi yao imeraruliwa mbali, mahindi yote kana askari walioambiwa "Lie down" yote kwa umoja wala si huko na huko. Jan. 28 Walikuja Sisters A. Margaret na M. Elizabeth, kwa kupunga hewa siku saba Feb. 9 assubui naamka saa 12. Nalithani leo tumechuliwa hatta uwinguni kwani ukungu ulifunika pote hatta hawezi mtu kuona mbali sehemu yote ya Luale yote pia ilifumkwa hatta kwa saa ya kwanza.

Feb. 13, Muhamadi, ndiye mtoto wa yule mzee wa Misozwe aliyekufa mwezi wa August aliyetitwa Semhanda, ao Baba ya Mhando. Bassi huyo Muhamadi ndiye Mhando, hilo jina la Muhamadi alipewa na waalimu wa Kislamu alipokikubali Uislamu. Bassi huyo siku hii ya Feb. 18 amekufa. Feb. 16, nimekwenda Gonya ulipoanza siku hizi Upelekwa wetu. Nalimpeleka mwalimu Cyprian Lizani na pamoja nakwenda kuonana na wale wazee pia. Tuliokwenda ndio mimi na yeye Cyprian na Michael Mfungu na Edward Kingodi, na watoto wangu wawili Francis Nangonda na Daud Wakati; saa ya tatu tulitoka Misozwe tukaingia saa ya sita. Nikaita wazee si wote



MSIMULIZI. 541

nikaonana nao na kuwapa mwalimu wao, saa ya kumi nikarudi kwetu nikaingia saa ya thenashara.

Feb. 24, ndio siku ya Mattiya Mt. na Shahidi, saa ya saba ikipiga naona watu wawili wanatoka kwa Mwaimba, Mwalimu salam Allahu. Bwana mkubwa wa Tanga yuaja, mwekee vyakula na maji. Nisisadikishe hatta neno lo lote nikampa habari Padre Salfey kwani yupo hapa akawa kama mimi wote tusiwe na tumaini hatta lo lote la kuja saa ya nane nikawaacha watu kwenda zao.

Saa kenda nilikuwa nikitoka, hemkole napanda kwetu hatta mlima, hatupa macho kwa kaskazini matlai naona, loo, yule Bwana yuaja kweli kweli, nikahalaka nikampa habari Padre tukafanya tayari nyumba, marra twaona anapanda mlima wetu, amepanda frasi mweusi kidogo naye ndiye St. Paul. Na jemadari mwingine mtazamia merikebu ya vita naye amepanda frasi pia, na wa tatu aitwa. Fisher, ndiye akaaye Msasa, na askari asharini na wanne na wapagazi arobaini na kenda na Abdallah yule (alikuwa Liwali 1891, aliyekuwa Sega mji wa Boonde karibu ya Magila kama mayili nne toka Magila), na mkuu wa askari Wakinubi aitwa Abdallah mtu mrefu sana kupita Bwana Askofu ao labda sawa. Marra wakifika wakatutolea kufa kwa Herr Krenzler, yule Bwana jemadari akaniuliza kama atapata nyama ama ng'ombe ama kondoo anunue kwa majeshi yake. Nikamwambia ndio, akanituma nimtafutie. Bassi sikia tena karibu yetu kama mayili moja palikuwa na Washambara wanauza ng'ombe. Bassi wakiwaona wale Wadachi walithani labda tutanyang'anywa ng'ombe zetu, wakashika wakimbie wakaondoka kwendelea mbele upande wa Magila. Wakati huo mvua yanya, ndipo nami hatumwa nikatwaa mtu aitwa Kakucha kusudi anisayidie.

**MSIMULIZI. 542**

Bassi tukaondoka tukatafuta ng'ombe tukaenda tunaita. Waliposikia wakathani ndio askari kweli, bassi wakazidi kwenda mbele mbio na ng'ombe na mbuzi, wakatanguliza ng'ombe, mbuzi zikaja nyuma maana yake wakasema, Ah! haithuru hatta mbuzi zikinyang'anywa si hasara kama ng'ombe. Bassi tukawa kama tunafukuzana hatta kwa mayili labda tano kama mjini na Mbweni tukawafikia tukanunua ng'ombe kwa rupia 9, tukarudi njiani tukanunua kondoo ya rupia 5 tukarudi tukaingia saa tatu ya usiku. Tena jeshi la askari limelala majira hayo, nikamtoa kwa aliyenituma akaniambia mtunze ng'ombe hatta kucha assubui. Wakachinja ng'ombe kwa askari na kondoo kwa wapagazi. Saa hiyo akaja jumbe Makange kuwapa salaam akawaitea kondoo.

Ijuma assubui wakatoka kwenda Msasa.

March 2, tumeanza Kwaresima yetu. Ndio habari zetu chache tu na thaifu. Salaam. M. F.

**MKUNAZINI.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu. Na baada ya salaamu, nakuarifu habari zetu za hapa tukaapo chache tu. Panapo Ijumaa alituwasilia hapa Bwana Askofu akitoka Newala pamoja na Barnabas Farajala na mfalme wa Chitangali, jina lake Barnaba Nakaam, na tena watoto watano waendao kusoma Kiungani.

March 15, Bwana Askofu amekwenda kuangalia pande za Magila, amefuatana na watoto wawili wa hapa ndio Barnabas Farajala na Willie Boga.

Willie Boga anakwenda kutazama Magila kwa mwezi mmoja, kiisha atarudi tena hapa.

**MSIMULIZI. 543**

Na Bwana Faulkner alikuwa mgonjwa kwa juma tatu, homa ilimshika sana. Lakini sasa twatumaini atapata afya yake tena (kwani hajambo) na kutenda kazi yake vile vile.

Na labda baada ya miezi sita ao nane labda nyumba yetu ya wagonjwa itaisha, inatengenezwa vizuri.

March 6, ndio Juma a pili ya kwanza ya Kwaresima, walikuja mabaharia wa merikebuni kusali katika kanisa letu, pamoja na ngoma na filimbi, &c., wamechukua mikononi mwao, watu wengi wakawafuata; wakatoka saa tano. Kiisha na sisi tukaenda kwa sala ya pili. H.M.

**KIUNGANI.**

Ndugu, salaam, safari hii hapana habari nyingi illa hizi chache tu. Feb. 24, Siku kuu ya Mattiya, palikuwa na kwata Mnazi mmoja penyi kantini. Bassi jioni pamoja tulienda kutazama na tukarudi.

March 11, Askofu alifika akitoka pande za Newala na watoto watano ndio Francis Sapuli, Ambrosio Mitande, Allred Mpetula, Augustino Malemla, Bartolomayo Mmreiha, na tena mfalme wa Chitangali jina lake Barnaba Nakaam, na mwalimu Arthur Kasembe.

March 13, watoto wawili wa hapa petu walitiwa mikono Mbweni ndio Sarmwil Faraji na Tomaso Yanikore, na kwa jioni yake akafika mwalimu Karlo Mwamiu na mtoto mmoja wa Magila jina lake Samwil Mhesa.

March, 15 Askofu ameshika safari ya kwenda Bonde. Mar 16, ametufikia baba wetu wa zamani aliyetuacha kama miezi edashara, bassi tulifurahi sana tulipomwona,

**MSIMULIZI. 544**

naye amekuja na makasisi wawili mmoja anakaa Mkunazini na mmoja hapa petu, na mmoja (Engineer) labda atakwenda Nyassa, na wameletewa mtoto mmoja wa Kihabeshia na Miss Allen ametoka utumwani, naye amebatizwa kwao.

Tuonavyo Arehdeacon amepata afya sana; alipofika tulipewa naye siku nzima ya kucheza. Mtg.

**MBWENI.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Baada ya salaam:

February 27, tulipolala mnamo saa nne tukasikia makelele na kishindo kikuu. Wangine wetu wakaamka kusikiliza kuna nini? Lo! kumbe ilikuwa mtu mwivi amekamatwa, lakini usiku ule wote hapana mmoja aliyejua ni jambo gani lililotendeka. Assubuhi tukauliza kulikuwa na nini? Tukaarifiwa ya kuwa mwivi amekamatwa. Tukakaa kitambo baada ya kutoka mezani marra tukamwona mwivi amefungiwa kuku na mwenyewe amekazwa mikono nyuma aletwa kwa bwana.

March 8, chuo chetu kimetolewa boriti nusu kwa sababu mvua ikinya kunavuja, sasa wametia boriti za chuma. Twatazamia sana kiisha upesi tupate kukisomea, kwani sasa twafanya masomo yetu mezani.

March 11, tumefurahi sana kuwaona Florence na Mona waliorudi toka Chitangali kuwaangalia wazee wao.

March 15, Mfalme Barnaba Nakaam alikuja hapa akashinda siku nzima, killa mtu tulipenda kumwona

**MSIMULIZI. 545**

tangu Wazungu hatta watoto, aliangalia killa mahali, hatta kwa shamba la Ulaya la Bibi mwalimu, jioni akaenda zake.

March 26, Bibi Bennett aenda zake Ulaya kwa kubadili hewa. B. M.

**SHAMBA LA MBWENI.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu.

Baada ya salamu nakuarifu habari za hapa. Panapo mwezi wa Feb. 4, mke wa Mwalimu W. E. Kanyopolea amepata mtoto mwanamke; siku ya saba mke wa Mwalimu Harry amezaa mtoto mwanamke.

Siku ya kumi na mbili tumefiwa na ndugu yetu Mary Maua.

Siku ya 17, tuliingiliwa na mwizi akaiba kuku za mjoli mmoja. Bassi tulipompata ilikuwa shangwi sana, wake kwa wanaume, tulimfunga mpaka assubui; hatimaye akapelekwa kwa General Mathews na kuku amefungiwa.

Siku ya 21, amebatizwa mtoto wa Mwalimu Harry. March 11, ametuwasilia hapa Bwana Askofu kutoka Newala pamoja na mfalme wa huko Chitangali. Siku ya 13, watu 24 walitiwa mikono hapa petu. Siku ya 15, Titus Mataula amemwokota baharia wa Kizungu aliyetoroka, kwani walikuwa watatu wawili walikamatwa, huyo aliwaomba akae. Bassi Juma a tano tukapeleka habari kwa Bwana Mercer akatuambia, mwambieni aende zake; naswi tukamwambia akaenda kwa shidda

**MSIMULIZI. 546**

sana kwa sababu merikebu ya matanga, na waliomo ni Waingreza, nao watu humwonea sana ndio maana akakimbia.

Siku ya 17, tumefiwa na ndugu yetu Maua. Siku ya kumi na nane tulijiwa na watoro wawili wakasema, sisi tumeibiwa, tena wataka watuuze, naswi tumetoroka na wake wetu wamechukuliwa na mtoto, ndipo tulipojifunga watu wanane kwenda kunyang'anya. Tulikwenda hatta Kiungani tulikutana na wake wao kama walivyosema tukarudi. Assubui wakapelekwa kwa General Mathews; hatujui sasa yamekuwaje.

Siku hizi pana shindo la kutafuta watumwa. Bassi walio hapa kutoroka tu kwa kuogopa wasitolewe mkononi mwa bwana zao. N.F.

**VITENDAWILI.**

Mimi, Msimulizi, nimeletwa vitendawili hivi, kuwategea ninyi, ndugu zangu. Lakini mtegaji halisi ameniahidia kama mtu yee yote mweusi aliye wa kwanza kuvifumbua vyote pasipo kusayidiwa na mtu mweupe atapata Rs 3, na aliye wa kwanza wa kujibu kimoja tu atapata Rs 1. Bassi killa mtu aandike akapeleke jibu lake kwa Padre wake, Padre akatie jina lake akaseme siku ngapi tangu alipoviona mpaka kuvifumbua. Kiisha ampelekee Mtengenezaji hapa Kiungani. Majina yao watakaovifumbua yatatangazwa humo mwezi mgine.

MSIMULIZI. 547

N. B. Wale wasionitwaa mimi Msimulizi, wakivifumbua hawapati thawabu.

VITENDAWILI

1. Chombo changu kinasheheni chakula halafu chaelea kitupu.
2. Nyumba yangu udongo mtupu, watoto wangu hula watu walalao humu.
3. Sijapevuka lakini ndevu zangu nyingi.
4. Nakwenda lakini sina miguu, nisimamapo nimeharibika.

>> Pages 547-548 missing!

MSIMULIZI. 549

>> Starting June 1891

### **KIUNGANI.**

Naona mtapenda kusikia tulivyoendelea sisi miezi hii miwili April na May. Kwanza mnajua kama ilitupasa kuingia katika huzuni na halafu yake kuwa katika furaha ya Pasaka.

Bassi sisi hapa petu Kiungani Juma a mosi jioni iliyo Juma a mosi ya Pasaka, sala yetu ilikuwa kwa shangwi sana kwani haiyamkini tuwe katika huzuni, huzuni tumeitupia mbali, tena kufikiri kesho.

Bassi assubuhi yake sala kubwa ya Usharika Mtakatifu kwa shangwi na kufurahi sana kuona sisi wa hapa petu tuliokaribia Mathabahu ya Bwana ni watu mia. Tena ndugu zetu watatu waliingia siku ile ile ya Pasaka katika Chama cha Paolo Mtakatifu. Majina yao ndiyo Kolumba Y. Mzigala, Petro H. Musa, na Klementi Mkajanguya. Tukakaa kidogo ukawa mkutano kwa desturi yetu hapa. Waanake wa Mbweni na Mkunazini pia walikuja hapa Kiungani kufurahi pamoja. Bassi siku ile tulifurahi sana. Baada ya siku chache mtoto mwingine aliingizwa katika Chama cha Paolo Mtakatifu ndiye Karlo E. Lisomba. Wakubwa wetu waliona vema watupe Juma nzima ya kucheza, bassi tukacheza.



MSIMULIZI. 550

Kazi yetu huku ilikuwa nini ndio kumtazamia sana Askofu kwani twalisikia atafika Juma ile ile tunayokicheza wallakini matumaini yetu burre, aliwasili hapa Juma a pili usiku. April 24, tukiisha kumngojea siku tano, akaleta pamoja naye mwalimu Ackworth Machaku na mkewe, na watoto wake wawili Angelina Tatu, na George, nao wanakaa Mkunazini. Tena na ndugu zetu waliokuja Kiungani kusoma, ndio Mwalimu John B. Mdoe, Hugh Mhina, Alfred Juma, na watoto Lawrence Mmaka, Edward Kingodi, Yakobo Chamdangwe, William W. Ngoma, Antonio C. Mchancha, na Geldarti Senkoba nduguye mwalimu John B. Mdoe.

Lakini naona mtapenda kusikia habari kidogo za "Class Room" yetu.

Tulitumaini atakuja kuizindua Askofu wallakini sivyo, kwa ajili ya vile kuchelewa kwake. Kasisi wetu akaizindua iwe tayari kwa Juma a tatu, nayo ndiyo iliyo nzuri sana, naona katika Upelekwa wetu hapana kama hii, kwa mapambo yake pia; shukurani nyingi sana, juu yote twawashukuru waliotuchangia fetha hatta tujengewe.

Nayo tuonavyo itaelea itaelemisha watu, itakuza watu katika elimu za namna zote; akipenda mwenyewe Bwana wengine wataondokea watu wa kufaa inchi zao na kuchunga watu wao. Na ndivyo wafulizavyo watu huko Ulaya.

Na kama ukiingia utaona killa kitu kimekukalia utamu kwa kutazamisha. Na pale pale kwa Class room zamani pamekuwa Museum kwa kuwekea vitu vingine vingine kwa mafundisho yetu, napo pana taa moja. Nayo imeunganishwa na kanisa letu, kwa upande wa makaburi hatta penyi mzambarau.

Bassi ni kubwa sana, inaweza kuchukua watu 45 ndani yake. Tena tumetia sana uzuri kwa mapambo yake na desks mpya. Na kiti cha mwalimu

MSIMULIZI. 551

mkubwa kiko juu kidogo, hatta tena madirisha yako mazuri ya vioo vitupu, katikati vyuma vizuri laini vimepakwa rangi nyeusi, tena taa mbili katikati.

Na taa hizo za ajabu sana kuwashwa kwake, ungeweza kusema namna yake kama za umeme, lakini sio, hizo namna ya peke yake. Tena chumba chenyewe kina nafasi ya kupitia huko na huko, desks hazisongani. Tena saa katikati ukutani juu kidogo.

Watoto wa darasa ya pili pia wana ruhusa ya kuja na kusoma humo kama waalimu. Na mna ubao mweusi mkubwa, mbao mbili pamoja ziwezazo kupandishwa na kushushwa,

April 28. Palikuwa mkutano hapa.

Watu wa Mjini wakaja na wa Mbweni pia wakakusanyika, ikawa furaha kuu. Hatta alasiri kama saa sita unussu wakaja Wazungu wakubwa wa kisiwa hiki cha Unguja, hawakukaa sana wakakaa kama nussu saa wakatuaga wakaenda zao kwao, tena na ndugu zetu wa Mbweni na mjini wakaenda zao.

April 30. Palikuwa Kuimbato, watu wa Mbweni na Mjini wakaja na Wazungu wasio wa Mission pia. Tukapamba mno chuoni na madaraja ya kwenda chuoni, kwa bendera nyingi na taa, tukapandisha piano. Bassi jioni wakaingia wageni walioitwa kwenyi Kuimbato, "Concert" Wazungu wengi na watoto wa Mbweni na Mkunazini, hatta Mapadre wa Kifransa walikuja.

Wote tukakusanyika chuoni na nguo safi, kwa killa mtu akabadili, waimbaji wanakaa juu na wasikiaji wote chini. (Kwani chuo chetu hapa kama wajuavyo wangine upande mmoja umepandishwa juu kwa mibao iliyofanywa kama madaraja). Bassi wote kimya kabisa wakisikiliza watoto wa Kiungani wanavyoimba vizuri sana. Hatta zayidi Wazungu wakafurahi

MSIMULIZI. 552

sana si kule kuimba tu, lakini tena michezo ya Kiafrika ya Wayao na Wanyasa, ndio "Mangolongondo" na "Ching'wenyeng'wenye". Kwa killa mwisho wa uimbo wakapiga makofi. Hatta sisi tulifurahishwa mno sana na Mzungu mmoja Mr. Boustead alivyoimba sana kwa sauti yake na vizuri sana, tukacheka kwa furaha; mwisho tukaimba "God save the Queen".

Tukashuka kwenda mezani na wageni wetu, tukala tukanywa, halafu killa mtu akaenda mahali pake.

May 1. Juma a pili ya pili baada ya Pasaka walitiwa mikono watoto wanne, Samwili Mhesa, James Chuma, Austini Shukuruni, na Chad Hamisi.

May 4. Askofu wetu tumemsafirisha kwenda Ulaya akiendea shughuli kubwa ya kupeleka habari za Upelekwa wake na kutafuta msayidia mwingine kwa kazi yake awe Askofu wa Nyasa, kwani kwa yeye Nyasa ni mbali amekuwa mzee, inchi yetu imemfanya mzee, akiwa si mzee bado, kwa kusafiri mno.

Baada ya haya tukaona Chama cha Paolo Mt. chazidi kubarikiwa na Muungu. Kwani mwingine tena aliingia, ndiye Lawrence Mmaka.

Baada ya haya tena waalimu wapya walifanywa ndio Danieli Usufu, Benyamini Mtepa, Lawrence Mmaka, Kolumba Y. Mzigala, na Klementi Mkajanguya.

Baada kidogo siku chache twasikia kuwa Mr. A. Carnon na Mr. S. Weigall wapo hapa Unguja, naye Mr. Carnon ni mgonjwa pia wakitoka Newala. Hawakukawia wakaenda zao Ulaya kwa ajili ya ugonjwa.

May 10. Ulikuwa upelekwa wa ndugu zetu hapa Waalimu: George J. Swedi, na Connie Mgoma wakienda Magila pamoja na Mr. Barrett, schoolmaster, mahali pa Mr. Bone; na Arthur Mvenya, Nyasa, akifuatana na Mr. W. Pullinger, engineer.

**MSIMULIZI. 553**

May 11. Mr. Hood na Nicholas Kusi walikwenda Newala na Cecil Majula.

May 14. Akawasili hapa mtoto mmoja wa Mkuzi Herbet J. Sehiza kuja kusoma, tukampokea kwa furaha.

May 22. Ndugu yetu mwingine tena aliingia katika Chama cha Paolo Mt. ndiye Danieli Usufu, bassi twalifurahi sana tukiwahesabu sita walioingia tangu siku ya Pasaka.

May 24. Watu wote wa Chama walioko hapa walifanyiwa Siku ya Faragha ya Rohoni tangu Juma a tatu jioni hatta Jumaa tano asubui.

Siku hizi amekuja Askofu wa Mombasa kukaa kwetu, amependa sana kujua habari zote na desturi zote za Upelekwa wetu, na Askofu wetu alipata kuonana naye miaka mingi siku iliyo mbele ya safari yake.

May 30. Amefika Kasisi mmoja mpya, Mr Griffin, amefanya kazi Ulaya. Sasa amekuja kusayidia Upelekwa wetu, bado siku kumi anasafiri Magila.

May 31. Samuel Saadi ameoia mwanafunzi mmoja wa Mbweni jina lake Jumaanne. Atazidi kufanya kazi yake aliyofundishwa hapa.

**MKUNAZINI.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi saalamu. Na baada ya saalamu nakuarifu habari za hapa tukaapo.

April 6. Siku ya Pasaka Juma a mosi tulipamba Kanisani kwetu vizuri sana, na Juma a pili ndio Siku ya Pasaka, tulifurahi mno kwa nyimbo pia. Na saa nne walitokea Baharia, Ah! Si mshindo wao huo, wakauchapa mshindo mpaka mlangoni pa Kanisa kiisha wakaamrisha wakanyamaza, wakaingia Kanisani.

April 18. Sisi tulikuwa papa hapa petu.

MSIMULIZI. 554

April 19. Sisi hapa tulifunga safari ya kwenda kisiwa cha Makaburi, palikuwa na mashua tano pwani, tatu za watoto wadogo, mbili zetu watoto wa kazi, na Wazungu wa kwetu waliokwenda ndio hawa. Dr. Hine, Mr. Bishop, Miss. Dean-pitt, Mr. Faulkner, na Mr. Dalebrook wa Kiungani, ndio hawa tu. Kufika pwani, sisi tukachukua mashua iendayo upesi upesi tukapakia vitu vyote pia tukaanza kwenda. Ah! Mashua yetu si kwenda kwake huko maana ndefu sana kuliko zote, tukatoka saa tatu tukafika saa nne kasorobo ginsi mashua ziendavyo, kufika tu kutazama mwitu tukasikia kitu kinalia ndiye mzee mwenyi mji, paa, tukasema haithuru kitu ngoja halafu. Bassi sisi hupenda kucheza mno, tukachukua mashua mbili kuchezea kidogo, marra tukaacha kwani hatukuzoea hatta kidogo, ndio saa sita.

Panapo saa tissa, Bwana Daktari akarudi pamoja na watoto wadogo sababu alikwitwa kwa barua. Lakini mtaona ajabu sana aliitwa kwa nini hapana simu kwenda kule, safari hii sielezi hatta kidogo labda kwa safari ingine, hii ni ajabu sana, sababu kwa Balyozi palikuwa na watoto wanya aliitwa kwenda kuchagua watoto, na siye tukarudi nyumbani saa thenashara. Juma a tano tupo hapa hatta Alhamisi.

Tumefurahi kumwona Bibi yetu aliyetulea tangu zamani sana ndio Bibi Miss Mills atokaye Ulaya awarudiaye watoto wake tena, akatupa gharama nyingi sana kuku wengi sana.

April, 24 Tulifurahi kumwona Bwana Askofu akitoka Magila pamoja na Barnabas Farijala na Willie Boga na Moris Gari anakuja kuo, pamoja na waalimu wa Kiungani na watoto wengi wa Kibondei waendao kusoma Kiungani. Na siku ya Alhamisi ndio siku kuu ulikuwa mkutano pamoja Kiungani, sisi wote tuliitwa kwenda kumwaga Bwana Askofu sababu anakwenda zake, tulifurahi wote.

**MSIMULIZI. 555**

Na mahali hapa petu pana wagonjwa wengi sana, sasa hawezi sana Bwana Mr. Lister aliyetoka Magila kwenda Ulaya.

Barnabas Farijala na Willie Boga wameshika vile vile kazi zao sasa; Barnabas Farijala anapika hapa Mkunazini. H. M.

**HABARI ZA HUZUNI.**

Katika May 12. Twalipatwa na huzuni kwa kutwaliwa ndugu yetu mpendwa katika taabu za dunia; Mr. Albert Beetham, ugonjwa wa juma nzima tu, hatta panapo Juma-a-tano alasiri akalala, akazikwa Alhamisi. - R. I. P.

Tena June 7. Tumeletewa tena huzuni kubwa sana kwani Bibi Miss Janet Emily Campbell akiisha kuuguza wagonjwa wengi sana weusi na weupe amekufa mwenyewe leo kama kwa uchofu mtupu, akitoa maisha yake kwa ajili ya rafiki zake. - R. I. P.

**MBWENI.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu, nakuarifu habari hizi.

April 1. Ametuwasilia Miss Caffin, kwani alitoka hapa kwenda kubadili hewa, na pamoja naye alifuatana na Sister Frances aliyekuwa hawezi pia. Walipowasili Port Said ikaja simu kusema kama yule Sister aliyefuatana na Miss Caffin amefariki.

April 5. Wametuwasilia Ellen Fayida na Josephine Selenge wakitoka inchi ya Bonde.

April 12. Tumefurahi sana kuwaona Rev. Key na Mr. Brough wakitoka Ulaya.

MSIMULIZI. 556

April 15. Siku ya Jumaa Kuu, watu wengi walikuja Kanisani.

April 16. Twalitengeneza killa mahali kwa siku kuu.

April 17. Ndiyo Siku kuu ya Pasaka. Usharika Mt. ulifanyika marra mbili, kwanza kwa Kiingereza assubuhi na mapema katika Kanisa dogo. Tena kwa Kiswahili katika Kanisa kubwa. Watu walilijaza sana Kanisa, nao waliopokea Usharika Mt. ni watu 171.

April 18. Watu hawakufanya kazi walipata ruhusa ya kucheza ngoma, Rev. Key aliwachukua watoto kutazama ngoma.

April 19. Twalishinda papa hapa tukijifurahisha tu.

April 28. Makusanyiko ya Kiungani, mchana kutwa tukashinda, alasiri tukarejea kwetu.

April 30. Tukakaribishwa Kiungani kuangalia michezo, ilikuwa mizuri ya kupendeza mno ya Kuimbato.

May 2. Siku kuu ya Atanasio Asikofu wa Iskandaria, tukapata ruksa ya kucheza tu, kwa sababu ni mtu mweusi.

May 4. Tukafanyiwa karamu kuu, mwenyi kutufanyia ni Bibi mwalimu, kwani alituahidia karamu hii kwa siku kuu ya kuzaliwa kwake. Karamu hii ilikuwa ya March 4, lakini kwa sababu March 4 ilikuwa siku za kufunga hakuweza kufanya karamu, hivi ikawekwa hatta May 4.

May 6. Sikukuu ya Yohana Mwanjilisti, siku kuu yake tukapata kucheza nusu ya siku.

May 17. Ilikuwa harusi kati ya Minnie Mwalema na Maurice Gari.

May 23. Ilikuwa siku ya kuombea, na kushukuru kwa mapando. Saa tatu unusu watoto wakatoka chuoni Msalaba ukachukuliwa, na watoto waimbaji walitangulia; tukaenda njia kuu tukapita pwani ya balyozi tukapanda kilimani tukatokea nyumbani. Tukaanza

MSIMULIZI. 557

kushuka pwani vile vile. Njia nzima tukiimba, tulipokwisha kuzunguka shamba zima tukafikia Kanisani, sala ya jioni ikaanza.

May 26. Ikawa siku kuu ya Kupaa, twalicheza papa hapa. Miss Boyd amerudi Mbweni tena, akitoka Mkunazini afanya kazi ya kufundisha Chuoni vile vile. B. M.

### **SHAMBA LA MBWENI.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam sana. Uwe rathi sina habari nyingi safari hii. Mwezi wa April tulitokewa na mtoro, na bwana akampeleka kwa balyozi.

Juma a pili ya mitende tulizunguka sana Kanisani. Na siku ya Juma kuu tulikwenda Mjini mimi na mwalimu W. E. Kanyopolea, tuliona habari za fimbo watu wawili wamekufa, na askari wametapakaa Mjini watafuta waliowaua.

Siku ya Pasaka ilikuwa furaha hapa petu, zilichezwa ngoma mpaka jioni.

April 21. Tumemkamata yule mwizi wa siku zote, Akapelekwa kwa mwamuzi.

April 23. Mwalimu W. E. Kanyopolea ameuua chatu mkubwa sana.

April 29. Tulikwenda Kiungani kwa siku kuu.

May 18. Ilikuwa harusi ya Adamu.

May 21. Tumefiwa na mwanafunzi mmoja.

May 23. Ilikuwa kulalia Siku kuu ya Kupaa, bassi ilikuwa kufunga, naswi tulilizunguka shamba lote. Killa palipopita mpaka, na Msalaba wetu kwa shangwi, na watu wengi sana, na Makasisi wetu wawili.



MSIMULIZI. 558

May 25. Kwa jioni tuliingia Kanisani kwa heshima kwa Siku kuu yetu ya Kupaa.

Juma a mosi tulifiwa na Mmasihiya, jina lake Rikado Baraka. Juma a pili maziko. Juma a pili ya kwanza baada ya Kupaa, panapo saa nane mke wa Nicholas Faraji amepata mtoto mwanamke.

May 31. Tumefiwa na Mmasihiya tena, Hilary Ng'andu naye hakuugua siku nyingi na leo amekwisha kumalizika, na kesho maziko. N. F.

### **MAGILA.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi, salaam. Baada ya salaam nakuarifu kama katika mwezi wa Jan. 6, Alibatizwa mtoto wa Yohana Lugulu, jina lake Mattiya. Na katika mwezi uleule siku ya 24, walibatizwa watu 17, waume wasita, mtoto wetu mmoja wa nyumbani ndiye William Waynflete Ngoma; na wake 11: ilikuwa siku kuu ya Paolo Mtakatifu.

Feb. 4, Akaingia hapa Mdoicha, akalala papa hapa. Assubui akaja kwenyi School yetu kuonyesha ginsi alivyo hodari kuandika sanamu. Bassi akawekewa ubao (blackboard), ah! Mdoicha huyu wa peke naye, kapea kabisa kabisa kwa elimu hiyo. Vitu vingi alituandikia sanamu ya askari wa Kinubi, mlima wa Kilimanjaro (naye atoka Kilimanjaro), Simba, nyumba &c. Naye aandikapo hafutifuti na kitambaa, huandika tu, chapchap naye, kama haandiki; baadaye tukampigia makofi, akaenda zake Tanga.

Siku hii hii saa nne wakawasili Mr. Ford na Mr. Allen wakitoka Unguja, pamoja na Mwalimu Lawrence Kombo naye akitoka Unguja kwa kuwapeleka akina Charles J. Mkumbukwa James na Chuma.

MSIMULIZI. 559

Feb. 8, Tukahama. Kanisa letu limepata fundi Mr. Allen, bassi likaanza kubomolewa, kutolewa boriti zote na kutengenezwa vizuri zayidi. Na kanisa letu sasa ndio ile school yetu, na school yetu ndio chumba cha kulia watoto. Twatumaini miezi minne mitatu litaisha, tuhame, kwani ile school haina nafasi kwa Wamasihya.

Panapo Feb. 11 Mr. Roberts akashika njia akaenda zake Ulaya, akimpeleka Mr. Edwardes aliye hawezi akitoka Unguja akamkute Tanga. Bassi sasa hatuna School-Master, illa naangalia mimi kama vile niwezavyo mahali pake, kwani si kama Kiungani ao jambo lishindalo mtu, na hatujui lini atarudi, ao harudi labda, hatujui. Je, rafiki yetu, Mr. Bone ao Mr. Kerlake mtarudi lini, anga mtuelimishe?

Feb. 23, Watoto wa Mkuzi wakaja hapa. Hatta panapo assubui yake siku kuu ya Mattiya, watoto tu wa Magila na wa Mkuzi walishindana mpila. Watoto wetu wa Magila walishinda, bassi ilitufurahisha zayidi, lakini nao wa Mkuzi walijaribu kama wawezavyo; lakini Magila, ni Magila; sio Mkuzi.

March 15. Panapo saa kenda akafa mtoto wa Robert Makange, alikuwa hawezi kifua; ni mtoto mchanga kabisa, hajabatizwa; akabatizwa mbele hajafa wakati uleule, jina lake Mary. - R.I.P.

March 17. Siku hii assubuhi panapo saa tatu akawasili Bwana Askofu akitoka Unguja, tukamfurahia hatta siku yote hii hatukusoma, na assubui yake siku ya Ijumaa akatoka hapa, akaenda kuangalia Mission mpya Korogwe.

March 19. Mkewe mwalimu Lewis Bondo akapata mtoto mwingine wapili, mke naye.

March 20. Wakabatizwa watoto wawili wachanga, mume na mke, Lewis na Anna.

MSIMULIZI. 560

March. 23. Askofu akaturudia tena akitoka Korogwe hana nguvu kabisa.

March 25. Siku kuu ya Kuhubiriwa kwake Bikira Maryamu wakabatizwa watoto 15 na mama mmoja wa nje; watoto wetu wa nyumbani ndio, Francis Mzimba, Harry Kidungwe, Charles Daudi Mfuko, Rafael Nyungu, John Janson Mbaruku, Henry Charles Semngindo, Benyamin Kingodi, Amani Mngodo, Stefano Sekitula, Henry Janson Mdimu, Nataniel Bungulu, Mikael Gao, Mikael Mwamtalu, Petro Kukuti, Yusuf Hiza, na mwanamke ndiye Blandina Bahati.

Katika March 29. Juma a nne hii usiku Wazungu wakaanza Retreat (siku za faragha ya Rohoni), hatta Jumaa usiku.

Twasikia kama Bwana mkubwa wa Tanga Herr Krenzler alikuwa hawezi sana, hatta akapelekwa Bagamoyo akapate hewa ingine, lakini akafa. Bassi twamsikitia sana, kwani alisayidia watu kwa killa jambo jema awezavyo, hatta wengi walimpenda. Na sasa ameingia mwingine mahali pake ndiye Baron Von St. Paul, aliyekuwa akishika forotha zamani Unguja. Na tena Herr Krenzler alimweka askari mkubwa wa Tanga (siye Mnubi), mtu hodari sana, kuwa liwali mahali pa Abdallah Gugu, ndiye anayehukumu siku zote tangu alipoondoka Abdallah Gugu; ni mtu mwema kwa upande wake, anakaa palepale Sega mji wa maliwali.

Siku hizi mwalimu Granville akaa pande hizi za Magila upande wa Kwamkuluwi, mji uitwao Hemsuza; naye anapata watoto zayidi ya 60 ao 70. Na mwalimu Herbert Feruzi anakaa Potwe. Angalieni majina ya waalimu mtaona mahali pao hao waliooa siku hizi, na wangine hawajaanza kukaa mahali pao, mtajua zayidi Msimulizi ujao. Kwa herini. J. B. M.

MSIMULIZI. 561

**NEWALA.**

Salaamu kwa Mtengenezaji wa Msimulizi. Nathani tumechelewa kuleta habari zetu. Bassi utuwie rathi.

Jan. 27 Tulifurahi kumwona Bwana Askofu. Bassi assubui tulipotoka hapa kwenda kumlaki kwa kijiji kimoja cha Mmakonde jina lake Naliogo, tukamkuta kule tukamleta kwetu kwa furaha, na bunduki nyingi.

Jan. 29 Wadoicha wawili walikuja hapa, na askari 100, Na mdoicha mmoja alikuwa Bwana mkubwa wa Lindi. Nao walikuja kufanya upatanisho kati ya watu wa hapa na Maviti kwani, walikuwa hawapatani kwa siku nyingi bassi sasa ni amani kabisa.

Feb. 2, Wadoicha walitoka hapa na Mfalme Matola kuwaendea Maviti kwani, ndiko ilikokuwa baraza. Hatta Feb. 7, wakarudi, siku ya pili wakaenda zao Lindi. Siku ileile Padre Cecil Majaliwa alitujia, kusudi ya "Retreat " Bassi Alhamis, Feb. 11, wakaanza "Retreat."

Feb. 14, Ndio Juma a pili, Bwana Carnon aliamriwa Ukasisi, bassi ikawa furaha kuu na watu wengi waliokuja kushuhudia. Bwana Cecil alituhubiria kwa Kiyao watu wakapendezwa sana. Juma tatu Bwana Carnon akatoa ushrika marra ya kwanza. Siku ileile tukamwaga Padre Cecil akaenda zake Mlolela, alasiri tukamwaga Askofu, akipitia Mlolela kwenda Masasi, na baadaye safari ya pwani, Pamoja naye tukasafirisha watoto wetu watano kwenda Kiungani ndio Francis Sapuli, Alfred H. Mpetula, Ambrosio Mitande, na Bartolomayo Mmeriha.

Feb. 21, Tukapata habari Kama Mr. Weigall yupo Chitangali, tukastaajabu sana kwani habari za ghafula tu hatukuwa tukimtazamia. Tukaanza kufurahi kwani ni rafiki wetu wa zamani.

Feb. 23, Akaja hapa, ikawa furaha sana kwa watu wote kumwona.

**MSIMULIZI. 562**

Bwana Askofu aliwatia mikono watoto 5 wa nyumbani. Ni mwezi huu tulipata furaha sana kuwaona watu 39 wakifanywa Waanafunzi kwa siku moja. Kwani naona hapana siku iliyo kuu kwa kuwafanya Waanafunzi kama siku hiyo. Nayo ilikuwa siku ya 20 ya mwezi huu, walikuwa waume 11, waanawake 28.

March 27. Bwana J. Hainsworth alitoka hapa kwenda Masasi kwani tulisikia kama Bwana Carnon mgonjwa bassi yeye alikwenda kumsayidia. Juma nne March 29. tukapata habari kama hajambo kidogo, lakini Bwana Hainsworth hajarudi hatta sasa. Salaam. D. M.

**CHITANGALI.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu habari kidogo tu.

March 25. Wamebatizwa watoto wadogo watatu, mmoja wa Yohana Nakaam, wa pili wa Luka Luya, wa tatu wa Adamu Twanje. Na siku ile ile ilikuwa ya furaha kwa kuwaona watu kumi na nne walipokea marra ya kwanza Siri Mbarikiwa.

April 5. Bwana Cecil na mimi pamoja na Wamasihiya twalienda kwenyi mashamba, na Padre wetu akabariki mavuno ya watu, kiisha tukarudi.

April 10. Juma a pili ya Mitende, assubuhi tulipotoka Kanisani kwa sala ya assubuhi, tukaiona nyumba yetu inaanza kuanguka, bassi wakaja Wamasihiya na Waanafunzi kusayidia kuhamisha vitu, ndio msiba uliotupata.

April 11. Nyumba yetu ikaangushwa.

April 12. Ndipo zikaanza kusimamishwa nyumba mbili ndogo mahali pa nyumba ile kubwa.

MSIMULIZI 563

April 16. Assubuhi tulipamba Kanisa letu, alasiri saa kenda unusu marra tukamwona mfalme wetu Barnaba Nakaam akatuwasilia hapa kwani alifuatana na Bwana Askofu kwenda Unguja, siku hiyo watu wote walikuja kumlaki njiani mpaka mjini kwa bunduki na vigelegele. Jioni ilikuwa sala kubwa sababu ni siku mbele ya Pasaka.

April 17. Ndio Pasaka siku ya furaha mno, saa kwanza assubuhi Siri Mbarikiwa, na saa nne sala ya assubuhi, watu wengi waliokuja.

April 19. Walikuja hapa watoto watatu wa Newala kutembea.

April 26. Walifika hapa Wazungu wawili hawawezi wanakwenda Unguja ndio Bwana Weigall na Bwana Carnon.

April 27. Wametoka hapa kwenda Lindi.

April 29. Bwana Padre wetu alikwenda Masasi kuwatolea Wamasihya wa huko Usharika Mtakatifu sababu kule hapana Kasisi.

May 5. Bwana Padre wetu ametuwasilia hapa, tena May 6, mwalimu Cyprian H. Chitenje amekwenda Lindi kutafuta vitu.

May 11. Nyumba zetu zimeisha kujengwa.

May 12. Tumeanza kuhamia nyumba yetu mpya. Tumepata habari za Makwangwara kama wapo Masasi, na mji mmoja wa Wamwera umeteketea, mmoja jina lake Kwilulu, kiisha tumesikia kama wataleta mkuki hapa kwa Mzee Barnaba Nakaam aangukie miguuni, lakini Mzee B. Nakaam anakataa kabisa.

May 13. Mwalimu Cyprian H. Chitenje amerudi hapa kwa safari yake ya Lindi.

May 10. Chuo cha watoto inanza kujengwa ya watoto waume na watoto waanawake. H. S. M.

MSIMULIZI. 564

**NYASA.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam sana. Baada ya salaam, nataka kuwaambieni habari tulizosikia kwa barua za ndugu zetu wanaokaa huko, sijui kama nitaendelea kueleza habari zote kwani nina huzuni sana kwa kusikia habari zao.

Tumeambiwa na mwalimu Augustiue zile habari za ndugu yetu aliyekufa Unguja; walipata habari mwezi wa Feb. 13, Bassi ulikuwa uthia mwingi sana kati ya waalimu na wazee wa yule mtoto, na juu ya yote ni kwa hawa ndugu zetu wawili Mr. Johnson na mwalimu Augustine Ambali.

Kwani yeye anakaa pale pale wanapokaa wazee wa huyu mtoto; bassi siku hiyo ya kwanza ya kuwafikia habari hizi walifanya uthia, babake na mamaye walikwenda kwa mwalimu Augustine kupata habari za mtoto yule, na huyu mwalimu alijaribu sana kuwaeleza kama alivyoweza, lakini mioyo yao haikutulia, na mamaye alitaka kujisonga kuko huko kwa mwalimu Augustine, na babake akataka kumwua huyu mwalimu kwa mshale; lakini kwa sababu walikuwapo watu wa kumtuliza; na jina lake mtu huyu Anjelenje. Na sasa huyu Anjelenje kabla uthia haujaisha, akashikwa na ugonjwa akafariki.

Bassi huzuni nyingi sana aliyo nayo mwanamke huyu, kufikiri habari za mumewe na kufikiri habari za mtoto wake, lakini hatujui yatakavyokuwa, kwani tunasikia marra kwa marra huyu mwanawe anataka kujiua lakini watu tu wanamzuia. Na Mr. Johnson hana mahali pangine pa kwenda siku hizi isipokuwa anashinda palepale Msumba.

Kwani yeye anajua sana habari za kule ametwaa kitu kidogo amewapa wapate kutulia kidogo.

Na Magwangwara siku hizi wanaanza kuwasumbua watu wa pande za Nyasa lakini hatuna habari nyingi. Kwa herini. J. H. M.

MSIMULIZI. 565

**KOROGWE.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu baada ya salamu, nakuarifu habari chache za huku tuliko.

Tangu bwana Lister kutuondokea hapa, tumekaa; hatta siku ile kuu ilioitwa Jumaa kuu sisi sote na watoto pia tukatoka kwenda Magila. Tukalalia Hemsuza pa mwalimu Grariville Ngoda asomeshapo. Siku ya pili yake tukaingia Magila, ndio kulalia Siku kuu ya Pasaka. Tumefurahi sana kuonana na jamaa zetu, na watoto wa Korogwe walifurahi mno kuonana, na watoto wa Magila wangine wasiowajua kabisa. Tukakaa Bonde mahali pa juma mbili, nami haenda zangu Mkuzi kufunga vitu vyangu, na kumchukua mke wangu kuja zetu huku Korogwe.

Kule Magila May 1, watoto wetu wa Korogwe wawili, Kidungwe na Mgaya, wakafanywa waanafunzi, ndio matunda yetu ya kwanza hapa.

Panapo May 2. Tukashika safari ya kuja huku, tukalalia pale pale pa mwalimu Granville, asubui tukatoka; tukasumbuka sana na maji ya mitoni na utelezi na matope, sababu kwa siku zilizopita ilikunya mvua nyingi sana. Illa tulijaliwa siku hiyo hapakuwa mvua wala jua kali, tukawasili huku jioni kama saa mbili. Watoto wafurahi mno kwa kurudi kwao



MSIMULIZI. 566

tena, na wazee wao kathalika sababu walikuwa wakiwatazamia sana. Killa mtu huku ana huzuni sana kwa kusikia kama bwana Lister amekwenda zake, Wazigua pia, kwa ginsi ya kumpenda.

Tulipofika huku watoto wakapata ruksa kwenda kwao kuamkia wazee na ndugu zao kwa siku chache, kiisha wakarudi tena; ndio tukaanza kazi yetu ya kusoma.

May 27. Mtu mmoja wa Korogwe, naye mzee ameuawa na Wazigua shambani kwake, sababu ya masa ya mtu mwingine tu. Ndio yaonyesha kama inchi hii haijatulia, machafuko matupu hatta sasa. Wazigua wawavizia Waluvu dayima kuwakamata, na kuwaua kwa masa yao ya kale; Waluvu hawana shauri moja ni watu wanaojiona killa mtu ni jumbe katika mji, na mtaa wake, kama ilivyokuwa Bonde mbele Dachii hajaitawala na kuitisha na kuweka Liwali. Nathani kathalika na inchi hii yahitaji vile vile. Kwa ginsi inchi isivyo na shauri moja, na mkuu ao wakuu wa kutengeneza maneno, mambo mengi yafanyika yasiyo ya sheria. Hatta gulio letu tungali na mashauri nalo bado.

May 28. Panapo tukatengeneza gulio letu la Korogwe. Siku iliyo mbele iwe gulio, siku ya Jumaa tukaenda tukafunga kamba gulioni ya watu wanunua bei wasimama upande, wauzao upande wao, na biashara ya nguo upande wao. Assubui ya Juma a mosi ndio siku ya gulio letu, dayima litakuwa siku ileile. Tukajivalia wote hapa wa petu kama tulivyoweza tukaenda gulio, nami haandika amri za kuwasomea watu waingiapo wengi mbele ya kuuziana vitu. Naliwaambia maneno ya amani, ni gulio la inchi nzima, mume na mke, mzee na kijana, na aina zote za watu wajao gulio. Hapana

MSIMULIZI. 567

kupigana ao kuvunja gulio, wala uthia wo wote, hapana kutoa ushuru kama walivyothani itakuwa kwa sababu gulio ni la Mzungu; lakini hawajulisha kama si la Mzungu tu wamefanyiwa liwafae watu pia. Tukathubutu kunyamazisha watu kwa shidda, wakanyamaa, ndipo hasimama kati na wenzangu, hawasomea amri hizi. Sababu watu wa inchi hii hawajui gulio vema vitu vikija, kama Wasambala wajapo na ndizi, na killa aina ya kitu, Waluvu hunyang'anyia wanunue, billa kufika gulioni, ndipo tukawatuliza kwa amri hizi. Sasa gulio letu tulilofanya bidii kulifanya lastawi, watu wengi wengi wajao, Waluvu, wa pande zote, Wazigua, Wasambala na wengine. Na wote kuuza bei zao kwa thamani sawa sawa. Kwa maneno, na amri hizi tulizozitoa zimewapendeza wote. Sasa inchi nzima imeenea gulio Korogwe la Mzungu, la mani, pasipo uthia wo wote. Na jina hili Kizungu ao Mission ya Korogwe linaheshimiwa kwote kwa msaada wauona katika inchi yao.

Na kazi yetu ya Dini nayo yaendelea kwa msaada wa Muungu astawishaye na afanikiaye kazi yetu hii ya kueneza Anjili. Kama mlivyoona katika Msimulizi uliopita kama tumepata watoto wa kukaa nasi na kusoma Mission. Sasa Juma a pili ya leo ni ya kwanza baada ya kuwaarifu kama killa gulio bosi ni siku ya Mulungu twapumzika na kumwabudu Muungu, bassi jana watu wa Korogwe wameanza kuungana nasi, na kuabudu pamoja nasi, baadaye nikawahubiria kuwaeleza ginsi ya kuabudu ni nini? na Kuabudu Muungu, ni nani? Assubui wakaja nussu, sala ya jioni wakakusanyana, wengi wakaja, watu wazima. Ndio Juma a pili ya kwanza kupata kusanyiko kuu la watu tukaao nao inchi hii, wa hapa twatumaini

MSIMULIZI. 568

sana sasa kama watakuwa wakija killa Juma a pili, ndio furaha yetu kuu. Siku zote ni thahiri, palipo na nia pana njia.

Ni watu watakao kufanyiziwa tu wakajifayidia nafusi zao, lakini kujisayidia nafsi zao kujua kama jambo lastawisha inchi na kufaa watu wote, haya ya gizani kwao.

Wajua habari ya furaha tena ni hii. Sasa waanake nao wameanza kuja kusoma, kazi yaendelea kidogo kidogo, wafundishwa na mke wangu. Kwani ilikuwa vigumu na shidda sana kwanza. Tena wengi hawadumu katika kufundishwa mpaka wasilimke na kuacha desturi zao kidogo. Ni kweli maneno haya: (Desturi ndio Mfalme wa ulimwengu pia). Bassi huku desturi amezidi kuwatawala kuwa Mfalme mwenyi nguvu juu yao. Killa ukiwaambia kwani mkafanya hivi, nanyi mwajua kama inchi nyingine pia hawafanyi, ni upumbafu sana huu. Wasema tufanyeje? Ni desturi ya wa kale wetu nasi twashika milimo. Hatta watu wangine wakiyaona ni mapumbafu sisi yatufaa. Sasa wengi kadri waja killa Juma a pili kumwabudu Muungu.

June 20. Edward Nyange karani wa Meta aenda Bonde kwa wakati chache kuamkia jamaa zake. Labda ataturudia baadaye. Sasa Meta amemleta Ackworth Gia kukaa mahali pake.

June 18. Leo Korogwe pamekuja wanubi askari na wapagazi waendao safari ya Kilimanjaro wakataka kufanya uthia, na watu kwa kutaka wapewe mbuzi. Watu wakanijia kunieleza nikawasayidie, kwa nguvu hashuka haenda kuwatuliza, wakawa rathi kwa unga, na kuku walizopewa.

June 18. Leo mtoto wa Jumbe Ngoma, Msambala Semlugu akaaye Usambaani amekuja kujulisha kwetu

MSIMULIZI. 569

kama ataacha watu wake waje gulio kama tulivyohitaji, na watoto wa kusomesha. Wazee wa inchi hii wamekuja niomba ruksa kama waenda kwa mfalme Kimweli kumwamkia, sasa wamekwenda.

June 11. Sasa ndio balaa kuu lililowapata Wamasai, njaa imeingia kwao na sasa wala ugali, na tena wauzwa, na wengine wapita njia hii wakipelekwa pwani, huko wadanganywa, wakija Zigua waambiwa na watu kuwadanganya tu: wengine huambiwa twendeni kwetu kuna chakula, bassi wafuata, huko waenda kuuzwa. Ah, nani aliyejua kama Mmasai atauzwa? Ndiyo yafaa tujifunze, Muungu humthili huyu akamwinua yule. Hatta hapa wamefika wanne waume wawili, wake wawili, wamekonda sana na chakula hawawapi waona njaa sana. Ginsi wanavyoshutumiwa na watu, enyi tungewanunua tukawaueni nyie mliokuwa mkituua na kutunyang'anya ng'ombe zetu. Sisi hapa twalikuwa na mihindi mibichi shambani tukachuma tukawapelekea, na tukawakokea moto wakachoma wakala, na Mhindi wetu Dosa akawapelekea nguo na kanzu akawavika, akawapa pesa killa mmoja, hawajui pesa nini, wathani wamepewa uganga, wasema, na wasikiaio Kimasai hutuambia wasemavyo, lakini tukawaambia watu wanaowashutumu, kama ni balaa la Muungu hili msiwacheke wamepigwa na Mola mwenyewe, tukumbuke yetu ya kesho twajuaje Muungu atakavyotutenda labda zayidi ya haya kwa ubaya wetu. Usiku walipokwenda kulala mmoja wao mwanamume akakimbia, assubui wakamtafuta wasimwone. Bassi waungwana warudi Masai wameshuka na wengi, Wamasai wamethoofika, waanaake wasichana, watu wazima, waume na wake, ah! vyatia huruma, na wengine wadogo wachukuliwa mabegani, waenda pwani utumwani. H. N.

MSIMULIZI. 570

## **MKUZI.**

Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu sana. Baada ya salaamu nakuarifu kama Bwana Woodward na Dale walikwenda Kwemnyese tulikofanya mashauri kujenga chuo pale na kuweka mwalimu; illa wenyewe walikataa kupokea mwalimu.

Bassi katika mji ule pana kijana mmoja aliyekaa hapa zamani, anajua kusoma illa bado kubatizwa. Na wazee wa mji ule Ewemnyese tulipokuja huku kwetu Mkuzi, wakamwingilia yule kijana na kumwambia, "Wewe ndiye unayetuletea Wazungu! Bassi hatukutaki humu mjini mwetu, toka katafute mahali pengine ukae." Na yule kijana akaenda mji mwingine akakaa.

Hatta panapo March 8. Akatuwasilia hapa mwenyewe, akatuambia; "Nimefukuzwa na wazee wa mji wangu, kwa ajili ya wewe Mr. Dale na Mr. Woodward mlipokuja kutaka kuweka mwalimu kule kwetu Kwemnyese." Bassi ndugu, ndivyo alivyotuelezea mwenyewe, jina lake huyu kijana ndiye Mayange, naye yupo hapa sasa anajaribia kujifunza zayidi, labda halafu ataenda kuwekwa mahali kufundisha.

March 12. Mwalimu Henry Nasibu aliondoka hapa kwenda Korogwe.

Panapo March 18. Alituwasilia hapa Joseph Hapiuwa kutoka Unguja.

April 1. Aaron Amwitamno na mkewe wamefika hapa kutoka Magila wanakwenda Unguja.

April 8. Akatufikia Bwana Askofu, ah! tulifurahiwa sana kumwona.

Panapo April 9. Wakafika hapa Wazungu wawili wakati wa mangaribi kutoka Tanga wanaenda Lewa, mmoja wao Mdachi na wa pili Mwingereza.

MSIMULIZI. 571

Panapo April 15. Ndio siku ya Jumaa Kuu wakati wa jioni tulionyeshwa sanamu za mateso ya Bwana wetu.

Na Juma a mosi ilio vijili ya Pasaka alibatizwa mtoto moja hapa, ndiye Kathbeti Mlangwa, ah! tulifurahiwa sana kupata jamaa wetu mwingine.

April 17. Ndio Pasaka yenyewe, Bwana Dale aliweza kututolea Usharika Mt. tu, illa kwa Sala ya Assubui hakuweza kuja, kwani alipatwa na homa naye hajapata nguvu bado, tena Rev. John Swedi alienda Magila kumsayidia Bwana Askofu.

Panapo April 18. Ndipo tulipata ruksa wa kwenda kukaa kwetu muda wa Juma mbili. Na jioni yake akafika Bwana Askofu na watoto nussu wa Magila kwenda Unguja kusoma Kiungani. Na siku yat pili yake mwalimu Henry Nasibu alifika hapa kutoka Korogwe pamoja na watoto wake wanne.

Hatta panapo April 30. Mwalimu Henry na mkewe walitoka hapa kabisa kwenda zao Korogwe, na kazi ya kufundisha watoto wa kike inashikwa na Rev. John Swedi. Na siku hii ndipo watoto wetu waliporudi tena.

Panapo May 11. Mtoto mmoja wa hapa alienda Kiungani kujifunza zayidi, ndiye Herbert J. Sehiza. Na siku hii usiku mwezi ukapatwa, ah! ilikuwa makelele sana usiku, watu wakagongagonga vitu pamoja, na Waislamu wanasali usiku, kusudi mwezi upate kuachiliwa, kwani ndio desturi yao.

May 15. walitiwa watu wawili kuwa waanafunzi, ndio Mayange na Mpela.

Panapo May 13. Alifika George Swedi kutuangualia, hatta May 16, akaenda zake Magila. Hatta athuuri siku ileile, akafika Mdachi mmoja kutoka Lewa anaenda zake Tanga.

**MSIMULIZI. 572**

May 24. Akafika M. Gari na mkewe kutoka Unguja wanaenda Magila.

May 26. Ndio siku kuu ya Kupaa tulikwenda kwenyi sala ya Usharika Mt. tu, hatta tulipotoka tu sisi na Padre wetu tulikwenda Magila, hatta Juma a mosi tukarudi, illa Padre tulimwacha huko, kwani ana homa.

Panapo May 27. Ah! bwana, panapo kama saa pili unussu walitokea Wadachi wawili kwa njia ya Pangani na wapagazi wao kama 327, na punda kama 30, tangu hiyo saa pili unussu hatta saa saba wanaingia tu, nao walifunikiza pote palipokuwa na uwanja wetu wa mpila wa zamani, hatta katika shamba letu lenyi migomba pia walijaa: na katika mji wa Mkuzi, na Kwe-Baa pia walijaa, na kulala kuko huko nje.

Hatta Juma a pili May 29. Waliondoka hapa asubui wakaendelea mbele, kwani wanaenda pande za Kilimanjaro.

Panapo June 11. Palikuwa na arusi ya mtu mmoja mwanafunzi, hatta mkewe pia naye mwanafunzi; jina la mume ndio Mngoma, na jina la mke ndio Matengu. A. A. S.

**MAGILA.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu kama katika mwezi wa March 29 wakaja watoto wa Gonja na mwalimu wao Alfred Chambo, kwa siku kuu ya Pasaka na kufurahi pamoja na watoto wenzao wa chuoni hapa Magila.

MSIMULIZI. 573

April 2. Bwana Lister na Bwana Ford wakaenda zao Unguja: na pamoja nao Sister Frances mgonjwa akipelekwa na Sister Margaret amfikishe Tanga, bassi wakaenda zao Unguja ndani ya mail, na Sister Margaret akarudi.

April 3. Katika Juma a pili hii Bwana Herbert Allen akaamriwa na Bwana Askofu Msomaji wa kanisa. April 8. Walitiwa Mikono watu kama 30, na watoto wa nyumbani walikuwa 15.

Jumaa Kuu yetu watu wengi walikuja, lakini hawakupata nafasi, kwani twasalia School, kanisa letu likatika kutengenezwa halijaisha bado.

April 16. Siku ya Juma a mosi mbele ya Pasaka wakaja watoto wa Korogwe 13, pamoja na mwalimu wao Henry Nasibu. Pasaka yetu ilikuwa ya furaha sana, ginsi ya watu wengi, tena kufurahia siku kuu. Sala ya Usharika Mt. watu 135 walioshariki. Na katika Sala ya pili, watoto wasio waanafunzi wake na waume tukaenda kusali katika kanisa kubwa linalojengwa, watu wengi sana waliokuja. Huko Kanisani kwenyi Wamasihiya, hapana nafasi kwa ginsi ya wingi wa watu. Katika siku zote hizi ni Askofu peke yake, tangu Ijumaa Kuu, Padre Woodward ameenda Misozwe kwa siku kuu, na Padre Salfey Msaraka kwa kazi ileile.

Siku hizi Kanisani wanaingia Wamasihiya tu na waanafunzi siku zote, wale wasio waanafuzi wakati ule Wamasihiya na waanafunzi wakisali, wao hufundishwa mahali pengine, chuoni, ao pengine. Isipokuwa wakiruhusiwa ndipo huingia kanisani, kama sala ya Juma a pili jioni wapate kusikia mafundisho.

Katika siku kuu hii jioni yake ikawa Kuimbato, mwalimu John B. Mdoe akaaga watoto wa Magila, kwa kuwaimbisha na kufurahisha watu, watu wengi



MSIMULIZI. 574

sana walikuja kuangalia, ikapendeza sana. Assubui Juma a tatu, watu wakafungafunga vitu vyao, hatta alasiri Bwana Askofu akatoka hapa kwenda Mkuzi kwa safari ya Unguja, pamoja na mwalimu John B. Mdoe, Hugh Mhina, Edward Kingodi, Lawrence Mmaka, Alfred Juma, William W. Ngoma, Antonio, K. Mchancha, Yakobo Chamdangwe, pamoja na nduguye John Mdoe, Geldart Senkoba, waendao Kiungani kusoma, wangine wao ndio safari yao ya kwanza.

April 19. Watoto wetu wa school wakapewa ruhusa kwenda kwao kwa juma 3, hatta May 7 warudi hapa.

April 27. Ackworth Baruti amepata mtoto mume amebatizwa siku hiyohiyo ya kuzaliwa, kwani alikuwa katika hatari kuu, jina lake aitwa Henry.

May 1. Watoto wawili wa Korogwe wamepewa misalaba, majina yao ndio Kidungwe wa pili Mgaya.

Huu ndio mwanzo wa mbegu, tazama si watu wakubwa ao watu wazima. La! ni watoto tu waliofunuliwa njia ya Muungu, twatumaini halafu wataendelea na kuwa Wamasihya katika inchi yao.

May 2. Mwalimu Henry N. na watoto wake wakarudi kwao Korogwe, safari hii mwalimu Henry Nasibu amemchukua mkewe kukaa kule.

May 11. Wametuasilia hapa Wazungu wageni, mmoja Kasisi aitwa Mr. Chambers, na mmoja Schoolmaster aitwa Mr. Barrett, Twafurahi kumpata Schoolmaster kwani tangu kutoka Bone hatukuwa na Schoolmaster. Nao wamekuja pamoja na waalimu wawili wa kukaa hapa kwa kazi ya Ohuoni, ndio mwalimu George Swedi, na Constantine Mgoma.

May 25. Tulifurahi kuwaona Maurice Grari na mkewe wakitoka Unguja. Katika siku hiyo ilikuwa Sala kubwa jioni yake, kwani ndio siku iliyokuwa mbele ya Kupaa. Watu wengi walikuja. Kwani

MSIMULIZI. 575

Sala ilikuwa saa 12, kengele zikaanza saa 11 unusu. Tulisali Sala kubwa.

May 26, Ndio siku yenyewe, ilikuwa Sala kama Juma a pili. Watu walioshariki siku hiyo walikuwa watu 35.

Bwana Mr. Dale, alikuja pamoja na watoto wa Mkuzi kushinda, katika siku ile ya Kupaa.

Katika siku hiyo, tulienda kushinda Seluka, na huko kabla hatujakaa sana, mtoto mmoja aitwa Juta, alianguka, na kuchukuliwa na maji. Naswi tulimkimbilia, lakini tumempata salama, lakini ameumia chavu, na kidole cha tano cha mkono wa shoto. Tulishinda huko, hatta jioni tukarudi. Katika siku kuu hii tulicheza siku mbili.

Na siku hizi zikiwa ni siku za kushukuru kwa ajili ya mashamba kustawi, bassi, siku ya Juma a pili baada ya siku ya Kupaa, zilitolewa sadaka za malimbuko ya mashamba. Katika siku hiyo hiyo, ndio May 29. Palikuwa Ubatizo wa mtoto wa Klement Mnkabenga.

May 17. Palikuwa Examination kwa killa darasa, na walioshinda katika ya kwanza: 1 Gabriel Vikavu, 2 Francis Mzimba: ya pili, 1 Gharles Mfuko, 2 Rafael Nyungu: ya tatu, 1 Benyamin Kingodi, 2 Amani Mngodo: ya 4, 1 Nataniel Bungulu, 2 Yusufu Hiza: ya tano, 1 Mikael Mwamtalu na Salu, 2 Mikael Gao: ya sita, 1 Zinga, 2 Mnkondo: ya saba, 1 Sekiabi, 2 Mkacha. Tena siku hizi wagonjwa wengi hapa, Mr. Barrett alikuwa hawezi sana, tena na Mr. Allen, na Rev. Dale.

Panapo June 1, Mwalimu Connie Mgoma alikwenda Mkuzi kumsayidia Bwaria Dale, kwani mwalimu Archie Semmanyi alienda Misozwe kwa kuwa Babaye amekufa; bassi alienda kutengeneza maneno. Salaam. M. M.

MSIMULIZI. 576

## **LIKOMA.**

Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu. Baada ya salaamu nakuarifu habari hizi.

May 3. Ilikuwa harusi ya Austini T. Mabruki na Tabitha Potanjila mtoto wa chuoni. Siku ile ile alikuja Mkolesya yule yule aliyekuja siku ya Pasaka, kuja kucheza, kwani aliitwa aje acheze. Mwalimu Yohana yumo Chizumulu pamoja na Gr. Feruzi anamsayidia. Mwalimu Clement yupo hapa Likoma, kwani safari yake ya kuja huko i karibu. Bwana Archdn. Maples alikuwa hawezi macho sasa hajambo kidogo, pia na Bwana Johnson mguu wake uliteguka, pia hajambo. Balozi Johnston ametupelekea fetha za Kiingereza nazo zimeanza kutumika siku hizi.

May 23. Mtoto mmoja wa chuoni jina lake Edward Chiwanga ameingia katika kazi ya sormala. s.s. Charles Janson yaweza kufika Matope, kwani maji yamezidi kujaa. Safari hii ilichukua makasha mengi. School mpya yetu karibu itakwisha.

April 13. Mwalimu Reggie Songolo alifika hapa pamoja na mashua ile inayotumika chini, tena ilileta mizigo mingi.

April 13. Charlotte ilikwenda Chizumulu kumchukua mwalimu Clement na G. Feruzi.

April 14. Charlotte ilikwenda Kungoffi kumchukua mwalimu So Songolo. Siku ile ile s.s. Charles Janson ilifika hapa pamoja na Waalimu wote chini, illa John Padiela ndiye hakuja kwani mkewe alikuwa hawezi.

April 15. Panapo saa ya kwanza Wamasihiya tuliokuwapo hapa twalikwenda Kanisani, kwani

MSIMULIZI. 577

Wamasihiya wangine wa mijini hawakuja upesi. Panapo saa sita Wamasihiya wote wakafika tukaingia wote Kanisani.

April 16. Assubui tukaanza kutengeneza killa mahali. Saa 11 tukapamba kanisani. Jioni ilikuwa Sala kubwa na waimbaji wakavalia.

April 17. Saa ya kwanza kengele zikaanza kupigwa za kwenda kanisani kwa Sala yetu kuu ya Usharika Mt. Watu waliokuja kushariki Walikuwa watu 111. Panapo saa 5 ulikuwapo ubatizo nao walikuwa Watu 28. Siwezi kukuandikia wote kwani siwakumbuki majina yao illa nitakutajia watoto wa chuoni tu: Frederick Tawene mtoto wa Pachia, Francis Knule, James Philip Chikwelamawa, Walter Kanchambo, Mikael Ngwatu, Mattan Zikoma, Harriet Bweyeye na Mabee Kuundani.

April 18. Ilikuwa karamu kwa wale waliobatizwa.

April 19. Watoto 46 wa chuoni walikwenda Chizumulu kushinda kule, muda siku moja tukarejea hapa siku ya Juma a tano.

April 21. Miss Woodward na watoto wake, na watoto wanaume nussu walikwenda kushinda pa Utonga, siku ile ile wakarejea hapa.

April 22. Watoto 22 wa chuoni walikwenda pa Kongo kushinda.

April 18. Stima iliondoka hapa kwenda Msumba kusudi wakabatizwe watu, Msumba watu 13 waliobatizwa na Pachia watu 12, ikarudi hapa April 20.

April 18. Alikuwa mtu aliyetufurahisha jina lake Mkolesya alikuja na michezo yake, watu wengi sana walikuja kumtazama. Kwa kutufurahisha kwake alipewa zawadi yake.

June 20. Mwalimu So alipata mtoto mume jina lake Charles Martin. A. T. M.

MSIMULIZI. 578

## **CHITANGALI.**

Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salam, nakuarifu habari kidogo.

June 3. Kweli ni furaha kuona kama ilipita hapa safari kubwa sana ya Newala ya kuwatwaa mabibi Lindi, lakini sisi hapa ndio tukawa na aibu mno kwa sababu hapa hapana waliofuatana nao. Hawa watu wa Newala kama watu 60 kuwachukua mabibi pasipo mshahara mwendo wa siku nne.

June 12. Tukawaona nussu wanarudi wakatupa habari kama mabibi hawakuja kwani bibi mmoja hawezi sana: Bwana Haines tu ndio aliyekuja.

June 13. Bwana Haines akawasili hapa saa nne assubui, na saa saba siku ileile akaenda zake Newala.

June 14. Chuo chetu kipya kimekwisha, kizuri na kikubwa kupita cha zamani, na Bwana Cecil aliletewa £10 na bibi mmoja Mrs. Combe, bassi ametwaa nussu ametujengea chuo hiki, na nussu iliyobaki atanunua nguo za kanisani.

June 18. Tulienda Msokosela kutazama mchezo wa Kiyao ndio wa masewe, walipokwisha wale wachezaji wakapewa gora la mleso wakaenda zao.

June 20. Alikuja fisi kwa mzee Maluchila, akakamata mbuzi akaenda zake. June 21, alikuja tena fisi akatwaa mbuzi vilevile; na June 22, pia fisi akaja hapa petu akafungua nyumba ya kuku akakamata batamzinga wa Padre wetu, marra tukaamka tukatoka nje kumfukuza, akaenda kwa mzee Maluchila akakamata mbuzi akaenda zake. Bassi tangu June 23, hatta leo July 8, tumemtega kwa bunduki wala hajaja tena.

**MSIMULIZI. 570**

June 24. Kuzaliwa Yohana Mbat. ndiyo siku tulipofungua chuo chetu, saa kenda unusu ilikuwa Sala, tulipokwisha tukala chakula; na watoto wanaosoma wakala karamu yao.

July 3. Padre wetu na Mzee Barnaba Nakaam, walienda Mwitu pamoja na watu wengi Wamasihya na Waanafunzi, kukata mianzi ya kanisa letu, kwani July 25, tutaanza kulijenga. Leo July 7, wamerudi na mianzi mingi sana. H. S. M.

**NEWALA.**

Kwa Mtengenezaji Wa Msimulizi salamu, baada ya salaam najaribu kukuarifu habari za hapa.

April 15. Panapo Jumaa Kuu hatukuwahi kukaa sana Kanisani tukakaa saa 2 tu bassi, labuda wangine wenu mmepata kusikia kwa ajili gani kukaa saa 2, kwani Bwana Rev. Weigall akawa hawezi sana. Hatujaangalia haya tukasikia kama Bwana Carnon hawezi sana huko Masasi. Aliposikia rafiki yetu wa zamani Rev. S. Weigall akamwambia Bwana J. Hainsworth, mimi hapa nirathi nimwendee Bwana Carnon, akaenda. Alipofika huko yeye akaona Bwana Carnon ni mgonjwa sana akamleta hapa, wote wakakaa hapa.

Juma a mosi yake tukapamba kanisa letu kupita miaka yetu yote. Na siku ya Pasaka yenyewe watu wengi sana wakashariki, kwani hatta nusu ya watu wa Masasi walikuja hapa kwa kuwa Bwana wao akiwa hawezi hapa Newala.

April 22. Ijumaa saa 2. Unusu ya usiku mtoto wa Petro Mbika akafariki.

MSIMULIZI. 580

Panapo April 27. Bwana Weigall na Bwana Carnon wakaenda zao Unguja, kwani ugonjwa wa Bwana Carnon ulizidi sana sana. Mr. Weigall alikuwa hajambo, alipotuacha tulikuwa na huzuni sana hatta na watu waliomwona zamani siku moja, ndio washenzi wakaa karibu yetu. Kweli hatta tulipomwaga kumwangukia uso kama wataka kulia, kwani ni rafiki yetu wa zamani aliyetutendea kazi nyingi sana: alikwenda Ulaya kupumzika, bassi tulifurahi mno kumwona, lakini hakukaa kwani ugonjwa ukamshika sana, ikampasa kwenda zake marra moja.

Siku hizi Bwana Hainsworth kaondoka hapa kwenda Masasi kuwafanyia Chakula kile cha Roho kwa Juma a pili.

Panapo May 8. Tulianza kujenga chuo chetu kwani hiki cha zamani kilichakaa ati, ikatupasa kujenga kipya na kizuri sana. Na tena waalimu wakatengenezewa vyumba wawezapo kusoma pasipo uthia.

Panapo May 4. Wakarudi zao hapa chuoni walikoazimwa chuo cha waanake kutumia.

Panapo May 10. Ilikuwa harusi ya Rikardo, na Luka, ilisitawi kwa upande wake, kwani huku ni barra haihitaji vitu vingi.

Na nyumba hizi za mabibi ni nzuri sana, kiwanja chao pia kizuri na School yao pia nzuri.

Panapo May 17. Tulifurahi kumwona Mr. Hood na mwalimu Nicholas Kusi aendaye kukaa huko Masasi, lakini siku hizi anakaa hapa mpaka apatikane Padre wa kukaa huko Masasi. Pamoja naye akaja Cecil Majula. R. S.

MSIMULIZI. 581

**MBWENI.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi Salaam. Baada ya salaam nakuarifu habari hizi.

Panapo June 15. Tulikwenda Chukwani kutembea, siku nzima tukashinda huko, tukapewa siku kuu hii kwa sababu ya Siku kuu ya Barnaba Mt. Tumekwenda Chukwani marra nyingi lakini hatujaingia jumbani mwa Mfalme, marra hii tu tumepata kuingia na kuangalia anasa za ndani. Jumba hili ni jumba kubwa na zuri sana, ndani yake vyumba vidogo vingi vimo, na mabirika ya maji.

Bustanini mwake mawaridi na yasmini yanukia utamu.

Panapo June 24. Siku kuu ya Yohana Mbatizaji hatukutembea popote twalishinda papa hapa.

Panapo June 26. Watu watatu wameingia katika daraja la ualimu, majina yao ni haya, Lulu Masuke, Nina Madisa, na Charlotte Sanga.

Panapo June 29. Ilikuwa Siku kuu ya Petro Mt. Tukashinda papa hapa, watoto wangine walifanya michezo, wakafanyiana karamu, wakakaribisha wazungu wangine, na watoto wenzao.

Panapo June 30. Tumefurahi sana sana kumwona Mr. Key akitoka Ulaya.

Panapo July 1. Furaha sana kumwona Bwana Porter. Siku ile ile tukafurahi tena kumwona Padre Salfey akitoka Magila.

Panapo July 2. Siku kuu ya kusalimiwa Bikira Mt. Ilikuwa kusanyiko la Chama ya Watakatifu wote, watu 28 walipokea Usharika Mt. Watu sita wakaingia, Miss Burke, Helen Penyewe, Salome Machaku, Sarah Amani, Myra Sekehola, na Emily Mrashi.



**MSIMULIZI. 582**

Panapo July 5. Ilikuwa kusanyiko la waalimu kwa kusudi la kumwaga mwalimu Louisa Mnubi aendaye Masasi kwa kazi ya upelekwa, Usharika Mt, ukafanyika kwa kiswahili assubui na mapema. Watu wote wa Chama wakaenda kanisani.

Aliondoka hapa saa sita, watoto wote walio wakubwa walimsindikiza nusu ya njia, twalisikitika sana kumwambia kwa heri, lakini hapana mmoja awezaye kumzuia.

Panapo July 9. Ilikuwa kusanyiko la Chama ya waalimu wa Mbweni. Kwanza assubui ilikuwa Usharika Mt kwa Kiswahili katika kanisa dogo, wote wa Chama walishariki. Alasiri ikafanyika sala tena, na Miss Burke aliingizwa katika Chama hii; naswi twaona furaha mno kuona Chama chetu kinazidi. Watu wa Chama sasa 25, na katika hawa 9 wafanya kazi barra; Kasisi mmoja Bwana Woodward, na waanake 8 wanaofundisha katika vyuo vya wanaake, wawili Nyasa, watatu pande za Masasi, watatu pande za Magila. Mr. Key akatuhubiria, na tulipotoka kanisani tukaenda shambani kwa bibi Mwalimu; huko tukafanyiwa karamu, tena tukasikia maneno ya Bwana Clarke aliyotuletea katika barua.

Panapo July 11. Watoto wa Mbweni wamepewa siku nzima ya kucheza kwa kusafiri kwake mwalimu Louisa Mnubi. B. M.

**KIUNGANI.**

Katika siku kuu yetu ya Pentekote, tulijaa furaha sana. Kwanza siku iliyo mbele yako, ndio Juma a mosi: ilikuwa Sala kubwa jioni, wakabatizwa watoto watatu wa hapa, Thoma Aundi, Fabiano Songolo, na Albano Kibandera. Tena kwa wema wa Mzungu mmoja anayekaa Shangani aitwaye Mr. Boustead akatutaka tukashinde wote katika shamba lake Bububu, mwendo wa

MSIMULIZI. 583

saa mbili njia ya kuendea Mkokotoni; tukapate kufurahiwa kule. Safari yenyewe ingalikuwa Juma a tatu ya Pentekote, nasi wote tulikuwa tayari kwenda, wengine waingie ndani ya dau wale wasioweza kwenda, na wengine kwa miguu. Lakini tulipatwa na jambo la huzuni lililozuia safari yetu: kwani Mkunazini Bibi Miss Campbell mtunza wagonjwa alikuwa hawezi sana, tukaletewa habari ya kuwa ni shidda kupona, bassi safari yetu ikavunjika: na kama mlivyosikia yule Bibi hatta Jumaanne assubui akafariki.

Lakini yule Mzungu Mr. Boustead kwa wema wake vile vyakula alivyotuwekea tule Bububu akatupelekea hapa, mikate, sherbeti, machungwa, machenza, na maandazi: tulimshukuru huyu hatta tusipokwenda: kwani mali mengi aliyotoa kwa ajili yetu. Na sisi Juma yote ile tulijikalia papa hapa tuisome. Panapo June 10. Rev. Griffin akatoka hapa kwenda Magila, pamoja na ndugu yetu aliyepolekwa, mwalimu Alfred Juma: akapate kuoa na kufanya kazi yake.

Panapo June 28. Usiku huu wa Juma a nne kulalia siku kuu ya Petro Mtume, Muungu akapenda kumtwaa ndugu yetu Isaya Nangauje, mtu wa Masasi, hatta assubui Juma a tano saa tatu tukaenda kumzika. Aliugua homa kali kwa siku nne tu. Lakini Muungu amependa kumtwaa. - R. I. P. Huzuni gani aliyo nayo nduguye aliyekuwa naye hapa naye akiwa bado hawezi macho, kufikiri mama na babake waliokufa wakiwa papa hapa Kiungani, na huyu nduguye akitwaliwa. Lakini ni mapenzi ya Muungu, Na huyu mtoto amepolekwa kwao Masasi, illi labda apate hajambo kwa macho yake: na kupeleka habari hii ya nduguye.

MSIMULIZI. 584

Panapo June 30. Akawasili hapa Bwana Porter akitoka Ulaya aendaye pande za Newala. Tena tumejiwa na Schoolmaster mgeni, naye anakaa hapa sasa, aitwaye Bwana Gillanders.

### **VITENDAWILI.**

Naliletewa mwezi wa April vitendawili kuwategeeni, rafiki zangu; naye mtegaji aliahidi zawadi kubwa kwake afumbuaye vyote vinne, kumbe vitatu vimewatega wote. Cha kwanza, jibu lake Karara, (tazama Msimulizi wa April, uk. 547) cha pili, jibu lake Nyugi ya nyumbani, cha nne, Saa; cha tatu ndicho wachache walidiriki kufumbua, ni Mhindi. Bassi aliahidiwa R1 yule afumbuaye kwanza kitendawili kimoja.

Bassi katika wale waliofumbua wengine wanakaa Bonde, mmoja Mvita, lakini wote wa Unguja na Wayao pia wameshindwa wasilete hatta jibu moja lililo sawa, wengi walibahatisha vyao tu pasipo kuwa na njia wakijibu, Msimulizi, ao 'Kiungani' ao 'maua' ao 'buyu' ao 'mwili' ao 'tumbo' ao 'mayiti' ao 'nyoka'!

Lakini aliyejibu upesi baada ya kuvisoma vitendawili ndio Rafael Nyungu, mtoto wa Magila, bassi amechukua ile R1. Kwani akajibu Mhindi.

MSIMULIZI. 585

**MISOZWE.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam.

April 3. Walipokezwa watu misalaba waanawake wazee watatu na watoto waanawake wa chuoni wawili, na wengine wasio wa chuoni wawili, na mtoto mwanamume wa chuoni mmoja, na mtu mzima mume mmoja, jumla yao 9. Usiku uliofuata akaja fisi usiku akala kuku kumi na moja.

April akaja Bwana Askofu, Mr. Allen, na Yusuf Kombo, tukafurahiwa sana kumwona Baba wetu Askofu. Siku ya Pasaka twalikuwa wote kwa moyo mmoja Padre Woodward akiwapo nasi.

April 27. Nalikwenda mwituni mwa mlima Mlinga kukata miti, na pamoja nami watu 4, Ambrosio Umali, Lupati Jupa na Kipingu. Hatta kwa saa ya nane tukasikia sauti kali mwituni mle, tukasemana sisi kwa sisi sharti tuende tuone ni nini? ni mtu, ni kitu, pia tuone: nasi wote hapana mwenyi selaha, tuna mashoka tu na miundu, tukafuata kule sauti itokako kwenyi mwitu, nako pote miiba mingi. Baadaye kidogo mwendo wa nussu ya saa tukaona mbwa, tukajua kama ni wawinda: bassi yule mbwa tukamfukuza vikali, na wale wawinda wawili walipotusikia walithani labda nguruwe amekamatwa: kwani ni wawinda nguruwe, wakaambiana kama nyama amekama

588 MSIMULIZI.

watoka kwa mbio wamejifunga selaha zao waenda angalia habari gani, wangine wakaja kuuliza kwetu, kama ni sisi tuliopiga bunduki, tukakana si sisi. Kumbe watu waliokuwa upande mngine wa mji wanasikia mashime yakilia akikatwa mtu ndipo wakafuata upande ule, wakiendelea wamwona mtu amelala, yu nusra ya kufa tena. Ilikuwa usiku wasijue nani waliompiga huyu, wakajaribu kutafuta huku na huku wasione mtu. Na yule wakamwacha pale pale, wangine wakaja kwangu kuazima taa wakamwangelie vema, bin Adam huwa mmoja jamaa ao kabila yao; ikatukia sivyo, akaja mtu wa pwani mmoja akasema naye kadri ajuavyo, kwani wamezoea kwenda Umasaini kwa uchumi wao wa pembe, akawaeleza ginsi alikotoka, nao waliompiga na wakaapo pia.

Jambo la pili tutamfanyaje bassi na sisi hapa Kizungu Wazigua wakishamwacha vile? Haenda mjini Korogwe hakusanya watu na wazee wao pia kuwauliza mashauri, ya kumtenda yule mtu haifai kumwacha pale naye ni mzima bado, na tena ni karibu na njiani. Ah! ni jambo kwao kabisa lilikuwa kumlipia mema aliye adui yetu zamani wakikamata ng'ombe zetu na kutwaa burre, sikuweza kupata neno la kanuni kwao. Ah! ni kwema kujua huruma nini? Wote tu damu moja na tu mfano wa Muungu wetu. Tena kujua kisasi ni chake Bwana yeye atalipa; Nathani ikanipasa kuwatazamisha sana, na jumbe wao akakubali, illa hakuweza kuwafanyia nguvu watu wake, nikawaambia sharti tukamchukue yule mtu tumtafutie nyumba tumweke tutamtunza sisi wa Kizungu hapa kwa chakula, hatta afe mwenyewe tumzike, bassi. Wangine wakaja tusayidia tukatwaa kitanda tukaenda kuchukua, hawezi kugeuka huku wala huku mikono

MSIMULIZI. 589

yake imekatika imesalia ngozi kidogo tu ya kuzuia isikatike yote. Tukiwa katika kumchukua pale mahali tulipotoka kumpeleka akakae mle mjini, akatokea mmoja mzee wa humo mjini, akasema mwalimu huyo mtu mwamchukua mtamweka wapi? ati, mle mjini mwetu; nikasema, Ndio; akasema Sitaki, atatunzwa na nani, mtu ni adui yetu; naye amejeruhiwa hivyo hatutaki na mji wetu, tukajadiliana sana na watu wale watusayidiao pia wananisayidia kusema na mtu huyu, kwa mwisho kaona mtu huyu moyo mbali mbali na tufanyavyo. Hamwambia kama kwa ukali, ukitaka usitake tutampeleka, si nyumbani mwako ni nyumba isiyo na mtu, hutamtunza wewe ni sisi wenyewe, ukitaka wacha mji nenda zako kakae kwingine ukiona jambo hili la kuchukizisha. Alipoona maneno yangu yana nguvu mno na ya hasira kwa ugumu wake asisimame marra akaenda zake. Illa tukaona afathali tusimchukize mtu, tukaenda mtafutia Mmasai huyu karibu na mji, penyi msitu uliozunguka mji, tukamfanyizia ndani ya msitu mahali, tukakoka moto pale tukamweka. Kwa bahati akatokea mzee mmoja jumbe wa mji mmoja mdogo wa mwaleni naye aitwa Selubwaza, alipotokea aona tuwafanyizia mahali mtu yule, akauliza kwani mkamweka hapo msituni, aliwe na nyama burre, tukasema wenyi mji wamekataa tufanyeje. Akaamuru kuitwa yule aliyekataa asiingizwe mji mtu huyu aliyejeruhiwa. Akasema naye sana kwa maneno yaonyayo kama ana nguvu juu yao, akamkaripia kwa kutoa kujua kwake mtu huyu. Mwisho asiwe na nguvu tena ya kukataa, ndipo hawaamuru watu tukamchukua hatta nyumba ya mtu mmoja aitwa Maiwe aliye chini ya jumbe Senjoya wa mji Korogwe, ndiye aliyekuwa upande wangu kabisa mtu huyu, na kunisayidia katika yote.

MSIMULIZI. 590

Ni Mmasai, na ule uadui walio nao kati yao, imezidi kuwafanya mioyo migumu juu yake; nami haenda waambia wenzangu usiku ule tukaangalie, tusiweze fanya neno tukarejea tukalala. Hatta assubui tukaenda mwangalia tena, na watu wa killa mji waenda kumwangalia. Kumbe vile yu mzima bado, illa hivyo alivyokatwa Ah! havitazamiki vyatisha mno, mikono yote miwili imekatwa katika vikonyo na mifupa imetokea, na upande mmoja wa uso hauonekani na jicho pia, amekatwakatwa na mguuni, wamemwacha kufa tu tena. Tukitazama watu wa inchi hawana shauri lo lote, illa ah, wasema, watu hawa waliotuulia mtu katika inchi nani? Wakijulikana walipe ng'ombe kwa kusafisha damu katika inchi yetu. Illa mashauri ya kusema kama jee mtu huyu tumfanyeje? Naye ni mzima bado akiachwa nje pale tena ataliwa na nyama.

Wao tu walipojua ni Mmasai walitaka, mmaliza wamtupe mtoni Luvu. Bassi sasa sisi imesalia mashauri tufanyeje? Tukatwaa nguo tukaenda kumfunika kwani hana illa kitambaa kidogo tu. Kwanza watu wakija mwangalia amenyamaza kimya kama amekwisha kufa kwa hofu nathani akithani watammaliza akipumzika kikogo kidogo tu, alipoona amefunikwa nguo naona alijua Ah! si watu kuniua hawa baada amefanywa vile. Bassi akaanza kusema tena "ngale ngale" ndio maana yake "maji maji" kwa Kimasai. Wangine kwa huruma wakaenda twaa togwa la ugali wakamnyweshwa, akaendelea kupata moyo hatta asema tena, illa watu wasikia, wangine neno moja moja tu.

Bassi tukamlaza ndani watoto wetu wa hapa wakafanya kama walivyoweza kwa utoto wao kusayidia kutafuta kuni na kumkokea moto. Bassi mimi nimeshangaa neno moja sana nilipokwisha yote haya; Jee majeraha Ah! ni yasiyofungika, tena dawa ya vidonda

MSIMULIZI. 591

hapana imekwisha yote. Sikuwa na la kufanya illa kumpelekea chakula uji zayidi, na togwa watu waliokuwa na huruma kwa kadri yao humpelekea. Tukalala juma ya atatu haandika barua Magila juu ya habari hii, na kumwita daktari kama aweza kuja kumtazama na labda kujaribu kufanya dawa kwa majeraha yake. Ikatukia mtu akakaa mzima siku sita kwa ajabu akawa hali hiyo mtu huyu kwa ginsi alivyojeruhiwa na hivyo akakaa siku hizo ilikuwa ajabu sana, na daktari alikuwa ameshikwa na shughuli nyingine nyingine za wagonjwa asiweze kuja upesi huku, ilikuwa kuja na Padre Woodward pamoja kwa kututazama kwa wakati mchache.

July 5. Alhamisi athuuri, wakatokea Padre na Dr. Henriques watoto wakaenda kuwalaki kwa furaha sana. Hatta jioni daktari akitaka kwenda mtazama alivyojeruhiwa, asiweze kwa kuchoka sana, bassi haenda mimi na mwenzangu kumpelekea chakula, tukifika kumtazama vile alivyolala ni vile vile tukamtikisa haamki, Oh, kumbe amekwisha kufa, amepumzika maskini katika maumivu yale machungu na makali mno. Bassi tukarudi mjini na chakula chetu, tukawaeleza kama yule mtu amekufa. Daktari aliona huzuni sana sababu alitaka kujaribu kumfanya kama alivyoweza, kwani akaja na vitu vyake tayari na dawa dawa na vya kukatia na kumshonea na kumfunga majeraha yake. Tukalala hatta asubuhi, tukitaka kwenda kumtazama aone hivyo alivyokatwa katwa tukafika hatta tangu Korogwe, tukaambiwa Oh, kaisha tupwa mtoni na wenyi nyumba. Ikawa hatuna la kutenda tena, tukarudi mjini.

Tena tukafanya mashauri kama mkimwona mtu aliye yote atokaye huko barra ana mtumwa ao wa Kimasai wamzuie asiende, sababu huko wanawadanganya



MSIMULIZI. 592

twendeni kwenyi chakula nao hufuata wamegonda hawana nguvu wakifika njiani, kama wamechoka hawezi kwenda amua hivi haifai. Hivi tukapatana, illi Ah mapatano ya mdomo tu yao, sababu juzi tumepata kuingia mjini Korogwe tukaambiwa kama mna mtu ana mwanamke wa Kimasai, tukawauliza majumbe kwani ahadi yetu jee mbona hamkushika na Padre Woodward na Padre Chambers pia wapo, bassi Padre akasema haina buddi yapasa mumtoe mtu huyu na Mmasai wake sasa hivi, ao habari hizi zikipatikana na Wadachi kama mwakaribisha wanaochukua watu kwenda uza mtaathibiwa; huku na huku maneno, mwisho wakaingiwa na hofu kama Ah, tutaathibiwa tusiposikia tunavyoambiwa wakaenda kumtoa mjini usiku ule.

July 7. Daktari Henriques amerudi Magila na mimi na mke wangu pia, tukaenda kukaa kwa siku chache, na mimi nimerudi yeye nimemwacha huko kwa wakati mchache. Bwana mkubwa Yohannes na Baron Von St. Paul, safari kubwa sana ya askari Wanubi na Wadachi 14, imepita siku hizi kwenda Kilimanjaro vitani, wanapigana na Mandara.

July 11. Jambo letu la furaha Korogwe tumepata Baba wa roho sasa kasisi mgeni atakayekaa nasi hapa akiwa na afya njema kama tutumainivyo, jina lake Padre Chambers. Sasa Mission tuna watoto 16 wakao nasi. Padre Woodward kesho aenda zake Magila baada ya kukaa nasi karibu na mwezi, sasa tutakaa na kasisi wetu mgeni.

May 28. Watu wa mji Korogwe wamelima njia toka Tanga Korogwe mpaka huku kwetu juu penyi ulalo wa kwenda Kizungu, burre pasipo kulipwa, kwa kupatana nao na kuwafaa wao wenyewe wajapo kwetu, na sisi kwao, nathani yapasa sifa, na jina

**MSIMULIZI. 593**

la Korogwe kusifiwa kwa kadri yao.

Tena watu wanadumu kuja kanisani Juma a pili, na bado tumepata kengele moja kubwa inasikiwa mbali, na wengine waja siku ya Juma a tano kufundishwa peke yao, wahitajio kujua zayidi mambo ya dini ya Muungu.

Mwaka huu watu wa inchi hii walichelewa kulima mtama kilicho chakula chao kikubwa wamelima, mihindi zayidi, na sasa ni wakati wa mavuno, watu waleta chakula mjini. Desturi Waluvu hawalimi vuli kama Wabondei, illa mwaka huu watalima sababu wamechachiwa sana, na njaa kidogo imeingia katika inchi hii.

Tena watu wanauthika na uthia wa hawa askari Wanubi, peke yao pasipo Mdachi dayima wapitapo inchi hizi hunyang'anya vyakula, kuku, pengine kuwakamata watu wachukue mizigo burre pasipo kuwalipa upagazi wao, thulumu tupu. H. N.

**MKUNAZINI.**

Kwa mtengenezaji wa Msimulizi saalamu, na baada ya saalamu nakuarifu habari za hapa tukaapo chache tu.

Panapo August 10. Tulifurahi sana kumwona mtoto wa hapa petu alifanya harusi, watoto wa hapa walienda kwa harusi, jina lake Joseph L. Hapiuwa, naye alitoka Magila.

Tena tulifurahi kumwona ndugu bibi yetu alituacha kwa miezi chache tu, ndiye Miss Shaw, sasa anakaa hapa anafanya kazi yake kwa wagonjwa pamoja na

**MSIMULIZI. 594**

Bwana Daktari, sababu Bwana Daktari ana kazi nyingi siku hizi. Kweli miezi hii miwili July na August, tumepata ugonjwa ulio mbaya sana ndio ugonjwa wa ndui, watoto wengine wameugua, lakini wamepona salama isipokuwa ndugu yetu mmoja A. Kiwisi amefariki kwa ugonjwa huu. - R. I. P.

Sasa tunafurahi sana kuona hospital yetu, sasa inakaribia kwisha, kwani nzuri sana, kwa kukaribisha wageni walio wagonjwa.

Panapo Aug. 27, Bwana A. C. Madan alitukarimia kwa ginsi hii, alituita twende Kiungani saa ya kwanza unusu usiku kutazama mwezi, nao ulikuwa mzuri sana, kwa ile darubini yake nathani wengine wamefahamu kuona; na tukakarimiwa kwa chakula kizuri, kuisha, saa tatu tukarudi hapa.

Siku kuu yetu ya Bartolomayo tulifurahi sana, tukaenda Kiungani kwa furaha kwa kushangilia, na bibi Dean-Pitt akawakarimia watoto wa hapa walio Choir killa mtoto rupia moja. H. M.

**LIKOMA.**

Kwa mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu, safari hii sina mengi ya kukuarifu, kwa sababu mtumishi wetu s.s. Charles Janson killa siku anakawia pande za chini. Kwani ndiye anayetupasha habari za huko.

Bassi panapo May 29. Watu 10 walifanywa wanafunzi, ndio hawa, Wyarigulu, Malisawa, Malizani, Weyapa, Maloya, Kaojele, Kalupo, Makawawa, Chupongula, Chatipati.

MSIMULIZI. 595

Panapo June 1. s.s. Charles Janson ilimchukua Bwana Archdeacon Maples kwenda Chizumulo, na panapo saa tatu aliwatazamia kusoma watoto. Alipokwisha akarejea hapa.

Siku kuu ya Pentekote Bwana Archdeacon hakuweza kufanya Usharika Mt. kwani alikuwa hawezi. Na watu waliotaka kuja kupokea Usharika Mt. walikuja kupokea Siku kuu ya Utatu, na sadaka za fetha pia zilikusanyika siku ile.

Panapo June 15. Ilifika hapa s.s. Domira ikitoka pande za Bandawe pamoja nao bibi Maclaughlin na bwana Atlay aliye Shemasi, naye anakaa hapa Likoma. Siku ile ikawa furaha tupu wala hatukuingia chuoni tena kwa kuwafurahia wageni wetu.

Siku ileile June 15. Watu wanne wa ng'ambo walitoka jioni kuja humu Likoma kwiba. Walipokwisha fika watu wawili wakatoka na pembe zao za madawa, wawili wakasalia ndani ya bwato, mwenyi madawa Ngapulika, zile pembe mbili akampa mwenzake Makwinja, akasimama nazo mwangoni, yeye mwenyewe Ngapulika akaingia ndani akaiba majembe.

Jembe likalia, marra mwenyi nyumba akasikia akathani paka, akatwaa majani akayawasha moto. Akamwona mwivi kasimama na majembe yake mkononi ataka kumpiga mwenyi nyumba, aitwa Amnyanje; akamwendea akamshika akamwangusha chini, akafanya nguvu akakimbia. Amnyanje akapiga kelele kwa kuwaita wenzake, marra wenzake wakatokea, wakawakimbiza wale wevi, Ngapulika alikamatwa, mwenyi kushika pembe alipigwa bunduki hatuna hakika kama atapona, Ngapulika alifungwa kongwa kwa siku kathawakatha. Na wale wangine waliosalia ndani ya bwato

**MSIMULIZI. 596**

waliposikia kelele tu, hao wakaenda zao usiku kwa usiku ng'ambo. Mtu mwingine jina lake Kunguni amekwiba nguo za Kanisa la Chizumulu, lakini alizirudisha tena usiku kwa usiku.

Bassi tulipoletewa habari hizo, Bwana Archdeacon alimpeleka Charles Nasibu kwa mfalme Chitesi kumwarifu habari hizi. Baada ya siku si nyingi tukamwona mfalme mwenyewe Chitesi amekuja humu Likoma kwa shughuli hiyohiyo, ametuma watu kwenda Chizumulu kuuliza, twangojea majibu ya wajumbe.

Tukatazamia wajumbe waliotumwa hawakuja, hatta akaondoka mwenyewe Chitesi kwenda Chizumulu, lakini mtu mwenyewe aliyekwiba amekimbilia Nkamanga. A. T. M.

**KIUNGANI.**

Panapo July 14. Ilianza kufanyika Examination ya darasa nne, kutazamiwa akili, mabwana wa hapa hapa ndio walioshika kazi hii, siku kama tatu. Na walioshinda katika darasa ya kwanza ndio hawa: 1. Samuel Chiponde, 2. Benedict, Madalito, 3. William J. Swedi. Ya pili: 1. Yakobo Kachanda, 2. C. Janson. Mkumbukwa, 3. Herbert J. Sehiza. Ya tatu: 1. Francis Sapuli, 2; Gabriel Katoma, 3. Barnaba Mtaala. Ya nne: 1. Chad Hamisi, 2. Bernardo Mkaki, 3. Bartolomayo Marmhei. Na siku zile zile Yakobo Kachanda akatiwa katika darasa la Ualimu.

Panapo July 25, Siku kuu ya Yakobo Mtume, ilikuwa mashindano ya mpila, kati ya H. M. S. Racoon na watoto wa hapa, ndio Luke Chivoko, Hugh Mhina, Benedict Madalito, Danieli. Usufa, Klementi Mkajanguya, Petro Musa, Julius Mkwaya, Hayley

MSIMULIZI. 597

Makusudi, Yohana Sonjo, William Mpagweje, na Yusufu Kasembe. Lakini wa manowarini walishindwa kabisa, walipata mawili kwa manne tu, bassi Wazungu hawa waliingiwa na haya sana, kushindwa na watoto weusi.

Panapo August 2, wakasafiri ndugu zetu watoto wa Kiyao kwenda kuangalia jamaa zao, pamoja na Bwana King, aendaye kubadili hewa kwa siku chache tu. Bassi katika siku hizi hapakuwa mpigaji kinanda tukisali, bassi watoto wetu wawili walikuwa walitupigia, karibu killa siku, ndio Charles J. Mkumbukwa, na Hayley Makusudi, ilipendeza sana, twatumaini wataendelea zayidi.

Panapo August 8, akawasili hapa ndugu yangu Wilfred Sezua kuangalia harusi yangu.

Panapo August 10, Ikawa harusi yangu Mbweni, watoto wa Kiungani wangine walikuja kuangalia. Sasa nakaa Mbweni pamoja na ndugu yangu Geldarti Senkoba.

Panapo August 24, Siku kuu ya Bartolomayo. Kwanza siku iliyo mbele yake tulipamba nyumba yetu na kutengeneza njia. Bassi siku yenyewe hii ilikuwa siku ya furaha sana. Assubui walikuja kushinda hapa, watoto wa Mkunazini na wa Mbweni kufurahi pamoja. Hatta saa kumi walikuja baharia wa H. M. S. Racoon, wakaupiga mdundo wa filimbi na ngoma yao hatta jioni, na Wazungu wengi waliokuja siku hii, hatta walicheza Tennis hatta kama saa za jioni, wageni wakarudi kwao.

Siku ya pili yake, Alhamisi, watoto walienda Mwera, hatta jioni wakawasili tena hapa: assubui ya pili tena Jumaa wakaingia chuoni, kuongeza elimu.

Panapo August 29, akawasili hapa Bwana King

MSIMULIZI. 600

**NEWALA.**

Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Baada ya salaam, naona hujapata habari zetu kwa siku nyingi, na sasa hatuwezi kuandika habari zote tangu mwanzo, lakini tutajaribu kuandika kidogo tunayoyakumbuka.

Aug. wakatujia ndugu zetu watokao Unguja pamoja na Mr. King, tukafurahi sana kuwaona, tukacheza nusu siku. Lakini Bwana Hainsworth hawakumkuta alikwenda Rovuma kuwinda. Na marra aliporudi huko Rovuma hakukaa sana marra akafunga safari ya kwenda Ulaya Ingreza. Bassi akatoka pamoja na Bwana King na Cecil Majula walipokienda Unguja.

Na Newala siku hizi anakaa Bwana Hood, na Masasi anakaa Mr. Porter, na Mr. Haines. Tukafurahi sana siku ya Bartolomayo, mwalimu Daudi na mwalimu L. Pesa siku ile ile pamoja na watoto wapata 13 wakaenda Rovuma pamoja na watoto waliotoka Unguja. Na watoto wengine wakaenda Masasi, wote wakupewa siku 10 kucheza. Lakini waliokwenda Rovuma hawakukaa sana wakarudi upesi kwani chakula chao kikeshwa, walipiga wanyama watatu tu.

Tunafurahi sana siku hizi kwa sababu tumeanza kutumia kitabu cha Mathbahu kwa Kiyao, kilichofasiriwa na Baba Cecil. Siku hizi Rikado anakaa akifundisha Makonga, kule kwa Mripa ametoka. Na mwalimu Harry atakaa kwa Chisanga. Na Yona anafundisha kwa Mauyamba. Watoto wetu wawili Benito na Andrea wamekwenda Lindi kufanya kazi kwa Dachi.

Sasa ndugu zetu wengine, ndio Samwil na Siluano wanakwenda Unguja, na wengine watakwenda

**MSIMULIZI. 601**

mwezi wa October. Lakini tunasikitika sana kwani katika safari hiyo wa Chitangali wamerudi kwa kuwa hawakuwa na barua ya kunena wanashuka Unguja. Bassi Mdachi alikataa kuwatolea nauli, tunatumaini watashuka mwezi wa October.

Lakini Kolumba hakushuka safari hii pamoja na Samwil kwa sababu amefiwa na babaye, alikuwa hawezi kwa siku nyingi, panapo Sept. 11, akafariki, lakini alibatizwa siku ya Juma amosi jioni.

Sept. 10, Na assubuhi Juma a pili ndipo akafariki, alasiri kama saa a tissa tukaenda kumzika chini walikolala ndugu zetu wengine. S. C.

**MASASI.**

Mtengenezaji wa Msimulizi salaam sana. Nataka kuwaambieni habari za hapa petu. Mwajua kama siku nyingi tulikuwa hatuna Kasisi.

Katika mwezi wa August twalifikwa hapa na Padre W. C. Porter na Mr. Haines aliye Shemasi, na mwalimu Nicholas Kusi.

Na habari za Siku kuu ya Bartolomayo ilikuwa furaha sana. Assubuhi saa kwanza ulifanyika Usharika Mt. na tena zilitolewa sadaka kwa kushukuria mavuno. Baada ya Usharika palikuwa Sala tena ya assubuhi.

Tulipotoka Kanisani palikuwa na mashindano, kwa watoto, na kwa watu wazima. Na baada ya mashindano tukala chakula, walichinjwa mbuzi wawili. Hatukwenda mbali kushinda lakini watoto wa Newala na Chitangali walikuja kwetu kutembea kama nussu juma, kiisha wakienda zao.



**MSIMULIZI. 604**

Miss Burke, na Mr Key, wakashinda huko siku nzima jioni wakarejea nyumbani.

Sept. 23, Ee, ndugu zetu wa mbali na karibu, hamna buddi kuona Msimulizi wetu wa safari hii mna habari nyingi zilizo nzuri, na nyingi mbaya, siwezi kunena wala kuwaelezea hasa ginsi yetu ya siku hizi. Ndugu zangu siku hizi sisi twataabika sana mno kwa mwivi, kwanza niliona si vizuri kunena habari hii katika Msimulizi huu, tumevumilia sana hatta tumechoka kwani tangu kuja huyu mwivi zayidi ya marra tatu.

Akija atwaa vitu vingi sana vya thamani, juzi akaja akatwa ngazi akapanda akaingia hatta ndani akatwaa alichopenda, kiisha akaacha ngazi ile nyuma ya nyumba, tena akaacha kisu chake na chuma.

Sept. 23. Amekuja tena leo hatujui ginsi alivyoingia hatta ndani, kwani milango pia imefungwa, safari hii ametuteka sana sana, ikiwa hatujui alipoingilia, alipotokea twapajua. Kiisha twaa vitu vingi mno akaja kwa njia ya Class room akatwaa vitu vya thamani sana, hatta taa ile inayopanda na kushuka kaikata mkufu akaenda nayo akiisha kavunja kufuli vipande vipande akaenda zake. Tulipoamka assubuhi killa mmoja kajaa na shangao kuona vitu vimetawanyika, na milango ya Class room imekuwa wazi. Ndugu zetu ikiwa anaingia hatta ndani kwa uerevu mwingi mwisho wa mtu huyu hatujui. Ndugu zetu hali yetu ya siku hizi ya taabu.

Sept. 24, Tumeletewa habari kama mtu yule anayetuuthiuthi amepatikana, naye amekamatwa na vijana wawili wanaake wa Mbweni, hatujapata habari zake vema bado, tukipata tutaelezea katika Msimulizi ujao. Si furaha hiyo kusikia amepatikana, si zayidi kumwona kwa macho yetu. Kitu kimoja alichotwaa kimerudishwa leo, ndiyo kofia kubwa ya kiume. B. M.

**MAGILA.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu, mtuwie rathi sana kwa kuwa hatukuweza kuleta habari miezi iliyopita. Na sababu yenyewe mtasoma mwisho.

June 8. Watoto wa hapa walio Wamasihiya pamoja na Padre Woodward walienda Misozwe kuzindua kanisa. Na huko Bwana Chambers aliugua sana. Akarudishwa hapa.

June 10. Andrew Yakuti alipata mtoto mwanamke. Mwezi huo huo Mr. Allen na Mr. Brockway waliugua sana.

Hatta June 24, siku ya Yohana Mbatizaji, walipelekwa Unguja, wakifuatana na Padre Salfey, katika siku hiyo hiyo, Joseph Hapiuwa alishuka kwenda Unguja, marra, katika siku hiyo hiyo alipita mzungu mmoja wa Msasa pamoja na wapagazi wake. Habari zake mzungu huyu ajabu, kwani katika kwenda kwake, alichoka; bassi akawaamuru watu wake, wamfungue makamba kote kote pasipo huruma. Bassi naswi, ah! alitustaajabisha sana. Na hii ndio desturi yake achokapo.

Katika June 19, tulianza kurudia kanisa letu la kwanza; kwani lilikuwa likitengenezwa; naswi tukawa tukitumia sala zetu katika nyumba ya kusomea.

MSIMULIZI. 606

July 1. Mwalimu Ackworth aliwaasili toka Unguja.

July 5. Ilikuwa harusi ya mwalimu Alfred Juma; kati yake na Josephine Mwamkuna. Tukafurahi sana.

July 3. Ilikuwa ubatizo wa mtoto wake Andrew Yakuti.

July 8. Padre Salfey akawasili toka Unguja.

July 11. Ilikuwa maziko kwa mtoto wa Ackworth Baruti aliyeugua kidogo akafa. - R. I. P.

July 14. Ilikuwa harusi ya Meta. Kati yake na Borra. Naye ni "Mhindi" aliyetoka kwao kwanza alikuwa mwanafunzi, lakini alipata kubatizwa baada ya kuoia kwake. Mume aitwa "Paratapsing."

Aug. 1, Watoto wote wa hapa walipewa ruhusa kwenda kwao kwa Juma tatu.

Karibu na mwisho wa Aug. Mwalimu Connie Mgoma alipata kuwa hawezi sana sana homa kali sana ghafula ilimshika kwa juma tatu unussu. Hapana awaye yote aliyemwekea tumaini la kupona. Kwani homa hiyo ilikuwa kali, hatta kusema hasemi, wala kuona, wala kula, wala fahamu yo yote hakuwa nayo. Hatta siku moja alikaribia mwisho; kwani alizimia.

Lakini kumbe amejaliwa kupona, na kuwa mzima tena, kurudia kazi yake. Twamshukuru Muungu.

Sep. 21, Alipelekwa Mkuzi kupata kubadili hewa. Tena Mwalimu wetu wa zamani Mr. Roberts tulifurahi kumwona alipotuwasilia katika October 13 pamoja na Bibi mmoja ajuaye kazi ya dawa. Pamoja nao tena tulifurahi kumwona Mwalimu Peter Limo kuwasili tena huku. Tena alifika Mwalimu Denys alikuja kutembea. Na tena siku hizi, nyuma ya nyumba ya kengele, kumejengwa nyumba ya wagonjwa. Nzuri sana, lakini haijaisha bado.

**MSIMULIZI. 607**

Tena Mwalimu Manfred Manyula. Amewasili tena petu. Kwani aliugua siku nyingi, akaenda kuuguzwa kwenyi Mwalimu Granville, kwa Mkului.

Sasa Padre Chamber akaa Korogwe na John L. Mwaimu. Na Oct. 26, Padre Griffin ameenda Mkuzi kukaa mahali pa Padre Dale kwani apelekwa Ulaya kupunga hewa.

**MKUZI.**

Sept. 23, Amefika hapa Bwana mkubwa wa Tanga Baron Von St. Paul na wenziwe watatu kutengeneza inchi; na kutia liwali mwingine mahali pa Mwinyi Kambi, ndio Chamkwinde.

Na Sept. 25, Katufikia Mr. Henriques kutoka Unguja kumpeleka Mr. Brockway, kwani alikuwa hawezi huko Magila.

Oct. 2, Tulikuwa na furaha sana, kwani watoto wetu watatu wamepewa misalaba, ndio Mwekaahangwa, Ngaja, na Abdallah.

Oct, 9. Tumefurahiwa sana kumwona mwalimu Willie J. Swedi kutoka Unguja.

Oct. 12, Tumefurahiwa tena kuwaona mwalimu Peter Limo, aliyekwenda Ulaya siku nyingi sana; tena mwalimu Denys Sayite, Mr Boberts, na bibi Daktari.

Oct. 26, Ametufikia Mr Griffin, kwani atakaa hapa, na bwana Padre Dale ameenda Ulaya kupumzika, na twatumaini ataturudia.

Oct. 28, Ndio siku kuu ya Siman na Yuda; wamebatizwa watoto wetu wawili, ndio John D. Sayidi na Marko Changale. Tena tumepata furaha ya watoto wetu wawili wa kike wanne wamepewa misalaba;

**MSIMULIZI. 608**

ndio, hawa, Mgaya, na Lukindo, na Mamkaa, Mawaboei, Mtagwa, na Mashaia.

Tena Nov. 3, Padre Dale na mwalimu Willie Swedi wanaondoka hapa kwenda Unguja; na kama nilivyosema, Mr. Dale anaenda Ulaya, na Mr. Griffin ndie atakayetuangalia. Leo sina habari nyingi. Salaam. A. A. S.

**MISOZWE.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi Salaama allahu. Wabadahu ya salaam, nakuarifia habari zetu chache na thaifu pia.

August 8. Walikuja Makasisi wawili hapa Padre Woodward, na Padre Griffin, kwa mambo ya serkali hii.

August 9. Ilikuwa arusi ya mmasihiya mmoja ndiye Daudi Mhina, na mkewe Maryamu Nekiyango.

August 11. Tulikwenda Gonja kuona hali ya mwalimu Cyprian Lizani. Na tuliokwenda ndio Padre Griffin, na mimi, na Yohana Mgonea, na mpishi Bichard Funge, na mwandishi Fabiano Kandolo, na Kijana mmoja Mmasihiya, nami Peter Mwande.

August 12. Tulikwenda Mlenge, Mlenge ndio mji bondeni mwa mlima wa Mlinga ndipo asomeshapo Yohana Mattayo Mgonea, tulienda kwa kuwatia moyo, wajenge chuo kwa watoto wao kusomeshea, tuliokwenda ni Padre Griffin, na mimi, na Yohana, na Daudi Wakati; tukafika saa tatu tukawangoja watu wote kukutanika hatta kwa saa ya sita wote wakawapo ndipo Padre

MSIMULIZI. 609

akitoa maneno nami mtafasiri wake, illa siku ile ya 12 hawakuja tukaenda tena siku ya 15, ndio wazee 30 waliokuja.

August 28. Watu wanakwenda kwa Mlinga kutoa sadaka mvua inye na kubadili mchezo wa inchi nzima siku ile ile, kasisi wetu alikuwapo hapa alikuwa hawezi hakuweza kufanya sala zote za Usharika Mt.

August 30. Tukampeleka Magila hawezi sana, tukatoka Misozwe saa 11 tukafika Magila usiku saa nne.

Sep 4. Tumepata vuno zuri la inchi, watoto wa kike wanane wa kibondei wamejitoa kwao kukaa nami, kwa shida sana wameshinda wazee wao.

Kwanza wazazi wao wa kike hawataki wanasema, Ah watoto wakienda Kizungu, ndio kwa Station, labda watapelekwa Unguja, tusipojua ao kwenda Ulaya, wazungu wamemtuma yule Mwalimu kutuhadaa tu atwae binti zetu.

Bassi wazee wao wakasema ah, hatutaki mwende huko mkienda huko jueni mmetoka katika kuwa binti zetu tena, maana yake ndio kuwavunja moyo wao, lakini siyo, watoto wale watatu walikuwa Wamasihya na wanne ni mwaanafunzi billa mmoja hajawa, illa hatta hivyo naye akawa na moyo mkuu, hatta siku hii wakafanya shauri majira ya jioni wakaacha mji wao kuja kwetu. Assubui wakawatafuta watoto loo hawapo, wa wapi kumbe wasikia wapo Kizungu, ah! wengine wakajilaani kama hawatawakubali tena kuwa waana wao. Wakatwaa miti wakavunja ndio ishara mtoto hatakubaliwa tena kwao, illa watoto wasiangalie hatta moja lao, baada ya siku mbili nikawapeleka kwao nione kama ndio kweli watawakataa, ama sivyo wakawaondoa mjini kwa haraka, hivyo ikawa

MSIMULIZI. 610

juma mbili, na kidogo kidogo kwa upendo na amani watoto wakienda, na kurudi tena kwa siku tatu, ao nne, wale wazee ndio wakaona kama ndio kweli, wakatulia, sasa nia yao yafurahiwa wakiona binti zao walivyo, na tena kwa mambo mengine wawasayidia wazazi wao.

Sept. 5, Nalienda Gonja kwa kutazamia watoto wa mwalimu Cyprian Lizani, nalienda na watoto wawili Daudi Wakati na Mkumbo.

Sept. 14, Nalienda Magila kwa siku ya kanisa la Magila nikarudi siku ile ile.

Oct. 13, Watu wa upande wa inchi uitwao Mpyambile, na upande uitwao kwa Mkindu, na upande uitwao kwa Mwaimba, wote wamekutana watoe mapesa wampe mtu anayethaniwa nao kuwa mganga wa kuita mvua, kwani siku hizi tangu August hatta mwezi huu wa November ni jua tu nalo kali.

Oct. 17, Watu wa upande wetu ndio uitwao Luale wamekutana nao penyi gulio kwa jambo lile lile.

Oct. 18, Nalikuwa nimekaa jioni saa ya pili ya usiku naona wazee wawili wanakaa Hemkole, mji wa chini ya mlima wetu, na majina yao ni Kiluke na Sekumkati wakifika wasema mwalimu tumekuja, na neno liliotuleta ni hili kwanza twakupa swali, tutoe kodi ao tusitoe? nikawaambia kwaje? Nielezeni habari zote nijue, mmoja wao Sekumkati akasema "Wakati wa alasiri kama saa ya kumi, nalikuwa nagama marra naona mtu anayetoka Kangaiya akaniambia kusema mjini kwenu killa mtu hatta mtoto mdogo atatoa pesa moja, ukawaambie na watu wa Misozwe na wa Mugaza," bassi niliporudi hatoa habari kwa wote nao wameisha shauri lao,

MSIMULIZI. 611

wanena hii kodi twaijua sababu, illa enendeni kwa Mwalimu tusikie atasemaje naye, sababu ndio kutoa mapesa yote kumpa mganga anayethaniwa aweza kuita mvua, ndio habari.

Nami hawajibu hivi: Mwamjua ni nani atoaye mvua na vyote pia? wakasema wote wawili atoayo vyote ni Mulungu, wakaenda zao wakafanya shauri wasitoe pesa wote, katika miji mitatu, Henikore, Misozwe, Mugaza. Siku ile ile ya kumi na nane ya mwezi, ingalikuwa Ubatizo illa Kasisi alikuwa mgonjwa huko

Oct. 20, Nasikia kelele upande wa kwa Mwaimba, siku ya pili hasikia habari kama hii, mganga wa mvua amekimbia na mali yote pasipo kunyesha mvua.

Oct. 23, Akaja padre Griffin tayari kwa juma a pili na ubatizo pia, hatta assubui akaanza vema sala za Usharika, marra akiwa tayari kufanya Wakf, marra akaniita kumshika mkono kumtoa nje hamtoa tukamaliza sala kwa Litania. Saa ya nne akajitia nguvu akawabatiza watu wanane waume waliooa watatu na majina yao ni haya George Alfred Tupa, James Matthew Lupatu, Luka Bartolomayo Mbalazi, na watoto watatu wa School yetu ni hawa, Sisera Trajano Tengu, Paolo Tito Mhina, Daniel Kilua, ha watoto wawili wa kike wa nyumba yetu, ndio hawa Mary Grace Trukano, Fhith Hope Mtekwa, baada ya ubatizo akatoka, mimi nikamaliza sala zote, jioni watoto watatu walipewa misalaba nao ni wa nyumba yetu wawili wa kiume Mkumbo, na Masimba, na wa kike moja, Chonge. November 4, ndio siku ya kupatwa mwezi, leo habari nyingi washenzi wanenazo siwezi kutoa zote. Salaam. M. F.



MSIMULIZI. 612

**NANYANGA (KWA LIUMANGA.)**

Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu nyingi. Baada yake, nitajaribu kama niwezavyo kukueleza habari za hapa. Sisi ni watoto wa Mission ya Newala tukaao hapa. Tunajaribu kuwaambia wenzetu wakaao katika nguvu za giza habari ya Anjili. Naona marra kwa marra nimeamriwa kukuletea habari kwa mkono wangu, lakini umechelewa mkono wangu kukupelekea. Habari zetu njema sana na za kondeni pia. Na hapa tukaapo tumejenga Mission yetu katikati ya mji huu wa Mihuru. Nao wapenda kutukaribisha sana. Lakini ni wenyi nia ngumu kwa mafundisho yetu, kwani wengi waislimu bassi waona shaka sana kwa ajili Waislamu. Tumepata hapa wasikiaji kama arobatashara tu. Na watoto wengi wajao kusoma. September 30, ilikuja tufano kubwa sana, hatta ikaja juu ya nyumba yetu ikatoa manyasi yote, ikawa wazi. Bassi sasa tunajaribu kuiezeka tena.

Panapo July 16. Nalifunga safari kwenda Newala tayari kwa Siri Takatifu. Illa njiani nikamwona baba W. C. Porter. Akanirudisha hapa kuwa mgeni wangu. Tena kunisaidia kazi yote. Tukawa na furaha sana kumwona tena, kwani Bwana amependa kumrudisha tena katika inchi yetu ya bara. Bassi tukawa watu wa kuongea na kutusumulia habari za njiani alimopita, na Juma a pili akatuambia kama akipita njiani aliona bahari ile ya Sham na milima ile ile alipotoa Muungu maneno ya amri kumi na Torati. Panapo July 19, akaenda zake wahadi Masasi kwani ndipo akaapo sasa, kumshikia bwana wa pale kwani hapana Padre, bwana Carnon alikuwa mgonjwa akaenda zake Ulaya. Tena tumeletewa na

MSIMULIZI. 613

watu wa Ulaya kengele sasa imetundikwa juu.

Sept. 29, Ndio siku ya Mikael na Malaika zote, bassi nalienda Rovuma kuwinda pamoja na watu wa hapa, tukashinda siku moja. Hatukupiga cho chote illa kanga tu. Nalimpiga ndogolo risasi ikamvunja mkono wala hakufa. Tena bwana wa hapa aitwa Liumanga ukimwangalia ni hakimu kweli kweli. Na sasa amekwenda kuwinda kulekule Rovuma. Baada ya kwenda kuwinda alikutana na mzee nyati, akampiga bunduki ikamvunja mkono, wakamfuata hatta wakamkuta mnamo vichaka. Bassi hapo ilikuwa kishindo kama bin Adamu kwa bin Adamu washindanavyo. Hatta akaenda mzee mwenyewe akamnyemelea akapigwa risasi ya kitwa, palepale wala hakutoka, bassi ni furaha kwa Wamakonde leo. Na mzee amewasili leo bassi si kuranda walikorandaranda Wamakonde mjini pote watu wamejaa kuomba nyama. Lakini habari za humu angalieni, nyama ni moja na watu ni wengi, nyama haiwezi kuwachukua watu wote, lakini killa mmoja huthani apate kitoweo anga akatolee siku moja. Ndizo habari. Salaam. B. M.

NEWALA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi Salaamu. Baada ya salaam uwe rathi kwani marra nyingi twachelewa kuleta habari zetu.

Sept 25. Mfalme Matola alitoka hapa kwenda kunako mto Rovuma, kuwinda viboko, akapiga viboko watatu. Naona utapenda kusikia kama siku hizi tumefanya shauri la kusayidia wajaani, na wagonjwa, kuwapa killa mwezi R2 kwa killa mmoja, (wajaani hawa

MSIMULIZI. 614

na wagonjwa ndio walio Waanafunzi, Wamasihiya).

Oct. 3, Wamasihiya wote na waanafunzi walikusanyika kuezeka kanisa letu. Kwani ni desturi ikiwa karibu mvua kutia majani mengine.

Oct. 4, Tukapata habari kama Mr. Williams yuko Masasi akitoka Nyasa.

Oct. 7, Akawasili hapa pamoja na mwalimu Clement Kathibeni. Tukafurahi mno kuwaona, na kusikia habari za ndugu zetu wakaao kule Nyasa.

Oct. 11, Wakatoka hapa wakienda Unguja. Nalifuatana nao mpaka Mlolela.

Oct. 14, Nikashika njia kuja zangu hapa. Njiani nikakutana na safari yetu ya hapa ikienda Lindi. Lakini nalistaajabu kwa sababu sikuwaona watoto wa Kiungani waliobaki safari ya mwalimu Samwil. Ila mmoja tu, naye ni Yusuf Kasembe nikaona huzuni sana Siku ya Kupriano Mt. mtoto mmoja jina lake Chihinde, alikuwa hawezi sana hatta alithaniwa atakufa. Bassi siku ya pili Padre Hood alimbatiza akaitwa Kupriano. Lakini sasa hajambo.

Nov. 1, Watakatifu wote. Tukafurahi sana padre wetu alitupa mbuzi tukamchinja. Na siku ya pili yake ndio siku ya Roho zote, Bassi sisi wote tulitoka asubui mapema, kwa taratibu, na kuimba nyimbo, Tukashuka chini inakostarehe miili ya ndugu zetu Ukafanywa Usharika Mt. tulipokwisha tukarudi zetu hapa.

Oct. 31, Watu wa hapa waliokwenda Makwangwarani wamefika hapa, wametupa habari kama wamefanyiwa heshima sana kwa ajili ya urafiki wao na mfalme Matola. Tena wametuingia kama kuna Wamakua waliotoka ng'ambo ya pili ya Rovuma, bassi walikwenda kuwaita Makwangwara wakawapigania kwa adui zao, walipofika kule waliuliza

## MSIMULIZI 615

habari? Wakasema tumekuja kukuiteni mkatupiganie. Lakini Makwangwara walikataa, hatta walipozidi kuwaita Makwangwara wakakasirika nao. Hatta kidogo wangepigwa. Bassi Wamakua wale wamerudi kwa aibu na kuchekwa tu.

Oct. 29, Habari za furaha, ndio mwalimu Leonard Pesa amepata mtoto mke. Nov 6. Amebatizwa akaitwa Rose Anjilina.

Tena Oct. 16, alibatizwa mtoto wa Danieli Mandowa, na Oct 9, alibatizwa mtoto wa Luke Mtopenyasa Nov 4, tumeona mwezi umepatwa na kivuli cha dunia. Nov. 6, safari yetu ya Lindi imerudi na barua za Unguja. Lakini ilichelewa sana kwani siku hizi Wadachi wanafanya uthia wa kufungua mizigo yote, na kupima killa kitu kilichomo hatta kwa uthia huu vitu vingi vimepotea havikufika. Pamoja na safari hii Andrea Kapanda aliyekuwa akifanya kazi kwa Dachii amerudi, waliobaki watarudi mwezi wa pili.

Nov 8. Mtoto mgine aliye mgonjwa amebatizwa ni mtoto wa kike, naye ni binti Mfalme, jina lake ni Maryamu Achuluiche. Kweli hawezi sana tumaini letu ni kwa Muungu tu.

Mwalimu K. Y. Mzigala anashuka safari hii kwenda Kiungani. D. M.

## **KIUNGANI.**

Panapo Sept. 30, Walituwasilia hapa wageni watokao Ulaya Ingreza, pamoja na mwalimu Peter Limo aliyetoka hapa zamani kwenda Ulaya Ingreza kusoma. Na katika wageni hawa mmoja wao ni schoolmaster, jinale Mr. Chambers, nduguye yule padre akaaye Korogwe.

MSIMULIZI. 616

Mwalimu Peter Limo hakukaa sana, marra akasafiri kwenda pande za kwake Magila, na pamoja naye mwalimu Denys aliyekwenda kutembea kule muda wa mwezi na sasa karejea tena, akaja pamoja na padre Dale anayekwenda kwake kupumzika kidogo, tena pamoja nao akaja na mwalimu Willie pia aliyekwenda kutazama jamaa huko.

Oct. 23, Wakatuwasilia wageni tena, wengine watoka bara ya Nyasa, ndio mwalimu Clement Kathbeni na Bwana J. Williams. Na wengine watoka barra ya Uyao, ndio watoto waliokwenda kutazama jamaa huko bara kwa muda kidogo.

Tena siku hizi wametoka watoto wanne hapa wa Nyasa, waliokaa hapa karibu miaka miwili, illa mmoja wao, amekwenda kwa kuwa yu mgonjwa macho. Lakini walipata hatari walipokienda, kwani "mail" yao iliingia funguni lakini hawakukaa sana wakatoka.

Kwenyi siku kuu ya Siman na Yuda, waalimu wote wa hapa tuliitwa kwenyi shamba la Mr. Boustead, laitwa Bububu. Na huko kuna kazi, nyingi, lakini kazi zote hutendeka kwa mitambo. Na kazi zenyewe ni kufanyiza kamba na mafuta. Bassi nazi, zimejaa tele huko lakini wao katika nazi hizo zote hapana wanachoharibu; kwani sisi tukipata nazi hula tui lake tu bassi, makumbi, na kifuu, machicha, hutupa lakini wao, wakiisha fua zile nazi, makumbi huloweka majini tayari kufanyiza kamba, mbata hukausha tayari kwa mafuta, vifuu hufanyiza makaa, ya kuendeshea mitambo illa maji ndio yanayomwagwa, kwa kuwa wana maji fathili, kwani mto unaingia ndani, lakini kama hawangekuwa na maji ya mto labuda wangetumia maji haya ya nazi kulowekea makumbi. Na mbata zile wakiisha fanya mafuta machicha hupeleka

MSIMULIZI. 617

Ulaya kuwa chakula chema kwa ng'ombe.

Na watoto watatu wa hapa wanafanya kazi huko huja hapa killa Juma a mosi jioni tayari kwa Jumaa pili.

Tulifurahi siku kuu ya Watakatifu wote. Sadaka zikakusanywa za kusayidia kujenga nyumba ya wagonjwa weusi Magila. Tena Bwana Kick pamoja na watoto wa kazi wakaenda kisiwa Bawe kushinda huko. Na kwenyi mshuko wa alasiri watoto wangine wakaenda Sebuleni kuvua makambale, kwani Sebuleni ni ziwa kwenyi njia ya kwenda Mwera kama mayili mbili tangu hapa, wakapata jumla makambale 32.

Nov. 13, Mwalimu Yohana B. Abdallah kasafiri pande sa Usambara kutazama dunia ya huko; na pamoja naye amekwenda Luke Chivoko na James Mpila walio wagonjwa wa macho, wamepelekwa huko kubadili hewa muda wa mwezi labuda watapata kuwa heri.

Tumefurahi sana kusikia kama amepatikana Askofu wa Nyasa, kwani ni jambo tulilokitazamia sana siku hizi. Jina lake Wilfrid Bird Hornby, kasisi wa Sunderland mji wa kasikasini wa Ingreza, tena zamani akawa mpelekwa wa Oxford Universities' Mission katika Kalkatta.

Nov. siku ya sabatashara ilikuwa arusi Mbweni, kati ya mwalimu Hugh Mhina na Agnes Naluwamba. Nao walikuja kukaa hapa kwa muda kidogo tu, walikaa hapa kama siku tano, wakashika safari kwenda pande za Usambara. Kwani aliambiwa akiisha oa tu arejea Usambara kufanya shughuli yake ya kufundisha.

Nov. 19, Mwalimu Kolumba alikuwa mgeni wetu hapa, akitoka barra Newala. Kwani nalinena katika Msimulizi uliopita kama alikuwa na uthuru ndio maana hakurejea upesi. Mtg.

MSIMULIZI. 618

**MBWENI.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi Salaamu. Baada ya salaamu nakuarifu habari hizi haba.

October. 17. Tulifanyiwa Examination, waliotufanyia ndio Rev Key na Bwana Matthews.

Examination hii tumetazamiwa kwa mda siku nne.

October. 20. Tumepata nusu siku kupumzika kwa Examination hii.

October. 18. Ikawa siku kuu ya Luka Mwanjilisti Usharika Mt. ulitolewa katika kanisa la shamba, jioni saa kenda unusu watoto wote wakaenda cheza shamba la bibi Mwalimu wakafanyiwa karamu huko.

October. 28. Siku kuu ya Siman na Yuda Mitume, Usharika Mt. ukatolewa katika Kanisa la shamba.

Nov. 1, Watakatifu wote, watu 41 walipokea Usharika. Mt. Jioni ikawa kusanyiko la Chama ya Watakatifu wote, Archdeacon P. L. Jones-Bateman aliwahubiria.

Nov. 4, Watoto wote walicheza tu siku nzima.

Siku ile ile ilikuwa kusanyiko la chama cha Mchungaji aliye mwema. Kiisha mahubiri uliimbwa uimbo wa kuaga.

Nov. 7, Bibi Mwalimu amesafiri kwenda Ulaya na pamoja naye akimchukua Mwalimu Keziah Shika Lako. Wapita njia ya Napoli, watakaa Rumi hatta siku za baridi zipite ndipo waende Ulaya. B. M.

**MKUNAZINI.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Baada ya salaam nitajaribu kukuarifu habari kidogo tu, za tangu Sept. hatta leo hivi. Sikia bassi.

Sept. 8, Ilikuwa siku ya furaha kwa Sultani

MSIMULIZI 619

wa hapa Unguja, sababu ni hii, Malkia wa Uingreza amepata habari kana Sultani wa Unguja apenda kutembea huko na huko kwa mashua, bassi Malkia Viktoria kaleta mashua ya mti wa Ulaya, mbavuni thahabu, sukanini thahabu, domoni thahabu, mibao ya kukalia mti wa Ulaya uitwao "Oak," na mito ya kukalia humo mashuani hariri swafi na zari mbavuni; tena ina kibanda chake sukanini madini tupu. Wallakini, bwana na uzuri wote huo ni ya makasiya: ukiona yapendeza kuwa ya moto wallakini sio makasia sitashara huku nane, huku nane, yang'aa hapo ilipo. Bassi iliposhushwa kuja bandani pake Sultani, wache mizinga ilie, kwanza Glasgow akaichemsha, pili manuari ya Mgereza akaichemsha, na mdundo papo. Walioileta bandarini ni baharia wa Manuari ya Kiingreza, wajua makasia tangu utoto, ndio habari.

Panapo Sept. 18, Ndugu yetu Harold A. Chechande kapata mtoto mwanamume. Sasa kabatizwa jina lake John.

Sept. 26, Nimepata habari kama C. W. Rehani ang'oa safari ya Uganda pamoja na Askofu Tucker.

Tena panapo Sept. 29, Harusi huko Mbweni za watoto wetu wa hapa Mkunazini, Baranabas Farajalla na Nutter Kawazi.

Sept. 30, Meli ya Ulaya imefika imetuletea ndugu zetu Peter Limo, Mr. Roberts, na wageni watatu, ndio Miss Whitbiead, na Miss Brewerton, watakao kuwa wauguzao wagonjwa wa 'Hospital' hii mpya ijengwayo, na Mr. Chambers mwalimu wa Kiungani. Panapo Oct. 7, Kafika hapa Mr. William Williams aliyekuwa kwanza katika Upelekwa wetu kule Likoma katika C. Janson, illa sasa kapata kazi ya



MSIMULIZI 620

kwenda kusayidia Serkali kwa kuunga pamoja merikebu tatu za huko Nyasa. Bassi kapita nazo hapa katika marikebu ingine kubwa sana.

Panapo Oct. 8, Bibi Whitbread kaenda Magila pamoja na Peter Limo na wengine, kusayidia kidogo mpaka Hospital iishe kabisa ndipo atarejea kwa kazi yake hapa, kwani walikuja wawili, bassi mmoja yupo hapa, na huyo wa pili kaenda huko Magila kwa kitambo tu.

Oct. 21, Tulipata habari za ghafula, ndio Merikebu hiyo iliyomchukua Mr. William Williams imezama, lakini sio. Kweli panapo October 23, tumepata habari zingine ndio haikuzama illa iliingia funguni tu, maji yalipojaa ikatoka ikaenda zake Chinde. Siku hiyohiyo. Oct. 23, Meli ya kusini ikafika, ikileta mwalimu Clement Kathbeni na bwana J. Williams wakitoka Nyasa, na watoto wengine wakitoka Newala, wote hao waenda Kiungani.

Oct. 27, Watu wawili wa hapa Mkunazini wamepewa misalaba, mume, na mke.

Panapo Nov. 1, Ilikuwa siku kuu kubwa ya Watakatifu wote, Bassi Mkunazini ilitawanyika, wengine Mwera, wengine Chapwani, wengine Kiungani kushinda huko, wengine Mashamba kushinda pia, jioni ndio ilikuwa mkutano.

Panapo Nov 8. Pamefika Mzungu mmoja jina lake D. Johnson, katokea pande za pili za Afrika peke yake na wapagazi tu, kaenda kwa miezi themintashara, kafika pande za Chinde na kamkuta Mr W. Williams na shughuli yake papo. Naye huyu mzungu aenda zake Ulaya Ingreza halafu huyo kwake Ulaya Amerika.

Hizi ndizo zilizopo, zingine ndio "Hospital" yetu karibu kukaliwa, kwani yatiwa chokaa nyeupe sasa. W. E. K.

MSIMULIZI. 621

**MKUNAZINI.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Baada ya Saalam utapenda nikuarifu habari zetu za pande hizi za mjini tangu Nov. hatta leo hivi; bassi sikia. Huko Ulaya Ingreza kumekuja simu, ya kusema Balyozi wa hapa Unguja aende pande za Uganda akatengeneze mambo ya huko, kwani yamefanya kuchafuka kwa ugomvi na vita wao kwa wao. Bassi ilikuwa safari kubwa sana, kwani sikia, mzungu mmoja alikabithiwa na balyozi watu miateen wa sabwini kutangulia nao hatta Mombasa, nyuma yake akafuata Kapteni Arthur pamoja na askari miateen. Na baadaye kidogo mwenyewe balyozi pamoja na watu mia moja wa hamsini; wote hao watakutana kuko mbele kuwa jeshi moja. Habari zingine ndio siku hizi tumepata mtunza hazina mzuri sana na hodari kwa kazi yake, kwani atoka kule kule Oxford, jina lake Mr F. Davonport wakashuka pamoja naye, Miss Bennett wa Mbweni, na Mr H. Lister wa Korogwe,

MSIMULIZI. 622

wallakini kwa leo hivi atakaa hapa kwa shughuli ya kuangalia watoto wa kazi, mpaka ajapo Askofu.

Panapo Nov. 30, Rev. J. Swedi ametuwasilia pamoja na mkewe, kwani mkewe ni mgonjwa. Bassi wamekaribishwa pande za Mbweni.

Panapo Dec. 3, Andrew Yakuti ametuwasilia akitoka Magila, lakini sio na mkewe.

Dec. 8, Mwalim Ackworth Machaku katuwasilia pia. Lakini hakukaa sana marra akarejea, yee na Andrew Yakuti pia. Habari zingine kana mjuavyo ndio panapo Dec. 21, Askofu mpya jina lake W. Hornby amewekwa wakf huko Ulaya akikusudia kwenda Nyasa, bassi siku hiyo watoto wote wa Kiungani walikuja hapa kufanya sala kubwa juu ya jambo hilo, na kumwombea apate kuipokea kwa moyo wa imani.

Bwana akatujalia tukafika hatta panapo Dec. 25, Ndio siku ya kuzaliwa Bwana wetu. Watu wakafurahi sana. Na tena ilikuwa furaha kubwa kwa masihiya wa kweli kuwaona wamasihiya wengine waliokuwa kama wamejitoa katika kanisa, lakini siku hiyo wakaja kwa sala zote, hatta kukaribia meza ya Bwana pia. Bassi hii si furaha kumwona kondoo aliyepotea yupo tena pamoja na wenziwe?

Panapo Dec. 26, Watoto wote wa kazi wa Mkunazini, illa walio wagonjwa walienda Dunga pamoja na bwana Daktari, na Mr. H. Lister, Mr. Faulkner, Tukashinda huko kwa siku moja ya pili yake tukarudi mjini petu. Tulifurahi sana huko.

Panapo Jan, 2. 1893, Bibi yetu Mills alifanya machezo mazuri sana ya watoto, kama vile "Evano" ao "Watoto mwituni," ya miaka iliopita. Lakini huu ni mdogo lakini ulikuwa mzuri, kwani palikuwapo mbwa wa mwitu, (Red Riding Hood) Kondoo, (Little Bo peep)

MSIMULIZI. 623

na watoto kiatuni (The old woman who lived, in the shoe) &c. Bassi yote hii walifanyiza kwa kuiga, ukawa mchezo mzuri, watu wengi walikuwapo kwa kuutazama, kwani walialikwa.

Panapo Jan. 3, Examination ya hapa ilianza alasiri saa nane kwa watoto wa bibi Mills tu. Aliyetazamia ni bibi Berkeley wa Mbweni ikaendelea hatta Alhamisi asubui ikamalizika.

Panapo Jan. 6, Andrew Yakuti katuwasilia akileta mkewe pamoja naye kwani kazi yao imekwisha kule. Panapo siku hiyo hiyo jioni yake Rev. J. Swedi akasafiri akienda kwake Mkuzi, kwani nalisema alimleta mkewe, bassi amemwacha Mbweni kwa kuuguzwa, ao kwa kupata afya na labda baadaye atarejea naye. Usiku wake wa siku hiyo, palikuwa mchezo, na kuimba, kwa watoto wa kazi wa hapa na baadaye wakapata chai kwa wema wa Mr. H. Lister.

Jan. 7, "Marks" za Exmination zilinenwa na bwana Daktari. Aliyetokea wa 1. katika Darasa ya kwanza ni Yustino Dodo wa 2 James Kathibeni wa 3 Yakobo Matozwe. Katika Darasa ya pili John Dunford Mlangwa na Kornelio Chonge hawa chanjali wa 2 wao akawa Rufo Changua. Katika Darasa ya tatu, wa 1 Obed Farijalla wa 2 Sila Jabu. Katika Darasa ya nne wa 1 Rorbert Ali wa 2 Stefano Taji, hivi ndivyo ilivyokwenenda.

Jan. 9, Bibi Mills, ameona chuo chetu imeharibika sana ukuta, kwa kubomoka chokaa na tena sakafu ya chini imefanya ufa sana, bassi ikawa haina buddi ijengwe. Bassi tumechukua vitu vyetu vya Chuoni kama ilivyo kwa mtu wa Chuoni, tumekuja Mbweni katika shamba la bibi Thackeray tunafanya kazi yetu hapo ya Chuoni, tutakaa mpaka Chuo chetu kisha kutengenezwa ndipo turejee tena. Watoto wanafurahi

**MSIMULIZI. 624**

sana sana kwa kubadili hewa hivi, juu yote ni wakati wa embe sana, bassi zinaona kazi yake.

Panapo Jan. 14, tumefurahi kumwona Daktari Ley akitoka Kepu. Alipofika Kilemeni akakutana na bibi MacLaughlin aliye mgonjwa akitoka pande za Nyasa kaja hapa kujaribia hewa akiona hajambo atarudia kazi yake vile vile. Na bibi Turner aendaye Ulaya Ingreza akipita njia ya Kepi naye atoka Nyasa.

Panapo Jan. 17 bwana Daktari, na Miss Shaw, na Dakatari Ley, wafunga safari ya Magila, Daktari Hine kwa kutembea tu, lakini bibi Shaw na Daktari Ley kukaa.

Za mwisho. Hospital yetu twangoja kuzinduliwa, kwani imekwisha.

Tena jambo jingine ndio killa Juma a pili panashuka waana maji wa Kiingreza kwa sala hapa Mkunazini huja na mdundo wao toka pwani hatta mwangoni. Ndipo hunyamazishwa, huingia Kanisani kwa sala, Ee bwana mdundo mzuri sana; na ni furaha kwetu kwani Kanisa letu huingiliwa marra sita panapo siku ya Juma apili ukikosa sala hii utaikuta hii. W. E. K.

**KOROGWE.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu, baada ya salaamu, naanza kukusumulia habari tulizonazo huku kwetu. Habari ya kwanza ni hii, nyumba ya Mwalimu Henry ilikuwa katika kujengwa sasa, yamalizika twatumaini kama mwezi huu wa Oct. itafunguliwa, na mwenyewe ataingia karibu kukaa humo, nyumba kubwa na ya nafasi kwa ginsi ilivyosimamiwa na mwenyewe kujengwa vizuri na imara sana. Watoto

MSIMULIZI. 625

wote hapa walipewa ruksa ya kwenda kwao kwa muda wa juma atatu, kama siku 20, kwenda amkia wazee na jamaa zao kwa siku kuu ya wakati wa mavuno.

Padre, na mwalimu Henry, na Alfred Konko, na Martin Kiyango, na watoto wetu wanne na wapagazi wetu watatu, tukasafiri juu milimani inchi ya Usambara, upande wa inchi hiyo waitwa Vugiri kwa jumbe mmoja wa Kikilindi aitwaye Ngoma, Msambara, habari yake mliyoona katika Msimulizi wa 24. Ndio milima ya kupanda, utaona mlima umesimama sawasawa mithili ya mti ulioinama kidogo tu.

Jumbe huyu akatupokea kwa furaha sana, kwa bunduki &c: tulipoingia tukataka mahali pa kujenga hema letu marra jumbe akaamuru watu na majembe yao wakalime mahali penyi kivuli wakachimba vema tukasimika hema letu, baadaye kidogo twaona twaletewa kondoo mwenyi mafuta; tukampokea kwa heshima na shukurani nyingi sana. Tukamchinja na vyakula vimepikwa tayari vikaja kutoka killa nyumba tukala, na wakaamrisha watoto wakaenda boondeni mtoni kukata miwa, ikaja mingi. Ikawa jioni watoto wote wakapewa nyumba yao ya kulala vitanda vya asili, (mabanti) ndio maganda ya mti yaliobanduliwa kama mbao. Na chakula cha huko zayidi ni ndizi, na ugali kathalika wafanywa katika ndizi, na nyumba zao zaezekwa na migomba, ndio wajuao kutumia hawa, kula na kufanya makao kwa ndizi, tangu juu hatta chini, na nyumba ni za miviringo, namna ya nyumba za Waluvu kwa upande.

Bassi Padre na mimi tukulala hemani, hiyo baridi bassi ah, haisemeki. Siku ya pili tukaita watu si wa mji ule tu lakini hatta miji mingine wakaja, tukaanza kuwahubiria mambo ya Mulungu ndio jambo

MSIMULIZI. 626

zayidi tuliloendea huko, sikujifurahisha siku kuu tu. Tukatembea sana siku ile, kuna mji huko umejengwa juu ya gamba la mlima wa mawe mji huo nyumba zake kama zaanguka haiyamkini kukimbia kimbia huko, ao kukimbiza kuku ao kitu, usipozoea utaanguka uvingirike hatta chini, na ndio mwisho wa maisha ya mtu, illa wenyewe wamezoea wanacheza huko na kufukuza watoto na kufukuza kuku &c.

Hatukuthubutu kumwacha Padre apande huko, kwani alipenda sana kwenda juu huko kutazama mji, na kutwaa urefu wa mlima na kujua pande zote, kwani zaonekana killa pahali ukiwa juu ya mlima huo, hatta Korogwe pia yaonekana na miji ya huku. Watoto walijaribu kwenda huko illa tuliogopa viatu vyake Padre kuteleza maweni, na mji waitwa (Kashihwi), na jumbe ndimo alimokuwa akikaa zamani, umejengwa mji huu kwa adui wasiweze kuingia wajapo kupigana. Nao kwa kweli ni ngome na mji wa hatari kwenda kupigana nao humo kwa hivyo ulivyo. Jioni yake watu wakaja wengi tena zayidi kusikiliza senturi ikilia wenyewe wakija wasema twataka pango bassi lafunguliwa; kwa hivi twavuta wengi sana wakahubiriwa tena, na kuwaambia watoe watoto wao wawalete kufundishwa kusoma na mambo ya Muungu wametuahadia kama baadaye watafanya shauri wawaache watoto waje kwetu kufundishwa, na Padre akampa Jumbe zawadi iliopasa ujumbe wake, kwani tangu kuingia mjini humo hatukutumia pesa letu moja kwa kununua vyakula wakatulisha mpaka kutoka kwetu humo. Tukulala usiku ule wa pili, assubui yake tukafunganya tukarudi kwetu. Kushuka milimani rahisi kuliko kupanda hakutuchokesha sana kama tulipokwenda. Tukawasili hapa kama saa tano za

MSIMULIZI. 627

assubui. Hii ndio habari ya safari yetu, tumejifurahisha kama tulivyoweza, tukarudi kwa furaha ya bunduki ikilia. Ah! ndugu zetu ushehzi na ukafiri si jambo jema; bassi huku Waluvu ni washenzi kamili kwa tabia zao walizonazo. Kwa jambo dogo walifanya jambo kuu ginsi wanavyoua watoto wachanga. Juzi juzi hapa mji wa Korogwe mtu mmoja aliamuru mwanawe akauawe na watani, mtoto mwenyewe amri wa miezi mitatu kamili, akachukuliwa akanyongwa, na mamaye kwa uchungu wa mwanwe akajitosa mtoni Luvu kutaka jiua, afe naye, lakini wakamdiriki kumwopoa majini, analia kwa uchungu mkali mno.

Baadaye tukawaeleza habari hii, ikatupasa kwenda mjini, Padre na mimi kuwakemea sana juu ya jambo hili, na kuwaambia ginsi habari ya Muungu na laana kuu lilivyo juu yao. Kwa kutoa roho ya kiumbe burre tu, ikatupasa kuwaambia kama kwa ukali sana, na kuwaogofya, kama wakiendelea kutenda uaji huu kama walivyozoea na tukijua tutawaarifu Wadachi waathibiwe kwa jambo kuu hili, twajua wamezoea, lakini yapasa kujaribu kufisha desturi hizi na kuziacha kabisa, tumejaribu kuwaonyesha kama ni ukafiri mkuu sana kufanya hivi. Kwa jambo kama hili la kuu watoto huwezi kuona mji mkubwa kama Korogwe watoto wachanga wengi ilivyopasa kuwa umati wa watu na watoto.

Oct 5. Jumbe Ngoma Msambara wa Vugri amekuja kutuamkia, kaja na watu wake kenda naye wa kumi. Kafanyiwa heshima kama tulivyoweza, akakaa hapa siku mbili ya tatu akaenda zake kwao na zawadi ya kumfaa ndio heshima yake, tukikumbuka alivyotukarimia kwake.



MSIMULIZI. 628

Wazigua marra kwa marra huja kuwavizia Waluvu mashambani; kupata kuwakamata mateka ao kuwaua.

Bassi bwana mkubwa huyu akaita majumbe wake wa Kizigua, nusu wakaja, wangine hawakuja kwa sababu mbali mno naye hakukaa sana, bassi ulikuwa mkutano mkubwa sana na mashauri mengi, na killa mwenyi neno lake la masa akaja na kushitakiana hapa. Wajua kama Waluvu hawapatani na Wazigua bassi Wazigua wakija kwa kuitwa na Mdachi, Waluvu wakawa na hofu sana wakajifunga mjini Korogwe, Wakasema watu hawa wanatuua sisi siku hizi zote, Mdachi amewaita na hatujui shauri lao nini wawaitalo, nao wakanyage mji wetu hatukubali, wasema hivi wasipofikiri na kujua kama wanagombewa wao, na kufanyiwa amani. Walikuwa na moyo uliopunguka kabisa, bassi mimi haenda mjini wakaniambia habari ile, hatutaki Wazigua kupita mjini mwetu ao kulala humu, hawaambia vema, lakini twendeni kwa bwana mkubwa mkiweza, ndiye aliyewaita Wazigua nao hawana buddi kuja alipo Mdachi.

Bassi nikawaleta kwa bwana mkubwa, wakasema kwa woga woga hapo, naye akawaambia msiogope nimewaita, nitatengeneza yote, nao hawatalala mjini mwenu, watalala pamoja nasi hapa Tanga, nao wajapo wakitaka kuvuka ondoeni malalo mpaka nilete asikari awatangulie hatta hapa Tanga - Bondei. Wakapata moyo wakaenda zao mjini tukamweleza habari zote kama tulizojua alizotaka kuzijua bwana mkubwa habari ya watu, na hali ya watu, na namna yao, mimi na Padre tulikuwapo hapo.

Siku ya pili assubui akaenda kupiga nyama akarudi alasiri ndipo ikawa mashauri, nasi tulikuwapo baada ya mashauri kuona watu wajao kushtakiana.

MSIMULIZI. 629

Oct. 20, siku hii ya Alhamisi twalifanya furaha tukakarimiwa siku kuu ndogo ya kufungua nyumba. Tukafanyiza karamu ikapikiwa mle nyumba mpya. Watoto wetu na watu wachache wa nje, na watu waliojenga nyumba tangu mwanzo hatta kwisha wakakaribishwa karamuni na wakapewa kiinua mgongo chao. Bunduki nyingi zilipigwa siku hiyo, na alasiri, watoto na sisi tukaenda uwanja wa mpila wakakimbilia zawadi &c., na kunyang'anyia mapesa na watoto wa nje pia walikuja tukajifurahisha sana siku hiyo.

November 1. Siku kuu ya Watakatifu wote tukaenda zetu mto Ulwengela kushinda kule na vyakula vyetu, na kondoo wa kuchinja kwa kitoweo, watoto wote wa hapa na nusu wa nje mji Korogwe na vijana vya humu mjini 3. wawili ndio wafundishwao hapa, pamoja na mimi na John L. Mwaimu, Padre hakwenda. Tukajifurahisha sana huko kwa kupiga ndege, na kufukuza nyama ziiwazo ntohe na michezo ya kupata zawadi za mapesa, huko tuliua nyoka wawili wakubwa sana, mmoja nyikani tulikokwenda, akapigwa bunduki na kijana aitwaye Abdallah, na mwingine wakati tukirudi kama saa kumi unusu tukamwona njiani atujia huku tuliko tukachoma moto majani alipoingia, kutokea tu yalinitoka hampata nazo za shingo akaingia majanini tukachoma moto tena, kumbe akauungua tukamwona. Wa kwanza aitwaye moma mzee huyo magamba tu yanamparuzi kama miba, na wa pili mkubwa kwa urefu, aitwaye kwarara. Tukarudi kwa kuimba na furaha sana hatta mjini kwetu hapa. Sasa huku watu wa inchi wanaanza kulima tayari kwa mvua ikinya wapande mtama wasipate kuchelewa kama mwaka ule wa jana wakafanyiza upumbafu wa kunywa pombe ya mtama dayima mwisho wakachelewa hatta kulima na balaa li miangoni. Illa miezi hii jua kali sana nyika zimeungua pia.

MSIMULIZI. 630

October 18 Juma a nne ilikuwa siku kuu ya Luka Mwanjilisti tulikarimiwa na Padre wetu siku kuu ya siku nzima. Assubui mbele ya Siri Tak: ilikuwa kufanyia mtoto wetu mmoja mwanafunzi, mtoto wetu mmoja wa kwanza wa Mission hapa jina lake Nyarige, mwana wa jumbe Vulu, sasa tuna watoro waliofanywa waanafunzi, kupewa misalaba, watano mmoja ameacha Missiori kwenda kaa kwao, aitwa Magola illa aja kuabudu Muungu killa juma apili.

Baada ya sala ya kufanywa uanafunzi: Siri Tak: na sala ya pili ya assubui ndio tukaenda kuzindua nyumba mpya yangu, Ni hivi: Padre na mimi tulivalia mavazi ya kanisani na watoto mbele wakitembea wawili wawili, na mmoja ametangulia mbele akishika msalaba, na watu 3 wafundishwao wa mji Korogwe pia walikuja, Chamdoma Abdallah, Mwangilo, na watoto wa nje pia walikuja wengine kwa sala hii na kufanywa uanafunzi. Tukikaribia nyumba kwa kuimba, tukazunguka nyumba yote, halafu tukaingia nyumbani, na kuimba Zaburi 15, ("Nani atakaye kaa katika masikani yako,") na sala zikasemwa za kuibariki nyumba na wakaao humo pia, ilipokwisha hivi tukatoka, na baadaye bunduki zikalia za furaha hatta watoto wakapiga pia. Siku ile ile twaona safari ya Wadachi na askari; na jumbe Mambo-Sasa wa Pangani na watu wake, Wadachi watatu, wakatua kambini ya Tanga Korogwe.

Shauri lao nini? wamekuja kuhukumu Wazigua wapiganao huko juu Uzigua, jumbe Mdami na jumbe mngine aitwaye Sampa mwana wa Mwabutu, na huyu asayidiwa na watu wa jumbe Mambo-Sasa Wa Bweni, Pangani, kwani ni jamaa zao; tena kuwafanyia hukumu kati ya Wrizigua na Waluvu.

MSIMULIZI. 631

**NANYANGA (KWA LIUMANGA.)**

Salaam kwa Mtengenezaji wa Msimulizi. Baada ya salaamu, nitajaribu kukueleza habari za hapa. Na habari za hapa ni mbaya sana siku hizi. Tuseme kwanza habari za taabu yetu hiyo ndio ya siku zote, mwajua kama jua ndio taabu yetu. Tena mkiangalia mnamo Msimulizi wa mwezi wa December. Mtaona habari za furaha, ndio nyama ya nyati. Baasi kunako Nov. 26, Juma mosi, nalienda Newala kwa Chakula kile cha Roho. Bassi juma apili ilikuwa Pombe ya kukata msitu hapa petu. Nao baada ya kunywa waanza kubishana kwa mambo zamani waliyokwisha kusameheana. Bassi kijana mmoja jina lake Sulimani akasema, "Wewe walikuwa unatukana vibaya, na bibi yangu analima karibu yenu Bassi nyie leo mmekuja katika pombe yangu bassi miye pembe hii sitaki tena, naenda zangu," akaenda zake. Kumbe kule kwenda si bure illa anakwenda kutafuta jambo la kuharibu. Akaenda akatwaa bunduki yake, akaenda akawavizia njiani. Nao wale pombe hawakunywa, walipomwona mwenyewe amekasirika wakashika njia ya kurudi kwao. Kumbe mwenzao umejiweka tayari na bunduki mkononi. Na walipokaribia akapiga bunduki na risasi zikampiga za kitovu akaanguka pale pale mkavu. Bassi nao vijana wanatoka mji mmoja uitwao Njaru. Wala si adui wa yule kijana aliyepigwa bunduki, wakamtia mikononi wakamfunga, pamoja na bibi yake wakampeleka kwake jamaa yao kijana aliyekufa. Na Bibi ana mtoto mchanga aliyezaliwa kama siku themintashara tu asiyeacha kunyonya. Bassi mtoto amebaki kwa babuye, mama na mumewe wafungwa. Na yule mume akachinjwa,

MSIMULIZI. 632

akabaki mkewe. Nao adui hawamwonei huruma yule mtoto. Nao baada ya kamchinja yule kijana, wakaenda mji wa jamaa yake yule kijana uitwao Chihembe wakautia moto, tena watu watatu wakauawa na watatu tena waliojeruhi kwa ajili ya jamaa aliyekufa. Na tena mateka wengi wameleta, ndio mbuzi na vitu vinginevyo. Bassi nao wao husema Njaru tuwekeeni tayari, kwa nini nyinyi mmemkamata Sulimani, na bibi akachinjwa kama achinjwavyo kuku, walla sisi ninyi hatuna hatiya nanyi wangemkamata wenyi jamaa yao aliyepigwa bunduki ina haki. Bassi huku pande zote za Makonde ni machafuko kabisa na watu wa Njaru hulala msituni. Na mbuzi zao zimewekwa petu. Na November 28, nikarudi hapa pangu.

Dec. 2, Mwenyewe Liumanga amewakusanya Wamakonde wote waliopigana tayari kwa hukumu na kuwaambia amani. Hatta nimethubutu kwa mkutano huu kutoa maneno machache.

Na maneno yenyewe ndio haya. Nikawaambia. "Ginsi gani enyi Wamakoude mbona mwafanya hivi? Sisi Waalimu tumekuja katika inchi yenu si bure, illa tuwaambie maneno yaliyofichwa kwenu msioyajua kwa asili yenu, ni Neno la Muungu. Nanyi hamtaki yetu, mnasikia kengele inalia "Lidua lake Mlungu" wala ninyi hamji kwa nini? "Kule ndio kupata amani na yote yalio mema." Nami nikanyamaza kwani nikaona nianze mimi maneno kidogo, na halafu yake maneno yakafanyika, mzee akaamua akakata maneno.

Nov 24, tumeanza kubomoa nyumba yetu na kuanza tena kujenga mpya Nov. 21, akatuasilia Padre wetu akaaye Masasi. Ndiye W. C. Porter akashinda, Nov. 25, akaenda zake Masasi akapita Newala. B.M.

MSIMULIZI. 633

**LIKOMA.**

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Nasikitika sana, kwa sababu habari zangu nilizokuandikia hazikukufikia, ao zimepotea njiani sijui. Mwezi wa Dec. Nalikuambia habari za Chizumulu juu ya vita. Tena nalikuambia bado haijaisha. Najaribu tena kukueleza. Ilipokwisha vita ile, watu wakubwa wakubwa walifanya shauri, waone nani amekosa? nani asiyekosa? Kosa likaonekana kwa Mataka. Mataka anachukua mbuzi kumpa Ambuluma. Tena Mbuluma alikuwa na watu wake wawili, nao wote hao walikuwa wakikaa kwa Mataka kabla hawajakoseana. Mataka alipokwisha kumlipa Mbuluma mbuzi akasema nirudishie na wale watu wangu wawili. Mataka akasema mimi watumwa siwarudishi hatta kidogo. Na huyu Mataka mbuzi zake zingine zinakaa kwa Mbuluma. Mbuluma asema mbuzi zako zote nitazila, kama hunilipi watumwa wangu. Mataka asema kama hunipi mbuzi zangu, itakuwa tena vita kama kwanza. Itakwisha lini sijui.

Sept. 18, Watu wa Makulawe na wa Kukuyu walitaka kupigana. Sababu watu wa Makulawe walipigana wao kwa wao, mmoja wao alivunjwa mguu kwa jiwe. Bassi kwa siku kathawakatha alikuwa hawezi. Mtu mwenyewe aliyevunjwa mguu jina lake Apondeo. Bassi panapo Sept. 17, Apondeo akafa. Watu wale waliomvunja mguu walipoona amekufa wakaondoka mjini pale, wakaenda mwingine wakakaa, mji wenyewe wanaokaa hawa watu waitwa Kukuyu. Watu wengine waliosalia pale mjini, wakasema twende nayo vita kwa mji ule. Nao wakafika kwa Malokotela mkuu wa mji. Watu wa Makulawe wakamtuma mjumbe kwenda Chiponde, Kungani,

MSIMULIZI. 634

Mvumu, kuwaita watu waje wasayidie kupigana. Wangine wao walikubali kuja kuwasayidia, na wangine walikataa. Wale waliokubali wakafuatana na mjumbe, njiani walipokuwa wakienda, wale watu wakamkimbia mjumbe. Mjumbe akajirudia kwao Makulawe, hawakupigana.

Sept. 27, Alikuwa mfalme aitwa Malipa, kusudi hilo hilo la vita awasayidie watu wa Kukuyu, lakini aliambiwa na Malokotela, hapana vita; siku ile ile alirudi kwao ng'ambo.

Sept. 18, Mwalimu Daudi B. na watu wangine walikuja humu Likoma, kusema bwana Johnson hawezi sana, kula hali, kusema hasemi. Bahati yetu Domira ilikuwapo hapa, kwani mtumishi wetu Oharles Janson alikuwa haijaisha kutengenezwa. Bwana Archdeacon aliingia upesi katika Domira, pamoja na Mr Crouch, siku hiyo ilikuwa Juma apili, Usharika Mt. haukufanyika, kwani bwana Archdeacon aliharakia Msumba amwone bwana Johnson. Jioni bwana kufumba na kufumbua twamwona Mr Johnson kaisha fika. Angefika mchana, lakini pepo zikamsukuma mpaka Chizumulu. Jioni saa thenashara Domira ikafika hapa. Ikawa furaha sana kumwona Mr Johnson.

Oct. 5, Watu walifanya ghasia sana, kwa kunyweshana pande (kitu kama sumu), kwa ajili ya Robert Kamtimbati, yule aliyekufa mwaka wa 1891. Naye alibatizwa na bwana Frere. Nao Walionyweshana ni hawa Kapolomuji na Ngoza, huyu Ngoza alikuwa mwanafunzi. Bassi katika kunyweshana kwao, hawakunywa wao wenyewe, illa walizinyweshwa mbwa. Jioni mbwa wa Ngoza alikufa, ikawa shangwi sana, ndio ishara ya kuwa Ngoza kweli alikuwa mchawi, ndiye aliyemwua R. K. Jioni saa tatu akafa

MSIMULIZI. 635

mbwa wa Kapolomuji, tukaisikia kimya, wala ngoma haikupigwa. Na yalikuwapo maneno wao kwa wao, wengine wakasema wote wawili walikuwa wachawi. Mwisho wa maneno haya Kapolomuji na Ngoza, wamechukua mbuzi wawili kumlipa Mngona kwani alikuwa jamaa yake Robert K. Ngoza alimrudishia bwana Archdeacon msalaba wako, kwani aliambiwa aurudishe.

Wangoni walitoka kwao na majeshi yao, wakashika njia ya Kuunangu. Walipofika kule, waliwakuta watu wako mashambani wanalima, kwani ilikuwa Assubui. Wakakamata watu, wengine wakauawa, wakaenda zao. Waliposikia wa mjini kama Wangoni walikuja na wamekamata watu, wakawafuata Wangoni. Jioni waliwakuta wamelala. Na wale Wayao hawakuwaendea upesi, lakini walilala. Usiku uleule Wayao waligawanyikana vikosi vitatu, marra hiyo waliwazunguka Wangoni, wakapiga bunduki pamoja (mzakulo). Wangoni walipoona kote kote wamewazungukwa, wakakimbia, wengi walipata majeraha. Wengine wakafika Kumanda, pale wakaapo wazee wake Mwalimu Yohana, wakangojea kupona majeraha yao. Mtambilika yule mkubwa wao asema ataleta majeshi mengi kupita yale ya kwanza waende tena Kuunangu kucheza nao. Na wengine walikwenda Kwizombe wakakamata watu wakaenda nao kwao, wenzao waliwafuatia mpaka kwao, wakapigana nao, Wangoni wengi waliuawa. Wayao wakarudi kwao Kwizombe. Pale nyuma wangoni walikusanyana, wapate kuwafuata, lakini hawakuwafikia wakarudia njiani.

Oct. 15, ilifika sitima ikitoka pande za chini Baharini s.s. Charles Janson na s.s. Domira walishindana, wapi bwana s.s. Charles Janson akawa wa



MSIMULIZI. 636

kwanza kufika Monkey Bay, walimkuta ameisha tia nanga. Walifika watoto hawa Manfred, Kufamaka. Watoka pa Chia. Wangoni wengine wako Msumba, kugoangoa mihogo ya watu. Na Mngoni mmoja alikuwa akikaa Msumba, usiku walikuja wenzake kumchukua. Na watu wa Msumba wanathani labuda vita itakuja, kwa nini wamemchukua mwenzao.

Oct. 18, Siku kuu ya Luka Mwanjilisti Stima ilikwenda pa Utonga pamoja na waana chuoni saba ndio hawa: Tito, Mattiya, William, Martin, Herbert, George, Yoel, walichukua na mpira kwenda kushindana nao. Watoto wa Utonga walifungwa 16, kwa moja lao. Sitima ikafika mpaka Kungoffi, Mr. Johnson ikamwacha kule na mtoto mmoja, Kavundula.

Oct. 19, Sitima ilikwenda Chizumulu pamoja na bwana Archdn. Siku ileile ikapita Kungoffi kumchukua Mr Johnson, ilimchukua mkewe mwalimu So pia, naye yuko hapa. s.s. Domira ilifika hapa Oct. 18, usiku saa tatu. Ikaondoka hapa Oct. 19, usiku.

Oct. 23, nyumba 11 zimeungua moto. Lakini viti vingi vimeokoka. Watu wa Mbamba na wa Kungani walikuja kutusayidia. Na school ile mpya sasa ndio kanisa letu upande mwingine, school na upande mwingine kanisa. Watoto wangine wamekwenda zao kwani hapana nafasi.

Oct. 26, Stima imekwenda Kungoffi, pamoja na Annie H. Songolo. Makanjila asema atavunja miji hii. Msumba, Pachia, Chisanga, sijui kama atakuja kweli ao uwongo wake.

Nov. 5, nyumba zetu zaliungua marra ya pili. Wakati ulipoanza moto sisi tulikuwa kanisani, tukasikia moto! moto! moto! tukatoka nje wote tuangalie nyumba ya Charles Nasibu inawaka moto. Vitu vyote

MSIMULIZI. 637

vikachukuliwa. Moto ukaendelea hatta kwenyi nyumba za mabibi.

Nov. 9, s.s. Charles Janson yampeleka Miss Fountaine Bandawe, akae huko hatta zitakapokwisha kujengwa nyumba. Mabibi wawili waja huko. Wanawake watoto wa chuoni walikwenda zao siku ile ile.

Nov. 6, Stima ilifika hapa ikitoka pande za chini, pia amefika Albano Mwanzo, yule aliyekwenda kuwatazama jamaa zake. Naye ameniarifu habari kidogo za kule. Walipokuwa wakipita karibu sana na Makanjila, wakawaona watu wamekaa mchangani. Wakatwaa darubini Wakatazama, wakaona mashua ile ya Balози Johnston iko paangoni wameificha. Mashua yenyewe waliichukua wakati ule ule walipokuwa wakipigana. Marra walipoiona stima wakaanza kukimbia. Stima ikasimama ikawa katika kupakia kuni, marra hiyo watu wengi wa Makanjila wakatoka mijini, wakaanza kuranda mchangani. Stima ikaendelea hatta Monkey Bay, ikafika majira ya jioni. Stima ikafika hatta Mkope. Wakathani wataikuta mashua ile Ousel na mizigo, lakini haikuwapo mizigo wakajirudia Monkey Bay. Nyumba nyingi za Kungoffi zimeungua moto, na Chisanga pia zimeungua. Na zilizoungua Msumba zapata 100. Na mtu huyo aliyechoma moto jina lake Akanda. Ng'Ombe zake wamemnyang'anya. Mfalme mmoja wa Ng'Ambo, jina lake Mkongojo, tangu siku nyingi amekuwa hawezi ugonjwa wa wazimu, amefungwa panda, chakula hali. Watu wengi wamemtafutia dawa, wala hapana aliyomfaa. Pana mtu wa Chizumulu alikwenda Kumochu usiku, marra akakamatwa akafungwa kongwa kubwa sana. Mfalme Mkumpa akachukua vita kwenda nayo kwa wale waliomfunga Chapema. Watu wa Kumochu wakakimbia, kwani wenzi wao walikwenda

MSIMULIZI. 638

Kumalawi (Msumba). Kosa lilimwangukia Chapema. Twatumaini zikiisha jengwa nyumba tutapata watoto wengi kama kwanza. Kwani watoto wengine tumewapunguza kwa sababu school yetu haina nafasi.  
A. T. M.